# ATHARI ZA MOFU AMBISHI NA NYAMBULISHI KATIKA UUNDAJI WA VITENZI VYA KISAMBAA

**NASRA HABIBU ALLY**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KWA MADHUMUNI YA**

**KUKAMILISHA SHAHADA YA UZAMIVU YA ISIMU (PhD)**

**IDARA YA LUGHA NA TAALUMA ZA FASIHI**

**KATIKA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2020**

# UTHIBITISHO

Waliotia sahihi hapa chini wanathibitisha kwamba wameisoma kazi hii yenye mada: **"Athari za Mofu Ambishi na Nyambulishi katika Uundaji wa Vitenzi vya Kisambaa"** na wanapendekeza ikubaliwe kwa utahini wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ili kukamilisha masharti ya kutunukiwa shahada ya Uzamivu ya Isimu ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

……………………………………

Dkt. Anna M. Kishe

(Msimamizi)

………………………………

Tarehe

………………………………..

Dkt. Nestory N. Ligembe

(Msimamizi)

……………………………..

Tarehe

## TAMKO

Mimi, Nasra Habibu Ally, ninathibitisha kuwa tasnifu hii ni yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa na wala haitawasilishwa katika chuo kikuu kingine kwa ajili ya mahitaji ya kutunukiwa shahada kama hii au nyingine yoyote.

………………………………..
Saini

…………………………….
Tarehe

## HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kuhifadhi kwa mfumo wowote ule au kutoa kivuli japo sehemu ndogo ya tasnifu hii kwa njia yoyote bila idhini ya maandishi ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania isipokuwa kwa shughuli halali, kwa ajili ya utafiti, kujisomea au kufanya marejeo ya kitaaluma.

## TABARUKU

Kazi hii ninaitabaruku kwa wazazi wangu kwa malezi na elimu waliyojitahidi kunipatia kwa kadri ya uwezo wao. Nimekuwa jasiri na mvumilivu kutokana na misingi mikubwa ya maisha waliyonipatia.

## SHUKURANI

Kwanza kabisa, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuvuka kila hatua niliyoivuka, naamini si kwa uwezo wangu pekee bali kwa nguvu zake zisizo na mipaka nimeweza kuikamilisha kazi hii. Kazi hii ya kitaaluma ni kazi ambayo nisingeweza kuikamilisha bila kuwepo misaada ya watu mbalimbali. Nawashukuru wote kwa michango yao mikubwa kwani huenda ningekata tamaa ya kusonga mbele. Si rahisi kuwashukuru kwa kuwataja wote kwa majina, nitawataja wachache kwa niaba ya wengine.

Aidha, ninawashukuru wasimamizi wangu Dkt. Anna Kishe na Dkt. Nestory Ligembe ambao hawakuchoka kuniongoza tangu pendekezo la utafiti, utafiti wa uwandani hadi kufikia uandishi wa ripoti ya utafiti huu. Bila kuwepo kwa mchango wao wa kunilea kitaaluma kwa kuisoma kazi na kuirekebisha mara kadhaa isingeweza kukamilika. Pia, ninaushukuru uongozi wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa kunipa udhamini uliofanikisha masomo yangu ya Uzamivu. Nawashukuru pia watoa taarifa ambao walinivumilia sana kwa kuacha shughuli zao na kukubali kutoa taarifa zilizohitajika. Nawashukuru pia wanaidara na wafanyakazi wenzangu wa kituo cha Mkoa Iringa, wamenisaidia kuvuka pale nilipokwama.

Vilevile, ninawashukuru wazazi wangu na ndugu zangu wote walionihamasisha na kunitia nguvu niikamilishe shahada ya Uzamivu. Bila kumsahau mume wangu Hassan Suleiman na wanangu kwa kunitia moyo na kunivumilia. Kwa hakika muda mwingi nilikuwa ninayaacha majukumu ya kifamilia ili niweze kukamilisha kazi hii.

## IKISIRI

Utafiti huu umechunguza na kuchanganua kuathiriana kwa mofu ambishi na nyambulishi katika uundaji wa vitenzi vya Kisambaa. Katika uchunguzi na uchanganuzi huo, utafiti huu pia umedhihirisha mashartizuizi yanayotawala uambikaji wa mofu katika kitenzi cha Kisambaa. Uchambuzi na uwasilishaji wa data, katika utafiti huu umefanywa kwa kuongozwa na Nadharia ya Umbo Upeo iliyoasisiwa na Prince na Smolesky. Data za utafiti huu zilikusanywa kutoka tarafa ya Mlalo Wilaya ya Lushoto, maeneo ambako Wasambaa wanapatikana. Data hizo zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usaili na usomaji wa maandiko. Utafiti huu umebaini kuwa mofu ambishi na mofu nyambulishi zinapoambikwa katika mzizi wa kitenzi cha lugha ya Kisambaa zinaathiriana. Kuathiriana huko kumebainishwa kwa kuzingatia mashartizuizi yanayotawala mfuatano na mpangilio wa mofu katika kitenzi cha Kisambaa. Mofu ambishi na nyambulishi ambazo huathiriana ni pamoja na mofu ya mofimu ya njeo, ukanushi, masharti, kutendea, utendeshi, ufanyikaji sana, kutendeka na mofu ya mofimu ya urejeshi. Mofu hizo huathiriana katika kudondoshwa kwa mofu, kubadili nafasi ya utokeaji wa mofu na kubadilika kwa umbo la mofu inayoathiriwa pale zinapokaa pamoja kuunda kitenzi chenye maumbo mbalimbali yanayokubalika katika Kisambaa. Matokeo ya kuathiriana huko ni kupatikana kwa maumbo mbalimbali ya vitenzi yenye fahiwa tofauti tofauti. Maumbo hayo ya vitenzi yenye mabadiliko ni kama vitenzi vyenye ukanushi, masharti, vitenzi katika hali ya kutendwa, kutendea, urejeshi na utendeshi. Aidha, utafiti huu unapendekeza kuwa tafiti nyingine katika lugha ya Kisambaa kuhusu maumbo ya vitenzi na namna mofu zinavyoweza kuathiriana kisemantiki na kisintaksia zinahitajika. Vilevile kuna haja ya kuzitafiti zaidi lahaja katika lugha ya Kisambaa. Pamoja na hayo suala la toni katika lugha ya Kisambaa ni muhimu litafitiwe kwa kina.

# YALIYOMO

**UTHIBITISHO** .......... ii
**TAMKO** .......... iii
**HAKIMILIKI** .......... iv
**TABARUKU** .......... v
**SHUKURANI** .......... vi
**IKISIRI** .......... vii
**YALIYOMO** .......... ix
**ORODHA YA MAJEDWALI** .......... xiii
**ORODHA YA ALAMA NA VIFUPISHO** .......... xvi
**SURA YA KWANZA** .......... 1
**UTANGULIZI WA JUMLA** .......... 1
1.1 Utangulizi .......... 1
1.2 Asili ya Wasambaa na Lugha Yao .......... 1
1.2.1 Lahaja katika Lugha ya Kisambaa .......... 3
1.2.2 Athari ya Kiswahili katika Lugha ya Kisambaa .......... 6
1.3 Usuli wa Tatizo la Utafiti .......... 7
1.4 Tatizo la Utafiti .......... 12
1.5 Malengo ya Utafiti .......... 13
1.5.1 Lengo kuu .......... 13
1.5.2 Malengo Mahususi .......... 14
1.6 Maswali ya Utafiti .......... 14
1.7 Umuhimu wa Utafiti .......... 14
1.8 Mipaka ya Utafiti .......... 16

1.9 Changamoto katika Utafiti huu ....... 16

**SURA YA PILI ....... 18**

**MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA ....... 18**

2.1 Utangulizi ....... 18

2.2 Mofu na Mofimu katika Umbo la Kitenzi ....... 18

2.3 Mapitio ya Tafiti Mbalimbali katika Lugha za Kibantu ....... 26

2.3.1 Mofu Ambishi na Mofu Nyambulishi katika Lugha ya Kisambaa ....... 26

2.3.2 Mofu Ambishi na Mofu Nyambulishi katika Lugha Nyingine za Kibantu ....... 33

2.3.3 Kuathiriana kwa Mofu katika Vitenzi vya Lugha za Kibantu ....... 39

2.4 Pengo la Utafiti ....... 44

2.5 Kiunzi cha Nadharia ....... 44

2.6 Muhtasari wa Sura ....... 55

**SURA YA TATU ....... 57**

**MBINU ZA UTAFITI ....... 57**

3.1 Utangulizi ....... 57

3.2 Muundo wa Utafiti ....... 57

3.2.1 Eneo la Utafiti ....... 57

3.2.2 Walengwa wa Utafiti ....... 58

3.2.3 Sampuli na Usampulishaji ....... 59

3.3 Mbinu za Kukusanyia Data ....... 62

3.3.1 Mahojiano ....... 62

3.3.2 Upitiaji Nyaraka ....... 64

3.4 Uchanganuzi wa Data ....... 64

3.5 Maadili ya Utafiti ... 65

3.6 Uthabiti na Ukubalifu wa Utafiti ... 67

3.7 Muhtasari wa Sura ... 68

**SURA YA NNE ... 69**

**UCHAMBUZI, UWASILISHAJI WA DATA NA MJADALA**

**WA MATOKEO ... 69**

4.1 Utangulizi ... 69

4.2 Mofu na Mofimu katika Kitenzi cha Kisambaa ... 69

4.2.1 Mofu Ambishi katika Kitenzi cha Kisambaa ... 70

4.2.2 Mofu Nyambulishi katika Kitenzi cha Kisambaa ... 75

4.3 Kuathiriana kwa Mofu katika Kitenzi cha Kisambaa ... 79

4.3.1 Kuathiriana kwa Mofu Ambishi katika Kitenzi cha Kisambaa ... 85

4.3.1.1 Mofu ya Nafsi katika Kitenzi Yakinishi ... 85

4.3.1.2 Mofu ya Nafsi katika Kitenzi Kanushi ... 91

4.3.1.4 Mofu ya Njeo katika Kitenzi Kanushi ... 112

4.3.1.5 Mofu ya Masharti katika Kitenzi Yakinishi ... 120

4.3.1.6 Mofu ya Masharti katika Kitenzi Kanushi ... 122

4.3.1.7 Mofu ya Ujirejezi katika Kitenzi Yakinishi ... 125

4.3.1.8 Mofu ya Ujirejezi katika Kitenzi Kanushi ... 127

4.3.2 Kuathiriana kwa Mofu Nyambulishi ... 129

4.3.2.1 MASHA-ZU ya Mfuatano wa Mofu ya Utendea na Utendwa ... 132

4.3.2.2 MASHA-ZU ya Mfuatano wa Mofu ya Utendea na Kutendana ... 134

4.3.2.3 MASHA-ZU ya Mfuatano wa Mofu ya Utendeshi na Utendea ... 136

4.3.2.4 MASHA-ZU ya Mofu ya Urejeshi katika Kitenzi cha Kisambaa ... 139

4.3.2.5 MASHA-ZU ya Mfuatano wa Mofu ya Utendwa na Urejeshi ................ 143

4.3.2.6 MASHA-ZU ya Mfuatano wa Mofu ya Utendea na Urejeshi ................ 145

4.3.2.7 MASHA-ZU ya Mofu ya Ufanyikaji sana na Utendwa ................ 148

4.3.2.8 MASHAZU ya Mfuatano wa Mofu ya Utendeshi na Kutendana ................ 150

4.3.2.9 MASHA-ZU ya Mfuatano wa Mofu ya Utendeshi, Utendea na Kutendana ................ 152

4.4. Muhtasari wa Sura ................ 155

**SURA YA TANO ................ 156**

**MUHTASARI WA MJADALA, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ................ 156**

5.1 Utangulizi ................ 156

5.2 Muhtasari wa Mjadala wa Utafiti ................ 156

5.3 Hitimisho ................ 163

5.4 Mapendekezo ................ 166

**MAREJEO ................ 168**

**VIAMBATANISHO ................ 178**

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 2.1: Mofu katika Umbo Neno .......... 22

Jedwali 2.2: Alomofu za Mofimu ya Kutendwa katika Kiswahili .......... 22

Jedwali 2.3: Uambishaji wa Mofu katika Mzizi wa Kitenzi .......... 24

Jedwali 2.4: Unyambulishaji wa Mofu katika Mzizi wa Kitenzi .......... 25

Jedwali 2.5: Mofu Ambishi katika Kitenzi cha Kichuka .......... 34

Jedwali 2.6: Mofu Nyambulishi katika Kitenzi cha Kikinga .......... 38

Jedwali 2.7: Athari ya Mofu Njeo katika Kitenzi cha Shimalila .......... 40

Jedwali 2.8: Athari za Viambishi Nyambulishi Kisintaksia .......... 41

Jedwali 2.9: Umboghafi oa .......... 52

Jedwali 4.1: Mfuatano wa Mofu katika Lugha za Kibantu .......... 70

Jedwali 4.2: Mofu Ambishi katika Kisambaa .......... 71

Jedwali 4.3: Mofu Nyambulishi katika Kitenzi cha Kisambaa .......... 75

Jedwali 4.4: Mofu Nyambulishi katika Kitenzi cha Kisambaa .......... 76

Jedwali 4.5: Mofu Nyambulishi Zinavyounda Kitenzi cha Kisambaa .......... 78

Jedwali 4.6: Kuathiriana kwa Mofu katika Kitenzi cha Kisambaa .......... 80

Jedwali 4.7: Seti ya MASHA-ZU. Umboghafi: nitajata ‘ninatembea’ .......... 87

Jedwali 4.9: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: Siighae ‘Sikupeleka’ .......... 93

Jedwali 4.10: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: ketiighae ‘hatukupeleka’ .......... 95

Jedwali 4.11: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: kuighaa ‘hupeleki’ .......... 97

Jedwali 4.12: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: kemuighae ‘hamkupeleka’ .......... 98

Jedwali 4.13: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: kaighaa ‘hapeleki’ .......... 99

Jedwali 4.14 : Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: kewaighaa ‘hawapeleki’ .......... 101

Jedwali 4.15: Mofu ya Wakati Uliopo katika Kitenzi Yakinishi .......... 104

Jedwali 4.16: Seti ya MASHA-ZU. Umboghafi: Atashenga ‘Anakata’ .................105
Jedwali 4.17: Mofu ya Wakati Uliopita katika Kitenzi Yakinishi ..........................106
Jedwali 4.18: Seti ya MASHA-ZU. Umboghafi: mzabua ‘mlifika’ .......................107
Jedwali 4.19: Seti ya MASHA-ZU. Umboghafi: muidosize ‘mmefuata’ ...............109
Jedwali 4.20: Mofu ya Wakati Ujao katika Kitenzi Yakinishi ..............................110
Jedwali 4.21: Seti ya MASHA-ZU. Umboghafi: newaghue ‘watachukua’ ............111
Jedwali 4.22: Mofu ya Njeo ya Wakati Uliopo katika Kitenzi Kanushi.................114
Jedwali 4.23: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: ketishezigha ‘hatuchezi’ .............114
Jedwali 4.24: Mofu ya Njeo ya Wakati Uliopita katika Kitenzi Kanushi..............116
Jedwali 4.25: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: kewatozize ‘hawakushika’ .........117
Jedwali 4.26: Mofu ya Njeo ya Wakati Ujao katika Kitenzi Kanushi ....................118
Jedwali 4.27: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: kewauye ‘hawatarudi’ ................119
Jedwali 4.28: Mofu ya Mofimu ya Masharti katika Kitenzi Yakinishi ..................120
Jedwali 4.29: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: wakiima ‘wakilima’.....................121
Jedwali 4.30: Mofu ya Mofimu ya Masharti katika Kitenzi Kanushi.....................123
Jedwali 4.31: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: akisheshama ‘asipohama’............124
Jedwali 4.32: Maumbo ya Vitenzi vyenye Mofu ya Ujirejezi ................................125
Jedwali 4.33: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: muzakieta ‘mlijileta’ ...................126
Jedwali 4.34: Mofu ya Mofimu ya Ujirejezi katika Kitenzi Kanushi.....................127
Jedwali 4.35: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: ketikifishiye ‘hatujajificha’ .........128
Jedwali 4.36: Mofu Ambishi na Nyambulishi katika Umbo la Kitenzi..................129
Jedwali 4.37: Mofu Nyambulishi ya Utendea Kuathiri Mofu ya Utendwa ............132
Jedwali 4.38: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: doewa ‘gusiwa’ ..........................133
Jedwali 4.39: Mofu Nyambulishi za Mofimu ya Utendea na Kutendana ...............134

Jedwali 4.40: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: ashiana ‘tupiana’ ......................... 135

Jedwali 4.41: Mfuatano wa Mofu ya Utendea na Mofu Nyambulishi Nyingine..... 137

Jedwali 4.42: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: waaghuushia ‘wanafukuzia’........ 138

Jedwali 4.43: Mofu ya Mofimu ya Urejeshi Kuathiri Mofu Ishilizi........................ 139

Jedwali 4.44: Mofu ya Njeo na Mofu Nyambulishi ya Urejeshi ............................. 140

Jedwali 4.45: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: ashungiyeye ‘aliyefunga’ ............ 142

Jedwali 4.46: Mofu ya Utendwa na Mofu ya Urejeshi ............................................ 143

Jedwali 4.47: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: Waghosholwewo ‘Waliotengenezwa’ .......................................................................... 144

Jedwali 4.48: Mofu ya Utendea na Mofu ya Urejeshi ............................................ 146

Jedwali 4.49: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: nishengeeye ‘niliyekatia’............. 147

Jedwali 4.50: Mofu ya Ufanyikaji sana na Utendwa ............................................... 148

Jedwali 4.51: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: shengeshwa ‘katwa sana’ ............ 149

Jedwali 4.52: Mofu ya Utendeshi na Utendwa ....................................................... 150

Jedwali 4.53: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: kinyana ‘angushana’.................... 151

Jedwali 4.54: Mofu ya Utendeshi, Utendea na Kutendana..................................... 152

Jedwali 4.55: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: hozeana ‘pozeana’ ....................... 153

# ORODHA YA ALAMA NA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| → | Inajitokeza kama |
| / | Katika mazingira ambapo |
| ☆ | Si sahihi |
| {- -} | Unukuzi wa mofu |
| /-/ | Unukuzi wa alomofu |
| ( ) | Maelezo ya msaada au ufafanuzi wa ziada |
| + | Ikifuatana na |
| — | Mpaka wa mofu |
| Mz | Mzizi |
| MASHA-ZU | Mashartizuizi |
| Knsh | Ukanushi |
| Nfs | Nafsi |
| Nj | Njeo |
| $M_i$ | Mofu ishilizi |
| $Nfs_{1U}$ | Nafsi ya kwanza umoja |
| $Nfs_{1W}$ | Nafsi ya kwanza wingi |
| $Nfs_{2U}$ | Nafsi ya pili umoja |
| $Nfs_{2W}$ | Nafsi ya pili wingi |
| $Nfs_{3U}$ | Nafsi ya tatu umoja |
| $Nfs_{3w}$ | Nafsi ya tatu wingi |
| $Wkt_{po}$ | Wakati uliopo |
| $Wkt_{pita}$ | Wakati uliopita |

| | |
|---|---|
| $Wkt_{jao}$ | Wakati ujao |
| Rjsh | Urejeshi |
| I | Irabu |
| K | Konsonanti |
| Ø | kudondoshwa kwa mofu |
| MF | mfano |
| Ymbw | Yambwa |
| Shrt | Sharti |
| Rjz | Ujirejezi |
| $T^{Knsh}$ | Kitenzi kanushi |
| $T^{Yknsh}$ | Kitenzi yakinishi |
| Tdea | Utendea |
| Tdw | Utendwa |
| Tdk | Utendeka |
| Tdsh | Utendesha |
| Fnysn | Ufanyikaji sana |
| Tdna | Kutendana |
| Bdf | Ubadilifu |
| Na. | Namba |
| # | Kutangulia kwa mofu |
| !* | Nguvu zaidi |
| ** | Nguvu |
| * | Hafifu |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.1 Utangulizi

Sura hii inahusu utangulizi wa jumla ambao umeanza kwa kuelezea asili ya Wasambaa na lugha yao. Pia, inaelezea vipengele muhimu vya utafiti kama vile, usuli wa tatizo la utafiti na tatizo la utafiti. Vipengele vingine ni malengo ya utafiti ambapo lengo kuu na malengo mahususi ya utafiti yamebainishwa, maswali ya utafiti yanayotokana na malengo hayo na umuhimu wa utafiti huu. Mwisho, katika sura hii imebainishwa mipaka ya utafiti na muhtasari wa sura.

## 1.2 Asili ya Wasambaa na lugha yao

Kisambaa kinajulikana pia kama Kishambala au Kishambaa, Ki- ikiwakilisha lugha na wazungumzaji wake wakiitwa Washambaa au Washambala. Neno Shambaa linatokana na neno Shambalai lenye maana ya 'ardhi ya Wasambaa'. Shambalai ni nchi yenye milima hivyo, Wasambaa kwa asili yao wanaishi milimani huku wakifanya shughuli za kilimo na ufugaji katika maeneo hayo (Feierman, 1974). Wasambaa hawa wanapatikana nyanda za juu za kaskazini mwa Tanzania katika mkoa wa Tanga (Habibu, 2016). Kutokana na mgawanyo wa lugha za Kibantu wa Guthrie (1948) na ule wa Maho (2003), Kisambaa kipo katika kundi lenye lakabu ya G20 pamoja na Kibondei na Kizigua  ambapo Kisambaa ni G23, Kibondei G24 na Kizigua G31.

Guthrie (1948) alizigawanya lugha za Kibantu kwa kuweka lugha ambazo zinakaribiana kiisimu katika kundi moja. Hivyo lugha ya Kisambaa, Kizigua na

Kibondei ziliwekwa katika kundi moja na kundi hili kupewa lakabu ya G20. Lakabu ya G20 inamaanisha kundi la 20 lenye lugha zinazokaribiana kwa sifa za kiisimu ambazo ni Kisambaa (G23), Kibondei (G24) na Kizigua (G31). Kisambaa, Kizigua na Kibondei zinasadikiwa kuwa lugha za kundi moja la Waseuta (Nurse na Phillipson, 1980; Nkondokaya, 2003). Kwa mujibu wa maelezo ya Athuman (2012) lugha hizi tatu zina uhusiano mkubwa wa kimsamiati ambapo zinaweza kuwa lahaja za lugha moja.

Lugha ya Kisambaa inazungumzwa katika Wilaya tatu ambazo ni Lushoto, Korogwe na Muheza (Tarafa ya Amani) mkoani Tanga (Besha, 1985). Hata hivyo, MLUTA (2009:120-121) unabainisha kuwa Kisambaa kina wazungumzaji katika maeneo mengi ya mkoa wa Tanga kama vile katika Wilaya za Handeni, Kilindi, Mkinga, Lushoto, Korogwe, Muheza, Pangani na Tanga. Hivyo, kwa mujibu wa takwimu za MLUTA (2009) wazungumzaji wa Kisambaa wapo takribani 535,163. Aidha, masimulizi ya Wasambaa yanaeleza kuwa Wasambaa wa asili wanajulikana kama Washee ambao waliwakaribisha Wakilindi, Wataita, Wapare na Wambugu kutoka Same na nchini Kenya.

Kwa hiyo, katika maeneo ya Wasambaa, Wasambaa wanaishi na watu wa jamii lugha nyingine. Mathalani, katika Wilaya ya Lushoto Wasambaa wanaishi na Wachasu na Wambugu. Katika Wilaya ya Korogwe, Wasambaa wanaishi na Wabondei pamoja na Wazigua (ambao pia hujulikana kama Waruvu kutokana na mto Ruvu). Vilevile, Wasambaa wanaoishi katika Tarafa ya Amani wilayani Muheza wanaishi pamoja na Wabondei.

### 1.2.1 Lahaja katika lugha ya Kisambaa

Kwa mujibu wa Besha (1993) Kisambaa kina lahaja tatu ambazo ni lahaja ya kaskazini inayozungumzwa Mlalo, lahaja ya kati inayozungumzwa Lushoto na lahaja ya kusini inayozungumzwa Korogwe. Katika utafiti huu lahaja hizi zitaitwa lahaja ya Mlalo, lahaja ya Lushoto na lahaja ya Korogwe. Tofauti kubwa ya lahaja hizi ni ya kimatamshi; lakini pia kuna tofauti ndogo ndogo za kifonolojia na kimofolojia. Aidha, Athumani (2012) anaeleza kuwa Kisambaa kinachozungumzwa katika Wilaya ya Lushoto na kile kinachozungumzwa katika Wilaya ya Korogwe vina tofauti ndogo sana za kilahaja. Tofauti hizo ni kama zinavyoonekana katika MF.1.

**MF.1**

| **Kisambaa Lushoto** | **Kisambaa Korogwe** | **Kisambaa Mlalo** | **Kiswahili** |
|---|---|---|---|
| ombeza | ombeza | lombeza | omba |
| bua | bua | bula | fika |
| hokea | hokea | hokela | pokea |
| tongea | tongea | tongela | fuata |
| uya | uya | luya | rudi |

Data hizo zinaonesha kuwa wazungumzaji wa Kisambaa cha Lushoto, Korogwe na Mlalo wana tofauti ndogondogo za kifonolojia. Katika mfano huo, inaonekana kuwa katika Kisambaa cha Mlalo fonimu /l/ huongezwa kwenye vitenzi vingi vinavyoanza na irabu au kuishia na irabu [**a**]. Aidha, Wasambaa wa Korogwe na Lushoto katika ukanushi wanatumia fonimu /h/ ambayo hutokea mwanzoni mwa kitenzi hali ya kuwa Wasambaa wa Mlalo wanatumia fonimu /k/ inayojitokeza pia mwanzo wa

kitenzi katika hali ya ukanushi. Hata hivyo, katika vitenzi vyenye nafsi ya kwanza umoja kama **siji** katika lahaja zote tatu, ukanushi hujitokeza kwa namna moja ambapo kitenzi huchukua fonimu /s/. Tazama MF.2 ufuatao.

**MF.2**

| **Kisambaa Lushoto** | **Kisambaa Korogwe** | **Kisambaa Mlalo** | **Kiswahili** |
|---|---|---|---|
| hetiita | hetiita | ketiita | hatuendi |
| huja | huja | kuja | huli |
| heaize | heaize | keaize | hatakuja |
| hewadika | hewadika | kewadika | hawapiki |
| siiza | siiza | siiza | siji |

Pamoja na hayo, Wasambaa wa Korogwe hutumia fonimu /s/ badala ya /sh/ kama ilivyo kwa Wasambaa wa Mlalo na Lushoto (Besha, 1985), kama inavyoonekana katika MF. 3.

**MF.3**

| **Kiswahili Lushoto** | **Kisambaa Mlalo** | **Kisambaa Korogwe** | **Kiswahili** |
|---|---|---|---|
| washeize | washeize | waseize | wasije |
| shindika | shindika | sindika | sukuma |
| shaghua | shaghua | saghua | chagua |
| shenga | shenga | senga | kata |

Vilevile Wasambaa wa Mlalo wanazungumza lugha hii katika utofauti unaosababishwa na kufundishwa dini na watu ambao si Wasambaa. Inaelezwa kuwa

Wamisionari wa kanisa la Kiluteri kutoka Ujerumani walijifunza Kisambaa kwa lengo la kueneza dini yao kwa Wasambaa. Kwa mujibu wa masimulizi ya historia ya Wasambaa, Wamisionari hao walifika katika tarafa ya Mlalo mwaka 1891 ambapo wa kwanza walikuwa Mchungaji Wolhrab na Mchungaji Johannsen waliofika tarehe 6.4.1891 (Mtafitiwa, Sept, 2016). Katika kueneza dini walijifunza Kisambaa ili kuweza kuwasiliana na wenyeji wa maeneo hayo.

Kisambaa walichozungumza Wamisionari hawa aghalabu kiliathiriwa na tabia lugha ya lugha mama yao hivyo kumekuwa na mgawanyo wa Kisambaa katika tarafa ya Mlalo, Kisambaa cha Misheni na Kisambaa cha asili. Wasambaa wanaoabudu katika kanisa la Kiluteri wanazungumza Kisambaa tofauti na Wasambaa Waislamu na Wakristo wa dhehebu la Kikatoliki na wengineo. Kisambaa hicho ndicho kimetumika katika maandiko mbalimbali ya dini yao kama agano la kale (Besha, 1985). Kisambaa cha asili cha Mlalo na Kisambaa cha Mlalo Misheni kinatofautishwa kwa kuwepo kwa sauti [l] katika maneno mengi kama inavyoonekana katika MF.4.

**MF.4**

| **Kisambaa Mlalo Misheni** | **Kisambaa cha Mlalo** | **Kiswahili** |
|---|---|---|
| togola | togoa | sifu |
| ikala | ikaa | kaa |
| hongelai | hongeai | asanteni |
| ghoshola | ghoshoa | tengeneza |

Pamoja na hayo, tofauti hizi za wazungumzaji wa lahaja ya Mlalo, Lushoto na Korogwe hazizuii kuelewana baina ya wazungumzaji wa lahaja hizo. Mzungumzaji wa lahaja ya Lushoto anaelewa mazungumzo ya wazungumzaji wa lahaja ya Mlalo na Korogwe. Vivyo hivyo kwa wazungumzaji wa Mlalo na Korogwe wanaelewana na wanaweza kuwaelewa wasemaji wa lahaja ya Lushoto (Besha, 1985). Hata kwa wazungumzaji wa Mlalo Misheni na wale wanaozungumza Kisambaa cha asili katika tarafa ya Mlalo, tofauti ya uzungumzaji wao haiwazuii kuelewana kwa kuwa maana za maneno haziathiriwi na tofauti hizo za kifonolojia.

### 1.2.2 Athari ya Kiswahili katika lugha ya Kisambaa

Katika ardhi ya Wasambaa Kiswahili kinazungumzwa sana hasa katika sehemu za mijini kama Korogwe na Lushoto mjini. Hata hivyo, urahisi wa mawasiliano na maendeleo ya sayansi na teknolojia yamefanya Kiswahili kiingie pia katika maeneo ya vijijini. Kwa hiyo, kutokana na mwingiliano huo Kisambaa kimeathiriwa hasa katika msamiati wake. Besha (1985) anafafanua kuwa katika lugha ya Kisambaa kuna baadhi ya maneno ya asili ambayo hayatumiki tena. Hivyo, Kisambaa kimekopa maneno mengine kutoka Kiswahili kama katika mfano ufuatao.

**MF.5**

| **Kisambaa** | **Maneno Yaliyokopwa** | **Kiswahili** |
|---|---|---|
| minga | damda | labda |
| vikibinda | halafu | halafu |
| ndima | kazi | kazi |
| tibuka | choka | choka |
| taa | hesabu | hesabu |

Vivyo hivyo kuna baadhi ya tarakimu za Kisambaa hazitumiki na hivyo kutumika zile za Kiswahili kama inavyoonekana katika MF.6.

**MF. 6**

| **Tarakimu** | **Kisambaa** | **Kiswahili** |
|---|---|---|
| 1 | ng'wenga | moja |
| 2 | mbii | mbili |
| 3 | $nt^{h}atu$ | tatu |
| 4 | nne | nne |
| 5 | shano | tano |
| 6 | mtandatu | sita |
| 7 | mfungate | saba |
| 8 | mnane | nane |
| 9 | kenda | tisa |
| 10 | muongo | kumi |
| 100 | gana | mia |
| 1000 | kulija | elfu |

Katika mfano huo tarakimu ambazo hazitumiki kabisa kwa sasa ni mtandatu (sita), mfungate (saba), muongo (kumi), gana (mia) na kulija (elfu) kwa Kisambaa elufu. Maneno hayo yanatumika kama yalivyo katika Kiswahili.

## 1.3 Usuli wa tatizo la utafiti

Kuna aina mbalimbali za maneno katika lugha ya Kisambaa ambazo ni pamoja na kitenzi, nomino, kivumishi, kielezi, kiunganishi na kihisishi. Kwa kuwa Kisambaa ni

lugha ambishi bainishi, kitenzi katika lugha hii ni aina ya maneno yenye umbo ambalo hukiwezesha kubeba na kupokea viambishi vingi sana kuliko aina nyingine za maneno. Kama ilivyo katika lugha nyingine za Kibantu ambazo viambishi vyake vimebainishwa kama Kinyamwezi (Lodhi, 2002); Kinyakyusa (Lusekelo, 2007); Kihehe (Mpalanzi, 2010) na Shimalila (Mwashota, 2016), zimetajwa tu baadhi. Kama tulivyoeleza hapo awali kuwa, lugha nyingi za Kibantu ni lugha ambishi, hivyo viambishi vinavyounda kitenzi katika lugha hizo ni mofu zinazowakilisha mofimu mbalimbali.

Watafiti kama Kihore, Massamba na Msanjila (2003), Rubanza, (1996) na Gawasike (2011) walichunguza viambishi vya kitenzi katika Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu. Katika tafiti hizo, wameviita viambishi hivyo mofimu badala ya mofu kama umbo halisi ambalo linaonekana katika umbo la neno na mofimu ambayo ni dhana dhahania iliyopo akilini mwa mzungumzaji wa lugha inayowakilishwa na mofu. Katika muktadha huo, utafiti huu umejikita katika mofu na mofimu kwa utofauti wake kama ilivyofafanuliwa na Nida (1952), Lightner (1975), Katamba (1993), Mgullu (1999) na Massamba (2004) kwa kutaja wachache.

Mathalani, Katamba (1993) anaeleza kuwa, mofu ni kipashio kinachoweza kudhihirika katika umbo la neno ambacho kinawakilisha mofimu katika lugha. Hivyo, mofu ni umbo la neno ambalo linadhihirika kimofolojia (Nida, 1952). Mfano, katika neno **wamesoma**, maumbo yanayounda neno hilo, yaani **wa-me-som-a** ndio huelezwa kama mofu ambazo zinawakilisha mofimu mbalimbali. Mofimu moja huweza kuwakilishwa na mofu kadhaa ambazo hujulikana kama alomofu. Kwa hiyo,

utafiti huu umejikita katika kuchunguza viambishi vya maumbo ya vitenzi katika lugha ya Kisambaa ambavyo ni mofu.

Alomofu kwa mujibu wa Wesana-Chomi (2013) ni maumbo tofauti yanayowakilisha mofimu moja. Aidha, mofimu ni dhana dhahania ambayo iko akilini mwa watu na inahusu maana inayosetiriwa na mofu (Lightner, 1975). Tazama mfano ufuatao unaofafanua dhana ya mofu, mofimu na alomofu.

**MF. 7**

alicheza ni neno lenye mofu **a**- **li**- **chez**- **a**

i. **a** ni mofu inayowakilisha kiambishi cha mofimu ya kiima nafsi ya tatu umoja
ii. **li** ni mofu inayowakilisha kiambishi cha mofimu ya njeo iliyopita
iii. **chez** ni mofu inayowakilisha mzizi wa neno
iv. **a** ni mofu inayowakilisha mofimu ya kiambishi tamati yakinishi.

Hata hivyo, neno alicheza linaweza kuwa anacheza, acheza, atacheza na amecheza. Maneno hayo, yana mofu: {**a – li – chez – a**}, {**a – na – chez – a**}, {**a- chez- a**}, {**a – ta – chez – a**}, {**a – me – chez – a**} nakadhalika. Katika mofu hizo kuna mofu {-**na-**}, {-**li-**}, {-**Ø-**}, {-**ta-**}, {-**me-**}. Hizi ni alomofu zenye kubeba mofimu ya njeo. Alomofu hizo zinawakilisha njeo ya wakati uliopo hali ya kuendelea (na); uliopita (li); uliopo hali isiyodhihirika (Ø); ujao (ta) na njeo ya wakati uliopita hali timilifu (me).

Pamoja na hayo, Besha (1985); Peterson (2008), Riedel (2009) na Kaoneka (2009) wameandika kuhusu viambishi mbalimbali vinavyounda kitenzi cha Kisambaa ambavyo ni viambishi ambishi (mofu) na viambishi nyambulishi (mofu). Utafiti wa

Besha (ameshatajwa) umeweza kubainisha viambishi vinavyounda kitenzi vinavyowakilisha dhana mbalimbali ikiwemo ya njeo na hali. Aidha, Besha (1993) amebainisha pia kitenzi cha lugha ya Kisambaa na minyambuliko yake ambapo ameonesha jinsi kitenzi hicho kinavyonyumbulishwa na kuunda vitenzi vingine katika lugha ya Kisambaa.

Vilevile, Peterson (2008) ameandika kuhusu baadhi ya vipengele vya uambatizi katika Kishambala (Kisambaa), ambapo amefafanua vipashio vinavyoweza kuambikwa kabla ya mzizi wa kitenzi cha lugha ya Kisambaa. Naye Riedel (2009) amefanya utafiti linganishi wa sintaksia ya viambishi yambwa vya Kisambaa na Kihaya. Katika utafiti huo Riedel (ameshatajwa) amebainisha kuwa umbo la kitenzi katika Kisambaa linaundwa pia na viambishi yambwa. Katika ufafanuzi wake, ametumia mkabala wa Kimapokea kuonesha kuwepo kwa viambishi katika kitenzi ambavyo vinawakilisha yambwa, navyo hujitokeza kwa kufuata upatanisho wa kisarufi katika lugha ya Kisambaa. Pamoja na hao, Kaoneka (2009) amebainisha viambishi nyambulishi na ujitokezaji wake katika umbo la kitenzi cha Kisambaa. Vilevile Kaoneka (ameshatajwa) amebainisha namna viambishi nyambulishi katika kitenzi vinavyoweza kujitokeza kisintaksia katika Kisambaa.

Hivyo, kutokana na tafiti zilizotangulia ni dhahiri kuwa katika lugha ya Kisambaa kuna mofu ambishi na mofu nyambulishi zinazounda kitenzi ambazo zimebainishwa na watafiti waliotajwa. Mofu ambishi ni mofu ambazo zinaambikwa kabla ya mzizi wa kitenzi na mofu nyambulishi ni mofu zinazoambikwa baada ya mzizi wa kitenzi (Lieber, 2009; Gawasike, 2012). Pamoja na hayo, Gawasike (2012) anaeleza kuwa

mchakato unaohusika na uwekaji wa viambishi (mofu) kabla na baada ya mzizi hujulikana kama uambikaji. Hivyo, katika utafiti huu mofu zinazoambikwa kabla ya mzizi ni mofu ambishi na mofu zinazoambikwa baada ya mzizi ili kuunda vitenzi mbalimbali vya Kisambaa ni mofu nyambulishi.

Hata hivyo, katika mchakato wa uambikaji wa mofu ambishi na mofu nyambulishi katika kitenzi, mofu huweza kuathiriana pale zinapokaribiana ama zinapokaa pamoja katika umbo la kitenzi. Kuathiriana kwa mofu katika kitenzi kunaweza kutokea kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na hata kisemantikia. Katika tafiti zilizotangulia kuathiriana huko kwa mofu ambishi na mofu nyambulishi hakujabainishwa. Mathalani, katika utafiti wa Besha (1985) na Besha (1993), Peterson (2008) na Kaoneka (2009) wanabainisha namna mofu ambishi na mofu nyambulishi zinavyojitokeza katika vitenzi vya Kisambaa pamoja na maumbo mbalimbali ya mofu hizo bila kuhusisha kuathiriana kwa mofu zinapokaa pamoja kuunda kitenzi cha Kisambaa.

Kwa hiyo utafiti huu umehusika na namna mofu zinavyoathiriana zinapokaa pamoja kuunda kitenzi cha Kisambaa. Katika utafiti huu kuathiriana huko kwa mofu kunahusisishwa na mabadiliko yanayotokea katika mofu kimofolojia au kimofofonolojia pale mofu fulani inapoambishwa au kunyambulishwa katika kitenzi cha Kisambaa.

Pamoja na hayo, kuathiriana kwa mofu zinazounda vitenzi katika lugha za Kibantu kumebainishwa na watafiti kama Rugemarila (1993) katika vitenzi vya Kirunyambo ambapo amebainisha namna mofu zinapoambishwa zinavyoathiri mofu nyingine

kwa kubadilisha maumbo ya mofu hizo. Naye Charwi (2011) amefafanua athari za kuambikwa kwa mofu kisintaksi ambapo kitenzi cha Kikuriya kinaweza kuwa elekezi au si elekezi. Pamoja na hao Mwashota (2011) amebainisha kuathiriana kwa mofu katika umbo la kitenzi cha Shimalila ambapo amefafanua athari ya mofu za njeo kifonolojia inavyoathiri mofu ya mofimu ya nafsi, mzizi na kiambishi tamati.

Hivyo, utafiti huu umeshughulika na kuathiriana kwa mofu zinapokaa pamoja katika kitenzi kimofolojia au kimofofonolojia kutokana na mchakato wa uambikwaji wa mofu hizo. Kuathiriana huko, kumebainishwa na kufafanuliwa kwa kuzingatia mashartizuizi yanayotawala utokeaji wa mofu zinapoambikwa katika mzizi wa kitenzi cha lugha ya Kisambaa. Hivyo, utafiti huu umefafanua mofu zinazounda kitenzi cha Kisambaa pamoja na kubainisha namna mofu hizo zinavyoathiriana kwa kubainisha mashartizuizi ya lugha hii wakati wa uambishaji na unyambulishaji wa mofu katika kitenzi.

## 1.4 Tatizo la utafiti

Kuna uwezekano mkubwa wa mofu zinazounda kitenzi cha lugha ya Kisambaa kuathiriana wakati wa uambikwaji mofu hizo; yaani wakati wa kupachika viambishi mbalimbali (kuambishwa na kunyambulishwa) katika mzizi wa kitenzi. Mofu zinaweza kuathiriana kutokana na michakato ya kifonolojia na kimofolojia pale zinapokaa pamoja katika umbo la kitenzi. Katika kitenzi cha lugha ya Runyambo kwa mfano, mofu ya njeo ya wakati uliopita **-ír-** na njeo ya wakati timilifu **-a-**,**-ir-** huhitaji mofu yakinishi **-e** na si **-a** (Rugemalira, 1993). Vilevile katika lugha ya Shimalila, Mwashota (2016) anabainisha kuwa uambishaji wa mofu ya mofimu ya

njeo ya wakati uliopita na ujao katika mzizi wa kitenzi husababisha mabadiliko ya kifonolojia katika mzizi, kiambishi tamati na toni katika mofu ya nafsi inayoambikwa pamoja na mofu njeo. Mifano hiyo inadhihirisha kuwa, kama ilivyo katika lugha nyingine za Kibantu, mofu katika kitenzi cha Kisambaa zinaweza kuathiriana. Miathiriano hiyo ya maumbo ya mofu inaweza kusababisha maumbo ya awali ya kitenzi cha Kisambaa kubadilika na kuunda aina nyingine ya neno (la Kisambaa) au kitenzi chenye maana nyingine tofauti na ya kitenzi cha awali.

Kuathiriana kwa mofu zinapokaa pamoja wakati wa kuunda kitenzi cha Kisambaa na mabadiliko ya umbo la kitenzi yanayotokea kama ambavyo imeonekana katika lugha nyingine za Kibantu kama Runyambo na Shimalila havijawahi kufanyiwa utafiti. Hivyo, utafiti huu umejikita katika kuyachunguza maumbo ya vitenzi vya Kisambaa na kufafanua namna yanvyoathiriana kimofolojia au kimofofonolojia wakati wa umbikaji wa mofu ambishi na nyambulishi zinazounda vitenzi hivyo. Vilevile, tumebainisha mashartizuizi ya lugha hii yanayoongoza uambikwaji wa mofu katika vitenzi. Hivyo, utafiti huu umekusudia kuchunguza ikiwa mofu hizo zinapoathiriana zinaweza kusababisha kitenzi cha Kisambaa kubadilika maana au kuunda aina nyingine ya neno la Kisambaa badala ya kitenzi cha awali.

## 1.5 Malengo ya utafiti

Utafiti huu una lengo kuu na malengo mahususi, kama ifuatavyo:

### 1.5.1 Lengo kuu

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza na kuchanganua namna mofu zinavyoathiriana kimofolojia au kimofofonolojia zinapokaa pamoja kuunda kitenzi cha lugha ya Kisambaa kwa kuzingatia mashartizuizi ya lugha hii.

### 1.5.2 Malengo mahususi

a) Kubainisha mofu ambishi na nyambulishi pamoja na mofimu zake zinazounda kitenzi cha lugha ya Kisambaa.

b) Kuchanganua namna mofu zinavyoathiriana kimofolojia au kimofofonolojia zinapokaa pamoja wakati wa kuunda kitenzi katika lugha ya Kisambaa.

c) Kudhihirisha mashartizuizi yanayotawala uambikaji wa mofu katika kitenzi cha Kisambaa.

## 1.6 Maswali ya utafiti

i) Ni maumbo gani ya mofu ambishi na nyambulishi pamoja na mofimu zake yanayounda kitenzi cha lugha ya Kisambaa?

ii) Mofu zinaathirianaje zinapokaa pamoja wakati wa kuunda kitenzi katika lugha ya Kisambaa?

iii) Je yapo mashartizuizi yanayotawala uambikaji wa mofu katika kitenzi cha Kisambaa?

## 1.7 Umuhimu wa utafiti

Kitenzi ni neno muhimu katika muundo wa sentensi na hivyo hatuna budi kujua umbo la kitenzi lilivyo katika lugha mbalimbali za Kibantu. Kitenzi cha Kisambaa kina umbo linalopokea mofu mbalimbali zinazoambishwa na kunyambulishwa katika mzizi wa kitenzi. Hivyo, utafiti huu wa kuchunguza namna maumbo ya mofu yanavyoathiriana wakati wa kuunda vitenzi ni muhimu ili kuongeza maarifa katika sarufi ya lugha ya Kisambaa kwa upande wa mofolojia ya vitenzi. Utafiti huu pia utabainisha upekee wa lugha ya Kisambaa kwa namna maumbo ya vitenzi

yanavyojengwa na mofu mbalimbali zinazoambishwa na kunyambulishwa katika mzizi wa kitenzi.

Pia, utafiti huu ni mwendelezo wa kutafiti lugha za Kibantu kwani utasaidia kubaini mofu, mofimu na alomofu katika kitenzi cha Kisambaa. Utafiti huu utasaidia kutambua uhusiano wa mofu zinazounda vitenzi kwa kuwa mofu hizo zimechunguzwa na kubainishwa namna zinavyoathiriana kimofolojia au kimofofonolojia na matokeo ya kuathiriana kwa mofu hizo katika umbo la kitenzi cha lugha ya Kisambaa. Vilevile utafiti huu utabainisha mashartizuizi yanayotawala uambikaji wa mofu ambishi na mofu nyambulishi katika vitenzi vya Kisambaa. Pamoja na hayo utafiti huu utakuwa rejeo kwa wanataaluma na watafiti wengine wanaoendelea kutafiti lugha za Kibantu na ni chachu kwa tafiti nyingine za kiisimu.

Aidha, utafiti huu utaendeleza uchambuzi wa masuala ya kimofolojia kwa kutumia nadharia ya Umbo Upeo. Kwa mujibu wa maelezo ya Massamba (2011), nadharia ya Umbo Upeo iliibuka kutokana na matatizo yaliyojibainisha katika Kiunzi Rasmi cha Fonolojia Zalishi kuhusu udhahania wa uwakilishi wa vipengele vya kifonolojia. Hivyo, madhumuni ya kuanzishwa kwa nadharia hii yalikuwa ni kushughulikia masuala ya kifonolojia, lakini baadae ikatumika pia katika uchambuzi wa masuala ya kisintaksia na kimofolojia. Kwa hivyo, utafiti huu utakuwa msingi wa namna sarufi ya lugha za Kibantu hasa katika kipengele uundaji wa kitenzi inavyoweza kuchunguzwa na kuchambuliwa kwa kutumia nadharia ya Umbo Upeo.

## 1.8 Mipaka ya utafiti

Kwa kawaida mofolojia ya kitenzi ni pana, hata hivyo, utafiti huu umejikita katika kuchunguza umbo la kitenzi cha lugha ya Kisambaa. Umbo hilo limechambuliwa baada ya kuchunguza viambishi vinavyounda kitenzi cha Kisambaa. Mtafiti alitarajia kuchunguza na kuchambua mofu zinazojenga kitenzi cha lugha ya Kisambaa na maana zinazowakilishwa na mofu hizo yaani mofimu zinazowakilishwa na mofu hizo.

Pamoja na hayo, utafiti huu umeshughulika na mahusiano ya mofu kwa kujikita katika kuathiriana kwa maumbo ya mofu wakati wa kuunda kitenzi cha Kisambaa. Mofu zinazokaribiana na kuathiriana kimofolojia au kimofofonolojia zimebainishwa pamoja na maumbo ya vitenzi yanayotokea baada ya muathiriano huo wa maumbo ya mofu. Mofu hizo zinazounda kitenzi cha Kisambaa kwa kuambishwa na kunyambulishwa katika mzizi wa kitenzi zimechunguzwa kwa kuongozwa na nadharia ya Umbo Upeo ambapo mashartizuizi yanayotawala mfuatano wa mofu katika maumbo ya vitenzi vinavyokubalika katika lugha hii yamezingatiwa na kudhihirishwa.

Lugha ya Kisambaa inazungumzwa katika maeneo mengi ya Mkoa wa Tanga, hata hivyo utafiti huu umejikita katika Kisambaa kinachozungumzwa katika Wilaya ya Lushoto. Vilevile katika Wilaya ya Lushoto kuna maeneo mengi ambako Kisambaa kinazungumzwa lakini data za utafiti huu zimekusanywa katika Tarafa ya Mlalo katika Kata tatu na si kata zote za Tarafa hiyo.

## 1.9 Changamoto katika utafiti huu

Katika utafiti huu, mbali na mafanikio aliyopata mtafiti kwa kukusanya data inayofaa pia alipata changamoto kadhaa. Kama ilivyoelezwa hapo awali eneo la utafiti ni Tarafa ya Mlalo iliyopo Wilaya ya Lushoto. Katika tarafa hiyo kuna kata mbalimbali lakini mtafiti aliteua kata tatu. Changamoto aliyoipata ni usafiri wa kufika katika kata hizo. Hivyo basi, ilimlazimu mtafiti atumie usafiri wa pikipiki ambao haukuwa salama. Vilevile mbali na kusafiri umbali mrefu changamoto nyingine ilikuwa kutowapata viongozi wa kata zilizohusika kwa wakati na wengine kuwakosa kabisa. Hali hii ilimsumbua mtafiti lakini ilimlazimu kuwatumia viongozi wengine wa vijiji badala ya watendaji wa kata inayohusika. Aidha kuna watoa taarifa wengine hawakuwa tayari kuhojiwa na hivyo kusababisha usumbufu mkubwa wa muda katika kujaribu kutafuta watoa taarifa wengine. Hata hivyo, mtafiti alijitahidi kuzikabili changamoto hizo ili kuweza kufanikisha malengo yaliyokusudiwa katika utafiti huu.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inahusu mapitio ya kazi mbalimbali za kinadharia na kazi zilizofanyiwa utafiti kuhusu mada inayotafitiwa katika utafiti huu. Mapitio ya kazi hizo yamefanywa kwa kuzingatia lengo kuu na malengo mahususi yanayoongoza utafiti huu. Lengo la kupitia kazi tangulizi ni kuonesha yaliyofanyika katika mada ya utafiti na pengo lililopo ambalo lilimsukuma mtafiti kufanya utafiti huu. Sehemu ya kwanza inaeleza dhana za mofu, mofimu na alomofu.

Sehemu ya pili inafafanua tafiti mbalimbali kuhusu mofu ambishi na mofu nyambulishi katika lugha za Kibantu. Sehemu ya tatu inahusu tafiti zilizokwishafanywa kuhusu kuathiriana kwa mofu katika lugha za Kibantu ambapo sehemu ya nne inahusu tafiti mbalimbali katika Kisambaa ambazo zimefafanua dhana muhimu zitakazotumika katika uchambuzi na uchunguzi wa viambishi vya kitenzi katika Kisambaa. Sehemu ya tano inabainisha kuhusu kiunzi cha nadharia kilichoongoza utafiti huu na mwisho ni muhtasari wa sura.

## 2.2 Mofu na mofimu katika umbo la kitenzi

Mofu ni dhana muhimu katika kufafanua maumbo ya maneno katika lugha kwa kuwa ndio kijenzi cha umbo neno. Dhana ya mofu na mofimu zimekuwa zikifafanuliwa kwa kuchanganywachanganywa kiasi ambacho huonekana kuwa na utata. Istilahi hizi zimetoholewa kutoka katika lugha ya Kiingereza, yaani mofu "morph" na mofimu "morpheme" (Mgullu, 1999). Kwa mujibu wa maelezo ya Mgullu (ameshatajwa) wakati wa Sarufi Mapokeo uchambuzi wa tungo uliishia

katika kiwango cha neno. Baadaye katika karne ya 18 na 19 ilionekana haja ya kubainisha vipashio vya chini zaidi ya neno, ndipo ilipoanza kutumika istilahi ya mofimu. Hivyo istilahi ya mofimu ndio ilianza kutumika katika uchanganuzi wa vijenzi vya neno (Katamba, 1993).

Mofu ilianza kutumika katika karne ya 20 hasa baada ya kuasisiwa kwa Sarufi Zalishi. Hivyo, dhana ya mofimu imekuwa ikielezwa kuwa ni kipashio kidogo cha neno chenye maana. Wataalamu kama TUKI (1990), Spencer (2003), Massamba na Msanjila (2003), Booji (2007), Lieber (2009) na Haspelmath na Sims (2010) wanamtazamo kuwa, mofimu ndio kipashio kidogo cha neno chenye maana na ambacho hakiwezi kugawanyika zaidi. Mathalani, Lieber (2009) anafafanua kuwa mofimu ni kipashio kidogo katika lugha ambacho kina maana. Kutokana na maelezo hayo mofimu inaweza kuelezwa kuwa ni umbo la neno linalodhihirika kimofolojia na lenye maana. Kwa mtazamo huu, mofimu zinazounda neno la lugha ya Kiswahili **anayefika** ni pamoja na {**a-na-ye-fik-a**}.

Hata hivyo, wapo wanaisimu kama Platt (1985), Katamba (1993), Lockwood (1993), Carstair-McCarthy (2002), Massamba (2004) na Štekauer na Lieber (2005) ambao wanaieleza mofimu kama maana inayowakilishwa na mofu wakati mofu ndio kipashio kidogo cha neno. Mathalani, Katamba (1993) anafafanua kuwa mofu ni kipashio kinachoweza kudhihirika katika umbo la neno ambacho kinawakilisha mofimu katika lugha. Katamba (ameshatajwa) anaendelea kueleza kuwa mofimu haziundwi na sauti bali zinawakilishwa na mofu ambazo ndizo zinaundwa na sauti. Kwa mtazamo huu wa mofu kuwa umbo linalodhihirika katika neno ambalo linawakilisha mofimu, neno **anayefika** linaundwa na mofu {**a-na-ye-fik-a**}. Mofu

{**a**-} inawakilisha mofimu ya nafsi ya tatu umoja, mofu {-**na**-} inawakilisha mofimu ya wakati uliopo, mofu {-**ye-**} ni mofimu ya urejeshi wa mtenda na mofu {-**fik**-} ni mzizi wa kitenzi ambapo mofu {-**a**} ni mofu ishilizi inayokamilisha maana ya kitenzi katika lugha ya Kiswahili.

Kwa hiyo, kutokana na fasili hizo za mofu na mofimu, utafiti huu umetumia dhana ya mofu kama kipashio kidogo cha neno ambacho hakiwezi kugawanyika zaidi bila kupoteza maana na mofimu kama maana inayowakilishwa na mofu. Vilevile, mofu inadhihirika pale inapoandikwa ama inapotamkwa. Mofimu haiwezi kudhihirika kiumbo ila ni maana ya mofu iliyomo akilini mwa mzungumzaji wa lugha. Mofu iko katika utendaji na mofimu ni kipashio dhahania na ni tafsiri ambayo mzungumzaji wa lugha huwa nayo akilini. Tafsiri hiyo, mzungumzaji anaipata katika mofu inayounda neno katika lugha (Lightner, 1975; Katamba, 1993).

Aidha, mofu katika umbo la neno inahusisha viambishi pamoja na mzizi na shina la neno. Kwa maana ya kwamba, mofu zinaambishwa na kunyambulishwa katika mzizi au shina la kitenzi ili kupata vitenzi vyenye maumbo mbalimbali katika lugha. Kwa mujibu wa maelezo ya Gambarage (2011) mzizi katika umbo la neno unabainishwa kama kiini au umbomsingi la neno linalohusika. Vilevile, Carstair-McCarthy (2002), Kihore (2011) na Haspelmath na Sims (2010) wanaufafanua mzizi kuwa ni sehemu ya neno ambayo haiwezi kugawanyika zaidi. Katika fasili hizo, mzizi umebainishwa kisemantiki kama kiini cha neno ambapo hata maana ya neno inajengwa kutoka katika mzizi. Pia, mzizi umebainishwa kimofolojia kama sehemu ya neno ambayo haiwezi kugawanyika zaidi. Hivyo basi, mzizi ni mofu ambayo haiwezi kugawanyika zaidi bila kupoteza maana yake ya kisarufi na ndicho kiini cha neno.

Pia, mzizi ni mofu ambayo inapokea viambishi mbalimbali ili kuunda vitenzi. Kama katika neno la mfano la lugha ya Kiswahili **anayefika**, mzizi wa neno hili **–fik**- ndio umepokea viambishi (mofu) {**a-**}, {**-na-**}, {**-ye-**} na {**-a**}.

Shina la neno, linaelezwa kuwa ni sehemu ya neno yenye mzizi na viambishi (Kihore na wenzake, 2003; Gambarage, 2011; Kihore, 2011). Katika muktadha huo, Gambarage (ameshatajwa) anaendelea kufafanua dhana ya shina kuwa, ni viambishi vinavyounda shina ambavyo vinaweza kuwa kiambishi kimoja au zaidi. Matahalani, katika Kiswahili maneno yafuatayo yanabainisha mizizi na mashina yake:

**MF. 8**

| **Neno** | **Mzizi** | **Shina** |
|---|---|---|
| pata | pat- | pata |
| kata | kat- | kata |

Katika mfano hapo juu tumebaini mizizi na mashina ya maneno ya Kiswahili. Hivyo, mofu katika lugha ya Kisambaa zinaambikwa katika mzizi au shina ambazo ni sehemu za maneno zinazoweza kupokea mofu mbalimbali katika lugha.

Hivyo, mofu katika lugha ya Kisambaa zinaambikwa katika mzizi au shina ambazo ni sehemu za maneno zinazoweza kupokea mofu mbalimbali katika lugha.

Katika kubainisha namna mzizi unavyopokea viambishi, Wesana- Chomi (2013) anabainisha namna maneno ya Kiswahili **imba**, **imbiwa, imbia** na **imbiana** yanavyoundwa na mofu (akiziita mofimu) zikiambikwa katika mzizi **imb**- kama inavyoonekana hapa chini.

**Jedwali 2.1: Mofu katika Umbo Neno**

| Neno | Mofu |
|---|---|
| imba | imb-a |
| imbiwa | imb-i-w-a |
| imbia | imb-i-a |
| imbiana | imb-i-an-a |

**Chanzo:** Wesana-Chomi (2013)

Hivyo basi, katika jedwali namba 2.1 mofu zinazounda vitenzi vya lugha ya Kiswahili **imba**, **imbiwa**, **imbia** na **imbiana** zimeambikwa katika mzizi **–imb-**.

Sambamba na hayo, Hartman (1972) anaendelea kufafanua kuwa kuna mofu tofauti tofauti katika mazingira fulani zinazowakilisha mofimu. Mofu hizo zinazowakilisha mofimu moja huitwa alomofu (Richards, Platt na Weber, 1985; Katamba,1993; Rubanza, 1996; Carstair-McCarthy, 2002; Haspelmath na Sims, 2010). Kwa mujibu wa maelezo ya Katamba (1993) alomofu ni mofu zenye maumbo kadhaa tofauti tofauti yanayoisitiri mofimu moja. Pamoja na wataalamu hao Wesana-Chomi (2013) anatubainishia vitenzi vya Kiswahili ambapo katika maumbo ya vitenzi hivyo kuna alomofu zinazowakilisha mofimu ya kutendwa. Tuangalie mifano katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 2.2: Alomofu za Mofimu ya Kutendwa katika Kiswahili**

| Kitenzi | Mzizi | Alomofu |
|---|---|---|
| somwa | som- | -w- |
| pigwa | pig- | -w- |
| katwa | kat- | -w- |
| ondolewa | ondo- | -lew- |
| tolewa | to- | -lew- |
| chaguliwa | chagu- | -liw- |
| fuliwa | fu- | -liw- |
| tibiwa | tib- | -iw- |
| jibiwa | jib- | -iw- |

**Chanzo:** Wesana-Chomi (2013)

Katika jedwali jedwali hapo juu tunabaini mofu zinazowakilisha mofimu ya kutendwa zina maumbo {-w-}, {-lew-}, {-liw-} na {-iw-}. Kila alomofu hutokea katika mazingira yake kwa hiyo kuna kanuni za lugha inayohusika zinazotawala utokeaji wa alomofu (Wesana- Chomi, 2013). Kanuni inayoeleza utokeaji wa alomofu hizo ni hii:

{M-} ⟶ ( m-/mzK
w-/mzI )

Kanuni hiyo inaeleza kuwa, mofu {M} huchukua alomofu /-m-/ katika mazingira ya mzizi wa neno unaoanza na konsonanti. Pia huchukua alomofu /-w-/ katika mazingira ya mzizi wa neno unaonza na irabu.

Kwa hiyo katika utafiti huu, uchambuzi na uchunguzi wa namna maumbo ya mofu zinazounda kitenzi katika lugha ya Kisambaa zinavyoathiriana umehusisha pia kupambanua mofu, mofimu na alomofu zinazowakilisha mofimu moja kwenye kitenzi cha lugha hii. Pamoja na hayo, Omar (2008) anaeleza kuwa lugha za Kibantu na lugha nyingine za kundi la Kikongo – Kibenue, pamoja na makundi yanayoambatana nayo, huunda vitenzi kwa kuongeza mofimu (kama alivyoziita) awali na tamati katika mzizi. Kwa mujibu wa maelezo ya Gawasike (2012) kitendo cha kuweka mofu au viambishi katika mzizi wa neno ili kuunda maneno hujulikana kama uambikaji.

Dhana ya uambikaji imeelezwa pia kama unyambulishaji na wanaisimu kama

Rubanza (1996), Kihore na wenzake (2003) na Massamba (2004). Dhana hii ya unyambulishaji vilevile katika lugha ya Kiswahili imekuwa na utata kwani kuna wanaoamini kuwa unyambulishaji ni uwekaji wa viambishi baada ya mzizi wa neno pekee kama Mohammed (2001) na Matei (2008). Wapo wengine wanaoona kuwa unyambulishaji unahusu uongezaji wa mofu kabla na baada ya mzizi wa neno kama Katamba (1993), Rubanza (1988, 1996) na Khamis (2009).

Hata hivyo, katika utafiti huu tumetumia dhana ya uambikaji kama mchakato wa kimofolojia unaohusika na kuongezwa kwa mofu katika mzizi wa neno. Gawasike (2012) anafafanua kuwa uambikaji ni dhana pana inayohusisha uambishaji na unyambulishaji. Uambishaji ukihusu uwekaji wa viambishi kabla ya mzizi wa neno kama anavyoeleza Lieber (2009) kuwa uambishaji ni mchakato wa kuunda maneno ambao hauhusishi mabadiliko ya kategoria ya neno bali viambishi vinavyoambishwa vinatoa taarifa za kisarufi katika neno. na unyambulishaji ni uongezaji wa viambishi baada ya mzizi wa neno. Hivyo katika utafiti huu, uambishaji unazihusu mofu ambishi, yaani mofu zinazoambikwa kabla ya mzizi wa neno na unyambulishaji unazihusu mofu nyambulishi ambazo zinaambikwa baada ya mzizi wa kitenzi. Katika mazingira hayo, uambikaji ni njia mojawapo ya uundaji wa maneno katika lugha ambishi. Kwa vile utafiti huu unashughulika na uundaji wa vitenzi katika lugha ya Kisambaa, mofu zimechunguzwa katika kuambishwa na kunyambulishwa katika mzizi wa kitenzi. Tazama Jedwali namba 2.3 na 2.4.

**Jedwali 2.3: Uambishaji wa Mofu katika Mzizi wa Kitenzi**

| **Neno** | **Ubainisho wa mofu** |
|---|---|
| hawatatuona | ha-wa-ta-tu-**on**-a |

| | |
|---|---|
| tutawatazama | tu-ta-wa-**tazam**-a |
| wametupiga | wa-me-tu-**pig**-a |

**Chanzo:** Gawasike (2012)

**Jedwali 2.4: Unyambulishaji wa Mofu katika Mzizi wa Kitenzi**

| **Neno** | **Ubainisho wa mofu** |
|---|---|
| bebeshana | **beb**-esh-an-a |
| pokezana | **poke**-z-an-a |
| fagiliwa | **fagi**-li-w-a |
| somesheana | **som**-esh-an-a |

**Chanzo:** Gawasike (2012)

Katika majedwali Na. 2.3 na Na. 2.4 hapo juu, tunabaini kuwa sehemu ya neno iliyoandikwa kwa wino mzito mweusi ni mzizi ambao unapokea mofu (viambishi) kabla yaani kuambishwa kwa mofu na baada ambayo ni kunyambulishwa kwa mofu. Massamba (2004) anaeleza kuwa uambishaji ni uongezaji wa mofu (akiziita mofimu) kabla ya mzizi wa neno. Naye Gawasike (2012) anaeleza kuwa unyambulishaji ni mchakato wa upachikaji wa mofu baada ya mzizi wa neno. Aidha, wanaisimu wengine kama Mutaka na Tamanji (2000) na Ngonyani (2003) wanaeleza kuwa unyambulishaji unauhusu uongezaji wa viambishi (mofu) baada ya mzizi wa neno ili kuunda vitenzi vipya. Hivyo unyambulishaji unahusika na uundaji wa vitenzi vipya katika lugha. Kwa hiyo, mofu ambishi na mofu nyambulishi zinazounda kitenzi cha lugha ya Kisambaa zimechunguzwa na kuchambuliwa katika umbo la kitenzi kwa namna ambayo zimeambikwa ili kubaini namna zinavyoathiriana kimofolojia au kimofofonolojia katika maumbo yake na kuathiri umbo la kitenzi kwa ujumla.

### 2.3 Mapitio ya tafiti mbalimbali katika lugha za Kibantu

Katika sehemu hii tunabainisha na kufafanua mofu ambishi na nyambulishi katika lugha ya Kisambaa na pia, tunajadili mofu hizo katika lugha nyingine za Kibantu.

### 2.3.1 Mofu ambishi na mofu nyambulishi katika lugha ya Kisambaa

Kitenzi cha Kisambaa kama vilivyo vitenzi vingi vya lugha za Kibantu kama Kihehe, Kinyambo na Kichuka vinaikubali kanuni ya kuwa na viambishi (mofu) kabla ya mzizi ambavyo ni viambishi awali na vambishi baada ya mzizi ambavyo ni viambishi tamati. Katika Kichuka kwa mfano, kitenzi cha lugha hii nacho kinaafiki kanuni hiyo kama wanavyoeleza Salesio, Mukuthuria na Matundura (2016). Kanuni hiyo inaweza kufafanuliwa kama:

Kitenzi: Viambishi Awali (VA) + Mzizi (Mz) + Viambishi Tamati (VT)

Katika muktadha wa mofu ambishi na mofu nyambulishi zinazoambikwa katika kitenzi, katika nafasi ya viambishi awali zinajitokeza mofu ambishi ambazo zinatokea kabla ya mzizi. Pia, katika nafasi ya viambishi tamati zinajitokeza mofu nyambulishi ambazo zinaambikwa baada ya mzizi wa kitenzi. Kutokana na sifa hiyo ya vitenzi vya lugha za Kibantu kikiwemo Kisambaa imewafanya watafiti mbalimbali kuchunguza namna mofu hizo zinavyojitokeza katika umbo la kitenzi katika lugha mbalimbali za Kibantu.

Katika ya lugha ya Kisambaa watafiti kama Besha (1985, 1993), Peterson (2008), Riedel (2009) na Kaoneka (2009) wamebainisha kuwa kitenzi kinaundwa na mofu

ambishi na nyambulishi. Besha (1985) ametafiti kuhusu njeo na hali katika lugha ya Kisambaa. Katika utafiti wake, anaeleza kuwa katika lugha ya Kisambaa kuna mofu ya njeo ya wakati uliopo yenye maumbo {**-Ø-**} (wakati uliopo tegemezi); {**-ta-**} (wakati uliopo) na {**-aa-**} wakati uliopo hali ya kuendelea, vilevile njeo ya wakati uliopita ina maumbo {**-te-**} (wakati uliopita muda mchache); {**-iye-**} (jana); {**-za-**} (jana); {**-a-**} (siku ile) na {**-aa-**} (siku ile) pamoja na njeo ya wakati ujao yenye maumbo {**ne-**} ( ujao karibuni) na {**nee-**} (muda mrefu ujao). Mofu hizi za njeo zimefafanuliwa kwa kutumia kitenzi cha Kisambaa ambamo zinaambishwa ili kuunda vitenzi katika lugha hii. Kama katika mfano ufuatao (Besha, 1985: 203-204).

**MF. 9**

ti-**te**-dika ‘tulipika’

ti-**za**-dika ‘tulipika’

ta-**a**-dika ‘tulipika’

Vilevile, Peterson (2008) amefafanua baadhi ya vipengele vya uambatizi wa vitenzi katika lugha ya Kisambaa. Katika ufafanuzi wake, Peterson (ameshatajwa) anabainisha baadhi ya mofu ambazo zinaambishwa kabla ya mzizi wa kitenzi ambapo ameongeza baadhi ya mofu ambazo hazikubainishwa katika utafiti wa Besha (1985). Mofu hizo ni pamoja na mofu ya dhamira amrishi {-e} ambayo hutokea mwishoni mwa kitenzi kama katika mfano ufutao.

**MF. 10**

**Kitenzi**

ntagh**e**

utagh**e**

mtagh**e**

senghook**e**

kemghook**e**

**Chanzo: Peterson (2008: 54)**

Katika mfano huo, mofu {-e} ambayo inaonekana mwishoni mwa vitenzi ndiyo inayowakilisha dhamira amrishi katika vitenzi vya Kisambaa katika hali yakinishi na kanushi.

Peterson (ameshatajwa), pia anabainisha mofu za njeo ambapo anafafanua mofu za njeo ya wakati uliopita {-**te**-}, {-**iye**-} na {-**za**-}. Mofu {-**te**-} ikiwakilisha wakati uliopita muda mfupi uliopita na {-**iye**-} na {-**za-**} zikidokeza wakati uliopita muda mrefu kama vile jana au juzi. Mofu ya njeo ya wakati uliopo katika ufafanuzi huu, imebainishwa kwa maumbo {-**a**-}, {-**ta**-} na {**-Ø-**} na njeo ya wakati ujao ikiwakilishwa na mofu {-**ne**-}. Aidha, katika ufafanuzi wa vipengele vya uambatizi mofu za hali pia zimebainishwa ambapo kwa mujibu wa maelezo ya Peterson (2008:57) katika Kisambaa mofu za hali hupachikwa sehemu ileile ya mofu za njeo. Mofu hizo ni {-**i**-} ambayo huwakilisha hali timilifu ya tendo, {-**ke**-} inayodokeza hali isiyotimilifu ya tendo, mofu {-**ki**-} ikionesha hali ya masharti na mofu {-**ku**-} ikiwakilisha uendelevu wa tendo au huambikwa katika vitenzi visoukomo.

Pamoja na hayo, mofu za upatanishi nazo zimebainishwa. Mofu hizi zinaonesha upatanisho wa kisarufi ambao hutegemea ngeli ya nomino inayohusika katika sentensi. Mofu hizo ni pamoja na {-**na/ta-**} katika nafsi ya kwanza, {-**mwa/wa-**} katika nafsi ya pili na {-**a/wa-**} katika nafsi ya tatu. Mofu nyingine za upatanishi ni

{-**u/i-**} na {-**ya**} katika ngeli za nomino **M/MI** na **-Ø-/MA.** Vilevile, viambishi yambwa vinadokezwa na Peterson (2008:60) ambapo anabainisha mofu {**-ni/ti-**} za nafsi ya kwanza, {**-ku/mi-**} za nafsi ya pili na {**-mu/wa-**} za nafsi ya tatu. Pia, mofu za urejeshi zinabainishwa ambazo nazo zinaukiliwa na ngeli za nomino. Mofu hizo za urejeshi ni {-**ye**}, {-**wo**}, {-**cho**}, {-**vyo**} na {-**zo**}. Kwa hiyo, katika utafiti huu mofu hizi za urejeshi zinabainishwa namna zinavyoathiriana na mofu nyingine katika umbo la kitenzi.

Pamoja na hao, Riedel (2009) amefanya uchambuzi wa kisintaksia wa mofu yambwa katika vitenzi vya Kisambaa. Katika ufafanuzi wake anaeleza kuwa, mofu ya yambwa katika kitenzi cha Kisambaa inaweza kuwa ya lazima, ya hiari au kutokuwepo kwa mofu hiyo kunaifanya sentesi isikubalike katika sarufi ya Kisambaa kulingana na aina ya nomino inayofuata kitenzi. Kwa hiyo, katika sentesi za Kisambaa kuna wakati ambapo mofu yambwa haihitaji kuambishwa kwenye kitenzi. Vilevile katika Kisambaa, mofu ya yambwa inayoambishwa katika kitenzi ili kuifanya sentensi ikubalike ina uhusiano na nomino ya kiima na nomino ya yambwa (Riedel, 2009:99-103). Pamoja na hayo, kitenzi cha Kisambaa kinaweza kuambishwa kwa mofu yambwa zaidi ya moja. Kitenzi kikiwa katika muktadha wa sentensi kinafuatiwa na nomino yambwa mbili, kama katika mfano ufuatao.

**MF. 11**

nizachimnk$^{h}$a ngwana kitabu ‘nimempa mtoto kitabu’

ni-za-chi-m- nk$^{h}$-a

Nfs-Nj-Ymb1-Ymb2-Mz-M$_{i}$

Katika mfano hapo juu, tunabaini kitenzi kimepachikwa mofu yambwa mbili ambapo yambwa ya kwanza inawakilisha nomino **kitabu** na yambwa ya pili inawakilisha nomino **mtoto**.

Kwa hiyo, Riedel (ameshatajwa) ameichambua mofu ya yambwa katika muktadha wa kisintaksia. Katika uchambuzi huo, amelinganisha uambishaji wa mofu yambwa na namna mofu hiyo inavyojitokeza kisintaksia katika Kisambaa, Kiswahili na Kihaya. Hata hivyo, bado namna mofu hiyo inavyoweza kuathiriwa au kuathiri mofu nyingine katika umbo la kitenzi hakujabainishwa.

Kwa upande wa mofu nyambulishi zinazoweza kunyambulishwa katika kitenzi cha Kisambaa, Besha (1993) amebainisha mofu ya utendea yenye maumbo {-**i**-} na {-**e**-}, mofu ya usababishi inayowakilishwa na {-**iz**-} na {-**ez**-}, ya ufanyikaji sana ambayo ina alomofu {-**ish/iz**-} na {-**esh/ez**-}, mofu ya kutendeka {-**ik**-} na {-**ek**-}, mofu ya kutendwa {-**ighw**-} na {-**w**-}, mofu ya kutendana {-**an**-} pamoja na mofu ya ubadilifu {-**u**-}. Aidha, Kaoneka (2009) naye amefanya uchambuzi wa mofu nyambulishi katika Kisambaa kwa namna zinavyoambikwa katika kitenzi cha lugha hii. Katika uchambuzi wake amebainisha mofu nyambulishi kama zilivyobainishwa na Besha (1993) lakini amefafanua zaidi alomofu mbalimbali za mofu nyambulishi na namna zinavyojitokeza katika maumbo ya kitenzi cha Kisambaa pamoja na dhima zake za kidhamira. Katika uchambuzi huo amefafanua pia kitenzi kisintaksia kwa namna mofu nyambulishi zinavyoweza kukifanya kitenzi kuwa elekezi au sielekezi. Mofu hizo nyambulishi kutoka kwa Besha (1993: 25) zinaonekana katika mfano ufuatao;

**MF. 12**

shum-**i**-e 'vinia'

kom-**e**-a 'ulia'

mem-**ez**-a 'jaza'

kund-**ish**-a 'penda sana'

kund-**an**-a 'pendana'

Kaoneka (ameshatajwa) amefafanua mofu nyambulishi za utendwa {-**y**-}, {-**z**-}, {-**s**-}, {-**sh**-}, {-**ish**-} na {-**esh**-} ambazo zinahusiha wahusika wawili kwa namna mbili tofauti (taz. Kaoneka, 2009:58). Mofu hizi za utendwa hukifanya kitenzi kuwa elekezi. Mofu nyingine ni mofu za utendea {-**i-/-e**-} ambazo huhusisha mnufaika, kifaa au mahali katika sentensi za Kisambaa na kukifanya kitenzi kuwa elekezi. Mofu nyambulishi ya kutendana {-**an**-} ambayo ina wahusika wawili lakini inakifanya kitenzi kuwa sielekezi. Mofu za kutendwa {-**ighw**-} na {-**w**-} zinapunguza wahusika na kukifanya kitenzi kuwa sielekezi. Mofu za kutendeka {-**ik-**} na {-**ek**-} zinapunguza wahusika na kukifanya kitenzi kuwa sielekezi (Kaoneka, 2009: 73). Mofu ya ufanyikaji sana nayo ina wahusika watatu na kitenzi ni elekezi. Baadhi ya mofu hizo zinabainishwa katika mfano ufuatao.

**MF. 13**

izw-**ish**-a 'ivisha'

kam-**i**-a 'kamulia'

watato-**an**-a 'wanapigana'

to-**ighw**-a 'pigwa'

ba-**ighw**-a ‘ibwa

**Chanzo: Kaoneka (2009: 57-68)**

Pamoja na hayo, Kaoneka (2009:77) anafafanua namna mofu nyambulishi zinavyofuatana katika kitenzi cha Kisambaa. Anaeleza unyambulishaji wa mofu nne (4) katika kitenzi kimoja cha Kisambaa. Aidha, katika ufafanuzi wake anaeleza pia kuwa katika uchambuzi wa mfuatano wa mofu nyambulishi nadharia moja haikuweza kutosheleza. Hivyo, ametumia Kielelezo cha Kimofolojia cha Hyman (2003) pamoja na nadharia ya Kanuni Tazamishi ya Baker (1985). Nadharia ya Kanuni Tazamishi ya Baker (1985) imetumiwa pia na Gawasike (2011) katika kueleza mofu nyambulishi katika kitenzi cha Kikinga.

Hyman (ameshatajwa) amebainisha kielelezo cha mfuatano wa mofu ambapo kuna mofu ya Utendeshi-Utendea-Kutendana- Utendwa. Kwa kutumia kielelezo hicho, mfuatano wa mofu nyambulishi katika lugha za Kibantu unaweza kubainishwa. Aidha Kanuni Tazamishi ya Baker (ameshatajwa) inadai kuwa unyambulishaji wa kimofolojia unaakisi unyambulishaji wa kisintaksia. Hivyo kuna uhusiano mkubwa wa mofolojia na sintaksia katika unyambulishaji wa mofu. Kwa kutumia kanuni hii mpangilio wa kimofolojia hubainishwa na mfuatano wa mofu ambao ni lazima ushabihiane na mfuatano wa mofu kisintaksia katika lugha inayohusika.

Mfuatano wa mofu alioubainisha Kaoneka (ameshatajwa) ni pamoja na **Utendeshi-Utendea**, **Utendeshi- Kutendana**, **Utendea- Kutendana**, **Kutendana na Utendea**, **Utendeshi-Utendwa**, **Utendeshi- Utendea-Kutendana** na **Utendeshi-Utendea-Ufanyikaji sana-Kutendana**. Vilevile mfuatano wa mofu nyambulishi nne katika

kitenzi ambazo ni **Utendeshi-Ufanyikaji sana-Utendea-Kutendana** na **Ufanyikaji sana-Utendeshi- Utendea- Kutendana**. Katika mfuatano huo kwa mfano, mfutano wa mofu ya **utendea - kutendana** pamoja na **kutendana –utendea** haukuweza kufafanuliwa kwa kutumia Kielelezo cha Hyman (ameshatajwa).

Aidha, Kaoneka (2009: 100) anaendelea kufafanua kuwa lugha nyingi za Kibantu katika mfuatano wa mofu nyambulishi zinaweza kuelezwa kwa kutumia Kielelezo cha Hyman (CARP) lakini katika Kisambaa baadhi ya mifuatano ya mofu haiwezi kuelezwa kwa kutumia Kielelezo hicho au Kanuni Tazamishi ya Baker. Kwa hiyo, utafiti huu umeongeza maarifa ili kuliziba pengo hili katika uchambuzi na uchunguzi wa mfuatano wa mofu nyambulishi katika vitenzi vya Kisambaa kwa kutumia nadharia ya moja ya Umbo Upeo. Pengo hilo limezibwa kwa kubainisha namna mofu nyambulishi zinavyoathiriana kimofolojia au kimofofonolojia pale zinapokaa pamoja kuunda kitenzi cha Kisambaa.

Pamoja na hayo, katika ubainishaji na ufafanuzi wa mofu ambishi na mofu nyambulishi, watafiti waliotangulia hawajaonesha namna mofu hizo zinavyoathiriana zinapoambikwa katika kitenzi cha Kisambaa. Katika maumbo ya mofu mbalimbali kuna baadhi ya mofu ambazo zimetokana na kuathiriwa kimofolojia au kimofofonolojia na mofu nyingine ambazo zinaandamana nazo katika umbo la kitenzi. Hivyo basi, utafiti huu umeyafafanua masuala hayo kwa kubainisha mofu ambishi na mofu nyambulishi zinavyofuatana kwa kutumia nadharia ya Umbo Upeo.

### 2.3.2 Mofu ambishi na mofu nyambulishi katika lugha nyingine za Kibantu

Wapo wanaisimu mbalimbali ambao wamechunguza mofu zinazoambishwa kabla ya mzizi na wengine wameshughulika na mofu nyambulishi katika lugha mbalimbali za Kibantu. Miongoni mwa watafiti waliochunguza mofu ambishi katika lugha za Kibantu ni Hyman na Mchombo (1992) katika Chichewa, Dunham (2002) katika Kilangi, Mkanganwi (2002) katika Kishona, Okoa (2012) katika Kihehe, Katushemererwe (2012) katika Runyakitara. Katika tafiti hizo wamebainisha kuwa mofu zinaweza kuambishwa kabla ya mzizi ambazo ni pamoja na mofu ya ukanushi, nafsi, njeo na hali na mtendwa.

Kiango (2000) anaeleza kuwa uambishaji wa viambishi mwanzo mwa mzizi wa kitenzi haubadilishi kategoria ya neno au kuunda neno jipya bali huwa na dhima za kisarufi katika kitenzi. Mkanganwi (2002) katika kueleza uambishaji wa mofu katika lugha ya Kishona amefafanua kuwa, lugha ya Kishona ina viambishi vinavyowakilisha nambari, jinsi, njeo na hali ambavyo huambikwa mwanzoni mwa mzizi wa kitenzi. Salesio, Mukuthuria na Matundura (2016) wameshughulikia mofu (wao wakiziita mofimu) za kisarufi katika kitenzi cha lahaja ya Kichuka wamebainisha mofu zinazoambishwa na kunyambulishwa katika mzizi wa kitenzi cha lugha hiyo. Mofu ambishi ambazo zinajitokeza kabla ya mzizi wa kitenzi cha Kichuka walizobainisha ni pamoja na kiambishi (mofu) nafsi, kiambishi kibainishi, mofu ya njeo na mtendwa kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 2.5: Mofu Ambishi katika Kitenzi cha Kichuka**

| Kitenzi | Mofu ambishi | Mzizi |
|---|---|---|
| makumukamatira<br>(wamembebea) | ma- ku-mu<br>ma- nafsi ya tatu wingi<br>-ku- wakati uliopita si muda mrefu<br>-mu- mtendwa (nafsi ya kwanza umoja | -kamat- |

| | | |
|---|---|---|
| niarimaga (alikuwa akilima) | ni-a-<br>ni- kiambishi kibainishi<br>-a- nafsi ya tatu umoja | -rim- |

**Chanzo:** Salesio na wenzake (2016)

Katika jedwali hapo juu, Salesio na wenzake wanabainisha mofu ambishi katika Kichuka ambazo zina dhima za kisarufi katika kitenzi. Utafiti huu pia umebainisha namna mofu ambishi zinavyojitokeza katika kitenzi, dhima za kisarufi zinazowakilishwa na mofu hizo na namna mofu zinavyoathiriana kimaumbo zinapokaa pamoja kuunda vitenzi vya Kisambaa.

Aidha, Okoa (2012) amefafanua mofu ambishi katika lugha ya Kihehe na kubainisha kuwa lugha hii ina mofu ambishi ambazo zinaweza kuambikwa kabla au baada ya mzizi. Mofu hizo ni pamoja na mofu ya ukanushi, njeo, mtenda, mtendwa na urejeshi kama inavyoonekana katika mfano ufuatao.

**MF. 14.**

i) si- i- ly- a (hali)

Knsh-Mtd-Mz- My

ii) si-tu – ku- mu – iuk- a (hatumkumbuki)

Knsh- Mtd-Nj-Mtdw-Mz-Ky

iii) re-si-va-ka-mu- tof- il-e (asiyempiga)

Rjsh-Knsh-Mtd-Nj-Mtd-Mz-Nj-Ky

Katika mfano hapo juu Okoa anaonesha namna ambavyo kitenzi cha Kihehe huambikwa mofu kabla na baada ya mzizi wa kitenzi. Hata hivyo, Okoa (ameshatajwa) anaeleza kuwa lugha zinatofautiana katika idadi ya viambishi

vinavyoambikwa kwenye mzizi wa kitenzi. Hivyo kutokana na sifa hizo za vitenzi vya Kibantu, utafiti huu umebainisha namna mofu ambishi zinavyojitokeza katika umbo la kitenzi na namna zinavyoweza kuathiriana kimofolojia au kimofofonolojia pale zinapokaa pamoja kuunda kitenzi katika lugha ya Kisambaa. Hata hivyo, wapo wanaisimu wengine walioshunghulika na mofu ya ina moja pekee, mfano mofu njeo kama (Besha, 1985; Muzale, 1998; Mreta 1998; Mpalanzi 2010; Nyinondi, 2013; Mwashota, 2016) wakichunguza zinavyojitokeza katika lugha za Kisambaa (Kishambala), Kihehe, Kiluguru na Shimalila.

Mathalani, Besha (1985) anaeleza kuwa katika lugha ya Kisambaa kuna mofu ya njeo ya wakati uliopo yenye maumbo **-Ø-** (wakati uliopo tegemezi); **-ta-** (wakati uliopo) na **-aa-** wakati uliopo hali ya kuendelea, vilevile njeo ya wakati uliopita yenye maumbo **-te-** (wakati uliopita muda mchache); **-iye-** (jana); **-za-** (jana); **-a-** (siku ile) na **-aa-** (siku ile) pamoja na njeo ya wakati ujao yenye maumbo **ne-** ( ujao karibuni) na **nee-** (muda mrefu ujao). Ufafanuzi huu wa Besha (ameshatajwa) katika lugha ya Kisambaa unadhihirisha kuwa zipo mofu zinazounda vitenzi katika Kisambaa zikiwemo mofu zinazowakilisha njeo. Hata hivyo, utafiti wake umeshughulika na namna mofu hiyo inavyojitokeza kimofolojia na hakushughulika na namna mofu hiyo inavyoweza kuathiri au kuathiriwa na mofu nyingine kimofolojia au kimofofonolojia zinapokuwa pamoja katika umbo la kitenzi. Vilevile mabadiliko ya maumbo ya mofu njeo kutokana na athari za mofu nyingine zinapoambatana nayo wakati wa kuunda kitenzi katika Kisambaa hayajaelezwa. Hivyo, utafiti huu umeshughulika na mofu za mofimu ya njeo pamoja na mofu

nyinginezo ambazo zimechunguzwa na kuchambuliwa pamoja na kubainishwa namna zinavyoathiriana wakati zinapokaa pamoja kuunda kitenzi.

Pamoja na hayo, wapo wanaisimu walioshughulikia unyambulishaji wa mofu katika vitenzi vya lugha za Kibantu kwa maana ya kuzichunguza mofu zinazojitokeza baada ya mzizi wa kitenzi. Baadhi yao ni Besha (1993), Rugemarila (1993), Mreta (1998), Lodhi (2002), Mushi (2005), Masebo (2007), Asiimwe (2011), Gawasike (2011) na Chipalo (2013). Katika kazi zao wamebainisha mofu nyambulishi zenye mofimu ambazo zinaonekana kufanana katika lugha nyingi za Kibantu, nazo ni mofu ya mofimu ya utendea, utendwa, utendeshi, kutendana na kutendesheana. Mathalani, Mreta (1998) amechunguza unyambulishaji katika kitenzi cha Chasu na kubainisha maumbo na mfuatano wa mofu hizo. Amefafanua kuwa mofu za utendea, usababishi (utendeshi) na utendwa zinaweza kufuatana katika kitenzi kimoja.

Lodhi (2002) aliyefanya utafiti linganishi kwa kulinganisha namna unyambulishaji wa kitenzi unavyofanyika katika Kiswahili na Kinyamwezi amebainisha kuwa, katika lugha hizi kuna mfanano wa maana na matumizi ya mofu nyambulishi. Hata hivyo, kuna tofauti zinazojitokeza katika unyambulishaji wa vitenzi vya lugha hizi kama ujirudiaji wa mofu moja katika kitenzi kimoja. Vilevile, kuna mofu nyingine hazitumiki sana katika Kinyamwezi kama zinavyotumika katika Kiswahili. Lengo hapa si kufanya ulinganishi wa lugha hizo bali ni kuzingatia namna mofu nyambulishi katika vitenzi vya lugha hizi zilivyoshughulikiwa.

Besha (1993) amebainisha baadhi ya mofu nyambulishi katika Kisambaa ikiwemo

mofu ya utendwa {-ighw- na -w-}; utendea {-i- na -e-}; utendeshi {-ish-, -esh- na -ez-}; kutendeka {-ek- na -ik-} na kutendana {-an-}. Hata hivyo, katika uchambuzi wao kuathiriana kwa mofu zinazokaa pamoja kuunda kitenzi na matokeo ya kuathiria kwa mofu hizo hakujashughulikiwa. Hivyo, utafiti huu ulishughulika na kuziba pengo hilo katika lugha ya Kisambaa ambayo ni lugha mojawapo ya Kibantu. Kwa upande mwingine, Gawasike (2011) ambaye ametafiti mfuatano wa mofu nyambulishi (akiziita mofimu) katika kitenzi cha Kikinga amefafanua namna mofu hizo zinavyojitokeza baada ya mzizi wa kitenzi. Amebainisha kuwa Kikinga kina mofu nyambulishi ya kutendea yenye umbo -**il**-, fanyizi (tendesha) -**its**-, kutendana -**an**-, kutendeka -**ikh**- na kutendwa -**w**- kama katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 2.6: Mofu Nyambulishi katika Kitenzi cha Kikinga**

| **Kitenzi** | **Mzizi** | **Mofu Nyambulishi** |
|---|---|---|
| tamila (kalia) | tam- | -il- |
| tamitsa (kalisha) | tam- | -its- |
| londana (tafutana) | lond- | -an- |
| tamikha (kalika) | tam- | -ikh- |
| nyilwa (kimbiwa) | nyil- | -w- |

**Chanzo:** Gawasike (2011)

Katika jedwali hapo juu, Gawasike amebainisha kuwa Kikinga kina mofu nyambulishi ya kutendea yenye umbo -**il**-, fanyizi (tendesha) -**its**-, kutendana -**an**-, kutendeka -**ikh**- na kutendwa -**w**-.

Naye Asiimwe (2011) amewasilisha mpangilio wa viambishi nyambulishi katika kitenzi cha Runyankore. Katika utafiti wake amebainisha kuwa katika lugha ya Runyankole mofu zinazoambikwa baada ya mzizi wa neno ni **-ir-**, **-er-** mofimu ya kutendea, -**es-**, **-sy-** kutendesha, -**ek-**, **-ik-** kutendeka, **-w-**, **ebw-**, **ibw-** kutendwa na **-an-**, -**angan-** kutendana. Katika mpangilio wa mofu hizo mofu ya mofimu ya

kutendea haiwezi kuwa pamoja na mofu ya mofimu ya kutendesha katika kitenzi. Vilevile, mofu ya mofimu ya utendeshi haikai pamoja na mofu ya mofimu ya kutendeka katika vitenzi nya Runyankole. Pamoja na hao, katika lugha ya Kisambaa vilevile mofu nyambulishi zimebainishwa na Besha (1993) na Riedel (2009). Watafiti hao wamebainisha kuwa Kisambaa kina mofu mbalimbali zinazoambikwa baada ya mzizi wa kitenzi kama mofu za utendea **-i-** na **-e**-, utendesha **-iz-** na **-ez-**, kufanya jambo kwa kuzidisha **-ish-** na **-esh-,** kutendwa **-ighw-** na **-w-**, kutendeka **-ik-** na **-ek-** na kutendana **-an-** .

Hivyo, tafiti hizo zinatubainishia kuwa lugha za Kibantu zina viambishi vinavyoambishwa na vinavyonyambulishwa katika mzizi wa kitenzi ikiwemo lugha ya Kisambaa. Kwa hiyo, utafiti huu wa mofu zinazounda kitenzi katika Kisambaa umelenga kuchambua na kuchunguza namna mofu hizo zinavyoathiriana kimofolojia au kimofofonolojia zinapokaa pamoja kuunda kitenzi cha Kisambaa vyenye maumbo mbalimbali. Kuathiriana huko kwa mofu kumebainishwa kwa kuzingatia mashartizuizi yanayotawala uambishaji na unyambulishaji wa mofu katika kitenzi cha Kisambaa.

### 2.3.3 Kuathiriana kwa mofu katika vitenzi vya lugha za Kibantu

Mofu zinapoambikwa katika mzizi wa kitenzi zinaweza kuathiriana. Baadhi ya athari zinazojitokeza kutokana na kuambikwa kwa baadhi ya mofu katika mzizi wa kitenzi zimebainishwa katika lugha za Kibantu kama Shimalila (Mwashota, 2016) na Kikuria (Charwi, 2011). Mwashota (ameshatajwa) amefafanua athari za mofu njeo kifonolojia katika kitenzi cha lugha ya Shimalila, ameonesha kuwa katika lugha hii uambishaji wa mofu ya mofimu ya njeo ya wakati uliopita na ujao katika mzizi wa

kitenzi husababisha mabadiliko ya kifonolojia katika mzizi, kiambishi tamati na toni katika mofu ya nafsi inayoambikwa pamoja na mofu njeo kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 2.7: Athari ya Mofu Njeo katika Kitenzi cha Shimalila**

| **Kitenzi Asili** | **Kiambishi cha Wakati** | **Mzizi** | **Kiambishi tamati** |
|---|---|---|---|
| yinga | áyinj**il**e (alitetemeka) | -yinj- | -e |
| gana | ágan**il**e (alipenda) | -gan- | -e |
| liga | álij**il**e (alioa) | -lij- | -e |
| lega | a**ti**leje (atakwepa) | -lej- | -e |
| liga | a**ti**lije (atatukana) | -lij- | -e |
| sya | a**ti**sye (atasaga) | -sy- | -e |

**Chanzo:** Mwashota (2016)

Katika jedwali hapo juu Mwashota (2016) anabainisha kuwa, mzizi wa kitenzi chenye sauti /g/ ambayo ni kipasuo ghuna cha kaakaa laini ukiambikwa mofu njeo ya wakati uliopita **-il-** au ujao **-ti-** hubadilika kuwa konsonanti /**Ɉ**/. Vilevile, kiambishi tamati **-a** hubadilika kuwa **-e** katika kitenzi chenye mofu ya wakati uliopita au ujao na katika wakati uliopita toni katika mofu nafsi iliyoambishwa ni toni juu. Hivyo, tofauti na lugha ya Shimalila ambayo imeshughulikia kuathiriana kwa mofu kifonolojia, utafiti huu umeshughulika na athari za kimofolojia au kimofofonolojia katika maumbo ya kitenzi cha Kisambaa. Mofu ambishi na nyambulishi zimebainishwa namna zinavyoathiriana katika maumbo yake kwa kuzingatia mashartizuizi ya lugha hii yanayotawala uambikaji wa mofu katika mzizi au shina la kitenzi.

Vilevile, Charwi (2011) katika uchunguzi wake wa vitenzi vya lugha ya Kikuria amebainisha namna unyambulishaji wa kitenzi unavyoleta athari za kisintaksia

katika uelekezi wa kitenzi cha lugha hiyo. Amefafanua kuwa, katika Kikuria mzizi wa kitenzi unapopokea mofu (akiita viambishi) nyambulishi huweza kuongeza au kuondoa sifa ya kitenzi kuwa elekezi kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 2.8: Athari za Viambishi Nyambulishi Kisintaksia**

| **Kitenzi elekezi** | **Unyambulishi** | **Matokeo** |
|---|---|---|
| Nyagie **ahancha** mokae (Nyagige anampenda mkewe) – kitenzi elekezi | bhahanch-**an**-a (wanapendana) | Nyagige na mokae **bhahanchana** (Nyagige na mkewe wanapendana - kitenzi sielekezi |
| omoona **arakúúra** (mtoto analia)- | arakóór-**er**-a (analilia) | Omoona **araarakóórer** eghekebhi (mtoto analilia kisu)- kitenzi elekezi |
| abhaana **bharatuka** amasimo (watoto wanachimba mashimo) –kitenzi elekezi | aratuk-**i**-a (anawachimbisha) | Marwa **aratukia** abhaana amasimo (Marwa anawachimbisha watoto mashimo) – kitenzi elekezi |
| abhaana **bhhararúta** urusiri (watoto wanavuta kamba) - kitenzi elekezi | rurarút-**w**-a (inavutwa) | urusiri **rurarútwa** na abhana (kamba inavutwa na watoto) -kitenzi si elekezi |

**Chanzo:** Charwi (2011)

Ufafanuzi huo unabainisha kuwa kitenzi cha Kikuria kinaponyambulishwa kinaweza kubadilika kutoka kuwa kitenzi elekezi kuwa si elekezi au kutoka si elekezi kuwa kitenzi elekezi. Vitenzi elekezi ni vitenzi vyenye sifa ya kupokea yambwa katika tungo. Katika lugha ya Kikuria, kiambishi nyambulishi cha kutendana na kutendwa hukifanya kitenzi elekezi kuwa si elekezi, kinyambulishi cha kutendea na kutendesha hukipa kitenzi si elekezi kuwa na sifa ya uelekezi. Athari hizi za mofu nyambulishi katika Kikuria ni za kisintaksia ambapo mofu zinaponyambulishwa katika kitenzi huathiri vipashio vinavyoweza kuambatana na kitenzi. Je, mofu katika kitenzi cha lugha ya Kisambaa zinaathirianaje kimofolojia au kimofofonolojia? Hivyo, utafiti huu umeshughulika na kuathiriana kwa mofu kimofolojia au kimofofonolojia pale mofu hizo zinapoambishwa ama kunyambulishwa katika mzizi wa kitenzi cha lugha ya Kisambaa.

Aidha, katika kitenzi cha lugha ya Kihaya mofu zinaathiriana kimofonolojia ambapo toni hubadilika kutoka katika mzizi wa kitenzi kwenda kwenye yambwa. Kuhama kwa toni hutokea katika kitenzi cha wakati uliopo kinapoambatana na yambwa (Nurse 2008:211) kama katika mifano ifuatayo.

**MF. 15**

ba-Ø-kóma 'wanafunga'

ba- Ø-koma Káto 'wanamfunga Kato'

Pia katika wakati uliopo hali ya mazoea toni katika mzizi wa kitenzi huondoshwa kutokana na kitenzi kinachohusika kuambatana na yambwa.

**MF. 16**

ba-a- kóm-aga 'hufunga'

ba-a-kom-aga Káto 'humfunga Kato'

Mifano hiyo inadhihirisha kuwa katika lugha ya Kihaya mofu mzizi katika kitenzi hupoteza sifa ya kuwa na toni kutokana na kitenzi kuambatana na yambwa.

Vilevile, katika kitenzi cha lugha ya Runyambo, mofu ya njeo ya wakati uliopita -**ír-** na njeo ya wakati timilifu -**a**-,-**ir**- huhitaji mofu yakinishi -**e** na si -a (Rugemalira, 1993). Pia, kuwepo kwa mofu ya njeo ya wakati ujao -**raa-** na mofu ya ukanushi katika kitenzi, umbo la kitenzi hicho huhitaji mofu yakinishi -**e**. Pia mofu ambishi -**ag**- ambayo huambatana na mofu ya ukanushi ni lazima itokee katika umbo la kitenzi ikiwa pamoja na mofu ya ukanushi na mofu ya wakati uliopita -**ka**- lakini mofu hizi si lazima zitokee pamoja na mofu hiyo. Swali linaloibuliwa hapa ni kuhusu kuathiriana kwa mofu zinazounda kitenzi cha lugha ya Kisambaa. Kwa hiyo,

utafiti huu umelenga kuchunguza na kufafanua namna maumbo ya mofu yanavyoathiriana wakati mofu hizo zinapokaa pamoja kuunda kitenzi. Kuathiriana huko kwa mofu kimofolojia au kimofofonolojia kumefafanuliwa kwa kuzingatia mashartizuizi katika lugha ya Kisambaa ambayo yanatawala uambikaji wa mofu katika kitenzi.

Kwa hiyo, mofu ambishi na mofu nyambulishi katika lugha nyingi za Kibantu zimeainishwa na kubainishwa kama inavyoonekana katika tafiti zilizotangulia. Hii inathibitisha kuwa kila lugha ina utaratibu wake wa kuambisha na kunyambulisha mofu katika mzizi wa kitenzi. Pia mofu hizo zina maana na dhima za kisarufi katika lugha. Hata hivyo, watafiti wengi waliochunguza mofu katika lugha za Kibantu wameziita mofu hizo kuwa ni mofimu. Hivyo katika ubainishaji wa mofu katika kitenzi cha lugha ya Kisambaa tumezingatia tofauti ya mofu, mofimu na alomofu. Mofu hizo zimechambuliwa kwa kubainisha utaratibu unaokubalika katika lugha ya Kisambaa.

Vilevile, katika tafiti zilizotangualia athari za mofu katika vitenzi vya lugha za Kibantu zimebainishwa kwa namna tofauti tofauti, zipo athari za kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia. Pamoja na hayo kuathiriana kwa maumbo ya mofu zinapokaa pamoja kuunda kitenzi katika lugha ya Kisambaa bado hakujajulikana. Kwa hiyo, utafiti huu umeshughulikia namna mofu zinavyoathiriana kimofolojia au kimofofonolojia zinapokaa pamoja kuunda kitenzi cha lugha ya Kisambaa kwa kuzingatia mashartizuizi ya lugha hii.

## 2.4 Pengo la utafiti

Kutokana na tafiti tangulizi zilizochunguza mofu mbalimbali katika lugha ya Kisambaa pamoja na lugha nyingine za Kibantu bado uchunguzi zaidi unahitajika katika lugha ya Kisambaa kuhusu mofu ambishi na nyambulishi. Watafiti walioshughulika na mofu katika umbo la kitenzi cha Kisambaa kama Besha (1985, 1993), Peterson (2008), Riedel (2009) na Kaoneka (2009) hawajachunguza namna mofu hizo zinavyoathiriana kimofolojia au kimofonolojia zinapokaa pamoja katika kuunda kitenzi cha Kisambaa kwa kuzingatia mashartizuizi ya lugha hii. Hivyo utafiti huu umekusudia kuliziba pengo hilo la namna mofu ambishi zinavyoathiriana na mofu nyambulishi zinavyoathiriana katika mfuatano wa mofu hizo kwenye umbo la kitenzi.

## 2.5 Kiunzi cha nadharia

Kwa mujibu wa maelezo ya Massamba (2009), nadharia ni taratibu, kanuni na misingi ambayo imejengwa katika muundo wa kimawazo kwa madhumuni ya kutumika kama kiolezo cha kuelezea jambo. Utafiti wa kiisimu una dhima ya kuchunguza lugha na uchunguzi huo wa kiisimu hufanyika katika misingi ya nadharia za kiisimu. Miongoni mwa nadharia za kiisimu, zipo nadharia zinazoongoza uchambuzi wa mofolojia ya lugha. Nadharia hizo ni pamoja na nadharia ya Mofolojia Ambishi yenye mkabala wa Faridi na Michakato ambayo iliasisiwa na Hockett (1958).

Msingi wa nadharia ya Mofolojia Ambishi ni kwamba katika uundaji wa maneno kuna viapashio ambavyo vinaambikwa katika mzizi au shina na kila kiambishi katika umbo neno kina nafasi yake na kazi yake. Uchanganuzi wa kimofolojia vilevile

unaongozwa na Nadhariatete iliyojengwa kwenye Neno iliyoasisiwa na Mark Aronoff (1976) ambaye anaeleza kuwa michakato ya uundwaji wa maneno imejengwa katika neno na neno jipya huundwa kwa kutumia kanuni ya kawaida katika neno moja lililopo tayari, lakini neno jipya na neno lililopo ni sehemu ya kategoria kuu ya leksika. Nadhariatete iliyojengwa kwenye Neno ni nadharia ya kimajumui na si ya lugha fulani mahususi. Suala la Sarufi Majumui ndio limekuwa likichagiza uanzishwaji wa viunzi mbalimbali vya nadharia katika uchanganuzi wa vipengele vya kiisimu.

Katika kuchanganua na kubainisha namna mofu zinavyoathiriana kutokana na mchakato wa uambishaji na unyambulishaji wa mofu, imetumika nadharia ya Umbo Upeo. Nadharia ya Umbo Upeo (UU) ni nadharia iliyoibuliwa miaka ya hivi karibuni. Kiunzi hiki cha nadharia kiliasisiwa na wanaisimu Prince na Paul Smolensky (1993) ambao waliutambulisha mswada uliojulikana kama “Optimality Theory: Constraint Interaction in Generative Grammar” ambao haukuchapishwa hadi mwaka 2004. Kiunzi hiki baadaye katika mwaka huo huo 1993 kikaendelezwa na John J. McCathy na Allan Prince.

Nadharia ya Umbo Upeo iliibuka kutokana na matatizo yaliyojibainisha katika Kiunzi Rasmi cha Fonolojia Zalishi kuhusu udhahania wa uwakilishi wa vipengele vya kifonolojia (Massamba 2011). Allan na Smolensky (2004) kwa mujibu wa maelezo yao walijaribu kuachana na sheria za ukokotozi wa umbo la ndani hadi kulifikisha umbo la nje na kupunguza udhahania ambao ulionekana katika kazi ya “Sound Patterns of English (SPE)” ya Chomsky na Halle (1968). Badala ya kujihusisha na kukokotoa umbo la ndani hadi umbo la nje hatua kwa hatua, nadharia

hii imekuja na misingi ya kutumia mashartizuizi ya kimajumui ambayo huweka vigezo vya kutathmini maumbo mbalimbali ya lugha yanayozalishwa katika hatua moja na kwa pamoja ili kupata umbo linalokubalika kutokana na sarufi ya lugha inayohusika.

Pamoja na hayo, madhumuni ya mwanzo ya kuanzishwa kwa nadharia hii yalikuwa kushughulikia masuala ya kifonolojia. Hata hivyo, baadaye kiunzi hiki kimetumiwa kushughulikia masuala ya kisintaksia (Grimshaw 1997, Ackema na Neeleman 1998, Dekkers na wenzake 2000) pamoja na mofolojia (Legendre 2000, Wunderlich 2001). Kwa hiyo basi, utafiti huu umetumia nadharia ya Umbo Upeo (UU) kwa kuwa ni nadharia mpya katika uchambuzi wa vipengele vya kiisimu na inafaa kuchambua vipengele vya kimofolojia kwa kufuata mashartizuizi ambayo ni ya kimajumui.

Madai ya msingi ya nadharia ya Umbo Upeo ni kwamba miundo mbalimbali ya lugha hujengwa kwa kuzingatia mikinzano kati ya mashartizuizi (MASHAZU) yaliyopo katika lugha inayohusika. Nadharia hii inadai kuwa sarufi majumui hujumuisha MASHAZU yanayoweka vigezo vya ukubalifu wa maumbo ya lugha zote duniani ambayo ndio hutumika kuundia sarufi ya lugha moja moja (Prince na Smolensky, 1993). Hii ina maana kwamba, tofauti zilizopo katika lugha za binadamu ni upangiliaji wa MASHAZU hayo ya kimajumui ambayo yanapangwa kimsonge (Massamba 2011).

MASHAZU yanapangwa kimsonge kulingana na nguvu ya thamani yake katika kuamua ukubalifu wa umbo linalozalishwa katika sarufi ya lugha inayohusika na wala si kanuni (Prince, 2002; McCarthy, 2002). MASHAZU ni masharti

yanayotuambia kwamba ukitaka kupata umbo fulani kwa usahihi kabisa basi unatakiwa utumie kanuni fulani na si kanuni fulani. Kwa mfano, katika Kiswahili mashartizuizi yanayojitokeza katika lugha hii ni kama katika mfano ufuatao.

**MF. 17**

| | | |
|---|---|---|
| a) | *mukutano | mkutano |
| b) | *mutu | mtu |
| c) | *mutoto | mtoto |
| d) | *mujukuu | mjukuu |

**Chanzo:** Massamba (2011)

Kutokana na mfano huo inadhihirika kuwa katika Kiswahili, mofu yoyote katika neno inayoanza na kiambishi {mu-} na kufuatwa na konsonanti halisi hujikuta ikipoteza irabu [u] na hatimaye maneno kama mutu kuwa mtu.

Vilevile, nadharia ya Umbo Upeo imejengwa katika misingi mikuu mitatu (3) ambayo ni Mashartizuizi (MASHA-ZU), Zalishi (ZALI) na Tathmini (TATHI). Msingi wa MASHA-ZU ambao ndio kiini cha nadharia hii, ni msingi ambao unahusu uwekaji vigezo na masharti yasiyoweza kuvunjwa na yanayoweza kuvunjwa. Kupitia vigezo hivyo ndipo uamuzi wa umbo linaloweza kufikia upeo wa ukubalifu hufanyika, kwa maana ya kwamba lile umbo ambalo ama halikuvunja masharti yoyote au ambalo limevunja masharti yanayoweza kuvumilika ndio linapewa ushindi. MASHA-ZU haya yanapangiliwa kimsonge kulingana na nguvu yake katika kuamua ukubalifu wa umbotokeo lililozalishwa na kukidhi vigezo vyote vya MASHA-ZU hayo.

MASHA-ZU kulingana na nadharia hii yamegawanyika katika makundi mawili ambayo ni MASHA-ZU ya uadilifu na MASHA-ZU ya uziada. MASHA-ZU ya uadilifu hujumuisha familia ya MASHA-ZU ya utangamano. MASHA-ZU haya yanahitajia kuwepo kwa mfanano baina ya umboghafi na umbotokeo (Prince na Smolensky, 2003). Katika MASHA-ZU haya ya utangamano kuna MASHA-ZU yanayozuia udondoshaji wa vitamkwa vilivyomo katika umbo ghafi ambayo huitwa FIKI-UKO (Fikia Ukomo wa Utangamano). Pia kuna MASHA-ZU ambayo huhitajia kwamba vitamkwa vilivyomo katika umbotokeo vitegemee vile vilivyomo katika umboghafi yaani, TEGE. Mashartizuizi haya ya TEGE yanazuia uchopekaji wa vitamkwa katika umbotokeo. MASHA-ZU mengine ya utangamano ni SHABI (Shabihiana) ambayo yanahitajia kwamba sifa za vitamkwa katika umbotokeo zishabihiane na zile zilizo katika umboghafi.

Pamoja na hayo, familia ya MASHA-ZU ya uziada ni yale yanayoruhusu mabadiliko katika umboghafi ili kuyafanya maumbotokeo yakubalike katika sarufi ya lugha inayohusika. MASHA-ZU ya uziada hulifanyia tathmini umbo kwa kuyapa kipaumbele mabadiliko ya umbotokeo likilinganishwa na umboghafi yanayoleta ukubalifu katika sarufi ya lugha inayohusika (Massamba, 2011).

Katika msingi wa ZALI kuna maumbo tokeo mbalimbali ambayo pia yanaweza kuitwa maumbo shindani ambayo huzalishwa. Sababu ya kuitwa maumboshindani ni kuwa katika maumbo hayo ndipo umbo linaloweza kufikia upeo wa ukubalifu hupatikana. Katika maumboshindani umbo litakaloshinda huwa ndio limefikia upeo wa ukubalifu. Pamoja na umbo hilo kufikia upeo wa ukubalifu, linaweza kuwa

limevunja mashartizuizi kadhaa lakini kwa kuwa mashartizuizi hayo ni ya hali ya chini na yanaweza kuvumilika litahesabika kuwa ndio lililofikia upeo wa ukubalifu katika lugha hiyo. Hivyo, kwa mujibu wa nadharia hii ukiwa na maumboghafi yoyote yale ZALI huweza kuzalisha maumbotokeo au maumboshindani katika idadi isiyo na ukomo. Katika maumbotokeo yanayozalishwa kulingana na mpangilio wa mashartizuizi katika lugha inayohusika litapatikana umbo lililofikia upeo wa ukubalifu.

Kwa upande wa msingi wa TATHI, hiki ni kipengele muhimu ambacho hutumika kuamua ni umbo lipi kati ya maumbotokeo yaliyozalishwa limefikia upeo wa ukubalifu. Katika seti ya MASHA-ZU yenye mashartizuizi yenye nguvu na yasiyo na nguvu ndipo tathmini hufanyika kwa kuangalia ni memba yupi katika jumla ya washindani amevunja masharti kidogo, yupi amevunja mashartizuizi mengi na yupi amevunja yale ya chini kabisa yanayoweza kuvumilika. Hata hivyo, sambamba na misingi hiyo ipo mihimili minne ya nadharia ya Umbo Upeo (Massamba, 2011) ambayo ni:

i. Umajumui: Sifa hii inabainisha kuwa sarufi majumui inatoa seti ya MASHA-ZU ambayo ni ya kimajumui na yanapatikana katika sarufi za lugha zote za wanadamu. Hivyo, kwa kuwa MASHA-ZU haya yamo katika lugha zote basi kila mpangilio wa MASHA-ZU ni sarufi ya lugha fulani.

ii. Uvunjwaji/ukiukwaji: kwamba MASHA-ZU yanaweza kuvunjwa au kukiukwa ili kukidhi ukubalifu wa sarufi ya inayohusika. Ukiukwaji ukiwa ni wa kukiuka MASHA-ZU yenye nguvu, hauvumiliki katika sarufi ya lugha

inayohusika na kulifanya umbotokeo lililovunja MASHA-ZU hayo kuwa si kubalifu.

iii. Upangiliaji: MASHA-ZU hupangiliwa kimsonge kulingana na nguvu au uhafifu wake katika kuamua ukubalifu wa umbotokeo kulingana na sarufi ya lugha mahususi. MASHA-ZU hayo hupwangwa kimsonge katika jedwali ambapo ndipo mchakato wa ufanyikaji wa tathmini hutokea (McCarthy, 2007; Massamba, 2011). MASHA-ZU yaliyopangwa juu zaidi (kushoto zaidi katika jedwali la MASHA-ZU) katika msonge yakivunjwa hayavumiliki na yale ya chini (kulia zaidi katika jedwali la MASHA-ZU) huvumilika.

iv. Usambamba: kwamba tathmini ya maumbotokeo au maumboshindani ifanywe kwa hatua moja. Usambamba unakataa uwepo wa mzunguko wa kanuni na hatua za uwakilishi wa maumbo yanayozalishwa katika uzungumzaji wa lugha. Katika uchanganuzi wa maumbo yaliyozalishwa, hakuna uwakilishi wa umbo la ndani, umbo la kati au umbo la nje bali uchanganuzi katika Umbo Upeo unahusu umboghafi na maumbotokeo tu yanayozalishwa na ZALI. Katika nadharia hii kuna ujumuishwaji wa hatua za kiuchanganuzi. Vilevile, McCarthy na Cohn (1998) wanaongezea kuwa kipengele cha usambamba kinafanya kazi kwa kuyatathmini maumboshindani yaliyokamilika na yenye kupitia athari zote za michakato ya kifonolojia na kimofolojia katika hatua moja.

Vilevile uchanganuzi wa data kwa kutumia nadharia ya Umbo Upeo hufanyika kwa kutumia majedwali ya ukiukwaji wa MASHA-ZU (Massamba, 2011). MASHA-ZU hayo yanapangwa katika safu ya juu na maumbotokeo au maumboshindani

yanapangwa upande wa kushoto kuelekea chini. Majedwali hayo yanayoonesha mpangilio wa MASHA-ZU kimsonge huwa na visanduku ambavyo huandikwa alama mbalimbali za uvunjwaji wa MASHA-ZU hayo. Hatua ya kwanza katika uchanganuzi wa data ni kuichunguza data na kuunda MASHA-ZU, kisha kuyafafanua na kuyapanga kulingana na nguvu yake katika kuamua ukubalifu wa umbotokeo katika maumbotokeo yaliyozalishwa. Hatua inayofuata ni uchanganuzi unaofanyika katika hatua moja kwa kutumia majedwali ambapo alama zinazoonesha kiwango cha uvunjaji wa MASHA-ZU hutumika kuonesha uvunjaji huo. Mashauri (2013) ametumia nadharia hii katika kuchanganua miundo ya silabi za Kiswahili sanifu. Mfano, amechanganua silabi yenye muundo wa Irabu peke yake.

**MF. 18**

Maumboghafi: oa, ua

Muundo wa silabi wenye irabu peke yake katika Kiswahili unazalishwa kwa MASHA-ZU ya uadilifu yafuatayo.

i. TangaMawa(ê) ambalo huhitajia kwamba kila silabi iwe katika mawanda silabi yake ili itamkike.

ii. Onyesha (Mfadhi-$K_n$) ambalo linahitajia mfadhili kiini aonyeshwe katika mawanda silabi ili silabi iwe na irabu.

iii. Pekee (Mfadhi-$K_n$) linalozuia silabi kuwa na irabu mbili katika mawanda silabi yake.

iv. Onyesha (Mfadhi-$M_z$ê) linalohitaji silabi kuwa na mwanzo silabi ingawa ni hafifu katika muundo wa silabi yenye irabu peke yake.

Mpangilio wa Mashartizuizi: **TangaMawa(ê) ›› Onyesha (Mfadhi-$K_n$) ›› Pekee (Mfadhi-$K_n$) ›› Onyesha (Mfadhi-$M_z$ê)**

**Jedwali 2.9: Umboghafi oa**

| **\$o\$\$a\$** | **Seti ya MASHA-ZU** | | | |
|---|---|---|---|---|
| | TangaMawa(ê) | Onyesha (Mfadhi-$K_n$) | Pekee (Mfadhi-$K_n$) | Onyesha (Mfadhi-$M_z$ê) |
| **a. (oa)** | *! | ** | | * |
| **b. (o)a** | *! | | | * |
| **c. o(a)** | *! | | | * |
| **d. (o) (a)** | | | | * |

**Chanzo:** Mashauri (2013)

Katika jedwali hapo juu, tunaona umboghafi **oa** ambalo limeingizwa katika kipengele cha ZALI na kuzalisha maumbotokeo (a) – (d). Kipengele cha TATHI kikafanya tathmini ya umbotokeo lililofikia upeo wa ukubalifu katika muundo wa silabi za Kiswahili sanifu. Tathmini hiyo imefanywa kwa kutumia kigezo cha kukidhi vigezo vilivyowekwa katika MASHA-ZU yaliyopangwa kimsonge kwa kuzingatia unguvu wake.

Hivyo basi, katika jedwali hilo tunaona kuwa umbotokeo (a) limekiuka shartizuizi lenye nguvu kabisa kwa kuingiza silabi mbili katika mawanda silabi moja hivyo kuondoa utangamano wa kila silabi na mawanda silabi yake. Vilevile, umbotokeo hili limekiuka shartizuizi linalohitajia kuwa na mfadhili kiini mmoja tu katika mawanda silabi kwa kuingiza irabu mbili katika mawanda silabi moja pamoja na shartizuizi hafifu ambalo linahitaji silabi kuwa na mwanzo silabi wake. Maumbotokeo (b) na (c) yamekiuka mashartizuizi yenye nguvu yanayohitaji kwamba kila silabi iwe katika mawanda silabi yake pamoja na shartizuizi linalohitaji

kuonyeshwa kwa mfadhili mwanzo silabi katika mawanda silabi. Umbotokeo (d) limekiuka shartizuizi moja linalohitaji kuonyeshwa kwa mfadhili mwanzo wa silabi katika mawanda silabi lakini umbo hili ndio limeshinda kwa kuwa shartizuizi hili ni hafifu na linavumilika katika sarufi ya lugha ya Kiswahili.

Kwa hiyo, nadharia ya Umbo Upeo imechaguliwa kutumika katika uchunguzi na ufafanuzi wa namna mofu zinavyoathiriana pale zinapoambikwa katika mzizi wa kitenzi cha Kisambaa ili kuunda kitenzi cha lugha hii. Muathiriano wa mofu katika umbo la kitenzi unatokana na michakato ya kimofolojia au kimofofonolojia. Hata hivyo, mwingiliano wa taaluma ya fonolojia na mofolojia katika uambikaji wa mofu unafaa kuelezwa kwa kutumia nadharia hii kutokana na mihimili yake ya kiuchanganuzi ya usambamba na ujumuishwaji.

Usambamba na ujumuishwaji ni mihimili muhimu katika uchanganuzi unaozingatia nadharia ya Umbo Upeo kwani inatoa utoshelevu wa kimaelezo wa mwingiliano wa MASHA-ZU katika uchanganuzi wa hatua moja (McCarthy na Cohn, 1998). McCarthy na Cohn (wameshatajwa) wanaendelea kueleza kuwa mhimili wa usambamba unafanya kazi ya kuyatathmini maumbotokeo ambayo yamekamilika na yenye kupitia athari za kifonolojia na kimofolojia katika hatua moja. Kwa hiyo, mwingiliano wa viwango vya sarufi unaweza kuchanganuliwa bila kuwa na hatua nyingi za uchanganuzi. Hivyo basi, usambamba unaweza kueleza mwingiliano wa viwango vya sarufi kwa kutumia kigezo cha nguvu ya shartizuizi la kiwango fulani katika kukidhi vigezo vya ukubalifu wa umbo linaposhindanishwa na shartizuizi la kiwango kingine katika hatua moja ya mpangilio wa MASHA-ZU hayo.

Pamoja na hayo, uchanganuzi wa maumbo mbalimbali ya kitenzi cha lugha ya Kisambaa ambayo yanatokana na kuambishwa au kunyambulishwa kwa mofu umefanywa kwa kutumia misingi yote mitatu ya MASHA-ZU, ZALI na TATHI. Maumbo ya kitenzi katika utafiti huu yamebainishwa kwa kutumia jedwali la seti ya MASHA-ZU yanayotakiwa kufuatwa katika mchakato wa uambikaji wa mofu katika kitenzi cha Kisambaa ili kuonesha tabia ya vitenzi vya lugha hii. Vilevile, katika namna mofu zinavyoathiriana, MASHA-ZU ya lugha ya Kisambaa yanayotawala katika uambishaji na unyambulishaji wa kitenzi cha Kisambaa ndiyo yanayobainisha kuathiriana huko. Maumbo ya kitenzi ambayo yana mabadiliko kutokana na kuathiriana kwa mofu yamebainishwa kwa kutumia seti ya MASHA-ZU yaliyopangiliwa kulingana na sarufi ya lugha ya Kisambaa.

Sambamba na hayo, katika uwasilishaji wa mashartizuizi yanayotawala uambikaji wa mofu katika vitenzi vya Kisambaa ZALI imetumika kuzalisha maumbotokeo mbalimbali kulingana na maumboghafi yaliyomo katika lugha ya Kisambaa. Kwa mujibu wa nadharia hii, maumbotokeo hayo huzalishwa kwa idadi isiyo na ukomo. Maumbotokeo yaliyozalishwa yametathminiwa kwa vigezo vya MASHA-ZU katika seti ya MASHA-ZU ili kuamua ni umbotokeo lipi katika maumbotokeo yaliyopo limeweza kufikia upeo wa ukubalifu kulingana na sarufi ya lugha ya Kisambaa. Msingi wa TATHI umetathmini maumbotokeo yaliyozalishwa ambayo yanatokana na uambikaji wa mofu na hivyo kuthibitisha ukubalifu wa maumbo hayo ya vitenzi kulingana na mpangilio wa mashartizuizi katika sarufi ya lugha ya Kisambaa.

Hivyo, nadharia ya Umbo Upeo katika utafiti huu imeweza kutumika katika uchanganuzi wa data na kufikia malengo mahususi ya utafiti huu. Katika malengo

mahususi hayo: Lengo la kwanza linahusu ubainishaji wa mofu ambishi na mofu nyambulishi pamoja na mofimu zake ambapo mfuatano na mpangilio wa mofu hizo umebainishwa kwa kuzingatia mashartizuizi yanayotakiwa kufuatwa katika maumbo ya kitenzi. Aidha, lengo la pili la utafiti huu ambalo limehusu uchanganuzi wa namna mofu zinavyoathiriana kimofolojia na kimofofonolojia pale zinapokaa pamoja kuunda kitenzi chenye maumbo mbalimbali katika lugha ya Kisambaa limetimizwa pia kwa kutumia nadharia ya Umbo Upeo.

Mashartizuizi ya lugha ya Kisambaa katika mfuatano wa mofu yamemuongoza mtafiti kuchunguza mofu zinazoathiri na zinazoathiriwa na mofu nyingine zinapoambishwa au kunyambulishwa katika mzizi wa kitenzi cha Kisambaa. Maumbo ya kitenzi ambayo yana mabadiliko kutokana na kuathiriana kwa mofu zinazounda kitenzi hicho yamefafanuliwa kwa kutumia jedwali la seti ya mashartizuizi. Vilevile mashartizuizi yanayotawala mfuatano na mpangilio wa mofu katika uambikaji wa mofu hizo yamebainishwa na kufafanuliwa ili kulifikia lengo la tatu la utafiti huu.

### 2.6 Muhtasari wa sura

Katika sura hii, tumefafanua dhana za mofu, mofimu na alomofu zinavyofasiliwa na wanaisimu mbalimbali, pamoja na kubainisha namna dhana ya mofu na mofimu zinavyotofautiana. Aidha, tumeonesha mofu ambishi na nyambulishi za kitenzi cha lugha ya Kisambaa pamoja na lugha nyingine za Kibantu. Pia, sura hii imeonesha kuathiriana kwa mofu katika lugha nyingine za Kibantu. Pamoja na hayo, tumebainisha pengo linalojitokeza katika tafiti hizo na kutufanya tuchague kuchambua na kuchunguza mofolojia ya kitenzi cha lugha ya Kisambaa kwa namna

mofu zinavyoathiriana kimofolojia au kimofofonolojia. Vilevile, katika sura hii tumebainisha na kufafanua nadharia iliyotumika katika uchambuzi wa mofu na ufafanuzi wa namna mofu hizo zinavyoathiriana wakati wa kuunda kitenzi na mashartizuizi yanayotawala uambishaji na unyambulishaji wa mofu katika vitenzi.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inafafanua muundo wa utafiti, eneo la utafiti, watoa taarifa, sampuli na usampulishaji. Pia, inahusu mbinu za kukusanyia data na namna mbinu hizo zilivyotumika kupata data ya utafiti huu, namna data zilivyochanganuliwa na maadili ya utafiti yalivyozingatiwa.

## 3.2 Muundo wa utafiti

Utafiti huu ni wa lugha katika uwanja wa isimu ambapo ukusanyaji na uchambuzi wa data umewasilishwa kimaelezo. Kwa hiyo, utafiti huu umejikita zaidi katika mkabala wa kitaamuli. Mkabala wa kitaamuli umetumika kwa sababu data za utafiti huu zinahitaji maelezo ya kina na si mabunio. Mathalani, ubainishaji na ufafanuzi wa mofu zinazounda kitenzi cha Kisambaa na namna mofu hizo zinavyoathiriana pale zinapokaa pamoja kuunda kitenzi umefanywa kwa njia ya maelezo. Ukusunyaji wa data ulifanywa kwa njia ya maelezo na ubainishaji wa makundi mbalimbali ya mofu zinazounda kitenzi cha Kisambaa na namna zinavyoathiriana umefanywa kwa njia ya majedwali.

### 3.2.1 Eneo la utafiti

Japokuwa Kisambaa kinazungumzwa katika maeneo mbalimbali katika Mkoa wa Tanga kama ilivyokwishaelezwa hapo awali, utafiti huu umefanyika katika Wilaya ya Lushoto. Mtafiti ameshughulika na Kisambaa cha Mlalo ambapo Mlalo ni mojawapo ya tarafa za Wilaya ya Lushoto ambayo ipo kaskazini mwa wilaya hii. Utafiti huu umelenga Tarafa ya Mlalo na si maeneo mengine katika Wilaya ya

Lushoto kutokana na kuwepo kwa wazungumzaji wengi wa lugha ya Kisambaa.

Kwa mujibu wa masimulizi ya watoa taarifa, Kisambaa cha Mlalo ni Kisambaa cha asili na hakija athiriwa na lugha ya Kiswahili kama kilivyo Kisambaa cha Lushoto mjini ama Korogwe ambako Wasambaa wamechanganyika na Wazigua. Mlalo ni Tarafa iliyo mbali na makao makuu ya wilaya ya Lushoto ambayo ni Lushoto mjini. Mlalo ni eneo ambalo lipo katika kimo cha mita 1450 kutoka usawa wa bahari magharibi mwa milima ya usambara. Vilevile kutokana na kuwepo kwa wazungumzaji wengi wa Kisambaa katika Tarafa ya Mlalo mtafiti ameweza kupata data za kitenzi cha Kisambaa chenye maumbo tofautitofauti yaliyomwezesha kufikia malengo ya utafiti. Hivyo basi, eneo hili liliweza kutupatia uwakilishi mzuri na data ya kutosha kuhusu kitenzi cha lugha ya Kisambaa.

### 3.2.2 Walengwa wa utafiti

Kwa kuwa utafiti huu ulihusu kitenzi cha Kisambaa, walengwa wa utafiti ni Wasambaa wote hususani kutoka maeneo ya Mlalo katika kata tatu (3) ambazo ni Mlalo, Mwangoi na Dule ‘M’ zilizopo katika Tarafa ya Mlalo, Wilaya ya Lushoto. Kata hizi zimeteuliwa kutokana na kwamba mtafiti asingeweza kukusanya data katika kata zote za Tarafa ya Mlalo. Mtafiti aliwatumia wazee ambao walisimulia mambo mbalimbali yanayohusu wasambaa ikiwemo aina ya visambaa (lahaja) vinavyozungumzwa katika Tarafa ya Mlalo. Kutokana na masimulizi hayo mtafiti alipata nafasi ya kuteua walengwa ambao walifaa katika kupata data za utafiti huu. Walengwa wanaoishi katika maeneo hayo yaliyotajwa ni wamahiri wa lugha ya Kisambaa.

Wazungumzaji hao wa Kisambaa hutumia Kisambaa katika shughuli zao nyingi za kila siku. Lugha ya kwanza wanayojifunza kutoka kwa wazazi wao ni Kisambaa na Kiswahili wanakipata wakianza kusoma shule ya msingi. Kwa mujibu wa masimulizi ya watoa taarifa, watoto wanaoanza shule za awali hujikuta wakitumia Kisambaa wakiwa shuleni. Hivyo kutoka kwa wazungumzaji hao mtafiti aliweza kukusanya data za kitenzi cha Kisambaa chenye maumbo tofauti tofauti yanayokidhi malengo ya utafiti huu.

### 3.2.3 Sampuli na usampulishaji

Field (2005) anaeleza kuwa sampuli ni kikundi cha watu kilichochaguliwa kwa niaba ya kundi kubwa ili kutoa taarifa zinazowakilisha kundi hilo. Aidha, Taherdoost (2016) anaeleza kuwa ili kujibu maswali ya utafiti ni muhimu mtafiti ateue kundi dogo la watoa taarifa ambalo litampatia taarifa. Usampulishaji unafanywa ili kuokoa muda na gharama zinazoweza kutumika katika kundi kubwa la watu. Mtafiti anatakiwa achague ni mkusanyiko upi unaofaa kufanyia utafiti wake na katika mkusanyiko huo lazima achague kundi dogo ili kupata data inayofaa kwa utafiti anaoufanya.

Katika utafiti huu, usampulishaji umefanywa katika maeneo mawili ambapo ni usampulishaji uliofanywa kwa makusudio. Kwanza ni usampulishaji wa eneo la utafiti, ambalo limeteuliwa kwa makusudio ya kupata Kisambaa cha asili tofauti na Kisambaa cha maeneo mengine ya Lushoto. Pili ni usampulishaji wa walengwa wa utafiti ambao walitegemewa kutoa vitenzi vinavyofaa kwa utafiti huu. Mbinu hii ya usampulishaji imetumika kutokana na taarifa mbalimbali alizopata mtafiti kutoka katika masimulizi ya wazee.

Ili kuelezea sarufi ya lugha fulani, mtafiti anahitaji kupata data ya kutosha na inayofaa. Vitenzi vilivyohitajika ni vitenzi vilivyoambishwa na kunyambulishwa kwa mofu zinazowakilisha dhana mbalimbali. Vitenzi hivyo vilikusanywa na kugawanywa katika makundi matatu: kundi moja ni la vitenzi vilivyoambishwa mofu za aina tofautitofauti, la pili likiwa na vitenzi vyenye mizizi iliyonyambulishwa kwa mofu nyambulishi mbalimbali na la tatu ni vitenzi vyenye mofu ambishi na mofu nyambulishi kwa pamoja.

Lengo la kugawa vitenzi hivyo ni kupata data inayofaa katika kujibu maswali ya utafiti huu. Data hiyo ilipatikana kwa kurekodi mazungumzo na mahojiano na wazungumzaji wa Kisambaa walioteuliwa pamoja na kusoma matini zenye vitenzi vya Kisambaa. Vitenzi mia tano (500) ambavyo vimeambatishwa vilipatikana kutoka kwa walengwa wote waliokusudiwa katika utafiti huu. Vitenzi hivyo pia ni vya Kisambaa cha asili cha Mlalo ambacho ni tofauti na lahaja ya Mlalo iliyotambulishwa na Besha (1985). Kisambaa hicho cha asili hakina fonimu /l/ katika maneno yake. Kwa mujibu wa taarifa zilizopatikana katika utafiti huu Kisambaa ambacho Besha (ameshatajwa) amekibainisha kama lahaja ya Mlalo ni Kisambaa cha Mlalo Misheni. Kisambaa hicho cha asili kimepatikana kutoka katika kata zilizolengwa ambazo zimesampulishwa kutokana na urahisi wake wa kufikika hivyo kumpunguzia mtafiti gharama za usafiri.

Idadi ya vitenzi hivyo ilifikiwa kutokana na mtafiti kufikia kiwango cha juu cha utoshelevu wa data aliyokusanya. Mack na wenzake (2005) na Jill na wenzake (2010) na Hennink  na wenzake (2017) wanaeleza kuwa katika ukusanyaji wa data katika utafiti wa kitaamuli sampuli inaweza kufikiwa kutokana na kufikia kiwango

cha juu cha utoshelevu wa data inayohitajika kulingana na maswali ya utafiti. Utoshelevu wa data unafikiwa ikiwa data inayopatikana haiongezi taarifa mpya zaidi ya zilizopatikana na zinazohitajika kujibu maswali ya utafiti. Vivyo hivyo, kwa watoa taarifa, watakuwa toshelevu kulingana na utoshelevu wa data. Kwa hiyo, idadi ya watoa taarifa ni kulingana na kufikia kiwango cha juu cha utoshelevu wa data ambapo hakuna taarifa nyingine mpya zinazopatikana.

Pamoja na hayo, utafiti huu umehusisha wazungumzaji wa Kisambaa ambao walipatikana kwa njia ya usampulishaji lengwa. Mtafiti alilenga kupata wazungumzaji wa Kisambaa wanawake sita (6) na wanaume sita (6) ambao waligawanywa katika makundi matatu ya wazee 4 wa umri kati ya miaka 50 - 70; watu wazima 4 wenye umri wa kati ya miaka 35 - 49 na vijana 4 wenye umri kati ya miaka 25 - 34. Umri wa watoa taarifa ulilengwa ili kupata uwakilishi wa wazungumzaji wa Kisambaa, si kwamba walio katika umri wa chini ya miaka 25 walikuwa hawahusiki bali mtafiti asingeweza kuwahusisha wazungumzaji wote wa Kisambaa.

Kwa hiyo, aliteua kundi aliloweza kulifanyia kazi lakini ambalo lilitosha kutoa taarifa zilizohitajika. Wazee walihusishwa kwa kuwa inaaminika kuwa lugha yao haijapata athari na kama zipo basi ni kwa kiasi kidogo. Katika utafiti huu wa isimu ya lugha, wakati wa kukusanya data lengo lilikuwa kupata vitenzi vingi vilivyoambikwa kwa mofu mbalimbali na si kuzingatia idadi ya watu waliohusika katika kupatikana vitenzi hivyo kama anavyoeleza O’Leary (2004) kuwa katika tafiti nyingi za kitaamuli usampulishaji haulengi idadi ya watoa taarifa, mtu mmoja anaweza kuwa chanzo cha data ya utafiti wa aina hizi. Lengo la kugawa watoa

taarifa katika makundi ni kuhusisha wazungumzaji wa lugha ya Kisambaa wa rika zote. Upatikanaji wa watoa taarifa ulikuwa wa makusudio ambapo mtafiti alilenga kupata wanawake na wanaume katika kila kundi. Katika mazungumzo na watoa taarifa hao mtafiti alikusanya vitenzi ambavyo alivichunguza na kuchambua mofu, mofimu na alomofu za mofimu hizo na kubainisha namna mofu zinavyoathiriana kimofolojia au kimofofonolojia katika kitenzi.

## 3.3 Mbinu za kukusanyia data

Hizi ni njia ambazo mtafiti alitumia kukusanyia data ya utafiti huu wa maumbo ya kitenzi cha Kisambaa. Kothari (2004) anafafanua kuwa kabla mtafiti hajakusanya data atambue kuwa kuna data ya msingi yaani data inayokusanywa kwa mara ya kwanza na data fuatizi ambayo ni mkusanyiko wa data ambayo imekusanywa na kuchambuliwa na watafiti wengine. Data fuatizi inaweza kupatikana katika vitabu, majarida, ripoti mbalimbali na magazeti. Katika utafiti huu, mtafiti ametumia data ya msingi na ile iliyokusanywa na watafiti wengine waliofanya utafiti katika Kisambaa. Data ya msingi ilikusanywa njia ya usaili ambapo mahojiano yalinukuliwa na mtafiti. Vilevile mtafiti alikusanya data fuatizi kwa kusoma tafiti zilizofanywa kuhusu Kisambaa na maandiko yaliyoandikwa kwa lugha ya Kisambaa.

### 3.3.1 Mahojiano

Hii ni njia iliyozoeleka kutumika kukusanyia data, aghalabu watu huongea na watu wengine kwa ajili ya kupata taarifa mbalimbali. Monette na wenzake (2011) wanafafanua kuwa mahojiano yanafanywa na mtafiti kwa kuwasomea watoa taarifa maswali na kurekodi majibu kutoka kwa watoa taarifa. Naye Burns (2000) anaeleza kuwa mahojiano ni mbinu ambayo mtafiti anawasiliana ana kwa ana au kwa njia ya

simu na watoa taarifa ili kupata taarifa fulani kwa lengo maalumu.

Katika utafiti huu mtafiti alifanya mahojiano ya ana kwa ana na watoa taarifa. Mbinu hii ilimwezesha mtafiti kuuliza maswali kadri ya mahitaji ya data yake. Watoa taarifa pia waliweza kuuliza maswali kama wanavyoeleza Jill na wenzake (2010) kuwa, mahojiano na watoa taarifa yanafanywa hadi kufikia kiwango cha juu ambapo hakuna taarifa nyingine mpya zinazosaidia kujibu maswali ya utafiti, zinazopatikana kutoka kwa watoa taarifa. Mahojiano hayo yalifanyika kwa lugha ya Kisambaa ambapo mtafiti aliipata lugha ya Kisambaa cha Mlalo ambacho ni cha asili na kukusanya vitenzi vilivyoambishwa na kunyambulishwa kwa mofu mbalimbali ambavyo ndivyo vilivyohitajika katika utafiti huu.

Walengwa wa makundi yote matatu yaliyoteuliwa walihusishwa katika mbinu hii. Katika mahojiano hayo mtafiti alikuwa na maswali ya mwongozo ambayo yalikuwa ni vitenzi vinavyoeleza dhana mbalimbali kwa Kiswahili vikiwemo vya ukanushi, masharti, vitenzi katika njeo mbalimbali, vyenye urejeshi, vitenzi katika hali ya utendeka, utendwa, utendea, kutendana nakadhalika. Mtafiti aliwahoji watoa taarifa vitenzi hivyo vinavyotamkwa kwa lugha ya Kisambaa. Mtafiti alihoji pia kupata vitenzi vingine vyenye maumbo kama hayo vinavyoeleza matendo mbalimbali katika Kisambaa.

Aidha, watoa taarifa walikuwa huru kueleza vitenzi vingine vinavyoeleza matendo mbalimbali katika Kisambaa. Hivyo, mtafiti aliyasikiliza mazungumzo ambayo yalikuwa pia na sentensi zenye vitenzi mbalimbali vya Kisambaa. Wakati usaili unaendelea aliihifadhi data yake kwa kunukuu vitenzi alivyovipata kutoka kwa

watoa taarifa hao katika shajala yake. Baada ya kunukuu, mtafiti alivibainisha vitenzi vya Kisambaa alivyovipata kutoka kwa watoa taarifa na kuviweka katika makundi ya vitenzi vilivyoambishwa na kunyambulishwa. Maumbo hayo tofautitofauti ya vitenzi yalichunguzwa na kubaini namna mofu zinavyoathiriana kwa kuongozwa na nadharia ya Umbo Upeo.

### 3.3.2 Upitiaji wa nyaraka

Data fuatizi ambayo imekusanywa na watafiti wengine inapatikana katika maandiko mbalimbali. Maandiko hayo yanaweza kuwa yamechapishwa ama hayajachapishwa. Kothari (2004) anashauri kuwa mtafiti awe makini na data ya aina hii kwani inaweza isiwe faafu katika utafiti wake. Mtafiti asichukue data bila kujua imekusanywa na nani, wakati gani, ni kipi chanzo cha data hiyo, je ilikusanywa kwa kutumia mbinu zinazokubalika na usahihi wa data hiyo. Besha (1993) amekusanya maneno mbalimbali ya Kisambaa vikiwemo vitenzi. Hivyo, mtafiti amekusanya vitenzi vya lugha ya Kisambaa ambavyo vimeorodheshwa katika kazi hiyo.

Vitenzi vilivyokusanywa vimetoa mwongozo kwa utafiti huu wa maumbo ya kitenzi cha Kisambaa. Vilevile data fuatizi ilimsaidai mtafiti kupata Kisambaa kilichokusanywa na kutumiwa na watafiti wengine. Pamoja na hayo mtafiti ameweza kutofautisha Kisambaa alichokiona kwenye maandishi na kile ambacho alikipata kwa watoa taarifa wake.

## 3.4 Uchanganuzi wa data

Katika uwasilishaji na uchambuzi wa data ya utafiti huu mkabala wa kitaamuli umetumika kwa sababu huu ni utafiti wa kiisimu ambao data zake zimehitaji maelezo ya kina. Kwa mujibu wa Enon (1998), mkabala wa kitaamuli ni njia ya

ukusanyaji wa data inayolenga kukusanya data kwa njia ya maelezo. Kwa hiyo, ubainishaji na ufafanuzi wa mofu na namna mofu hizo zinavyoathiriana katika umbo la kitenzi umefanywa kwa ufafanuzi wa kina. Uchanganuzi wa data ya utafiti huu ulifanyika kwa kugawa vitenzi katika makundi matatu. Makundi hayo ni pamoja na kundi la vitenzi vyenye mofu ambishi, kundi la vitenzi vyenye mofu nyambulishi na kundi la vitenzi vyenye mofu ambishi na nyambulishi kwa pamoja.

Makundi hayo ya vitenzi ndio yametoa maudhui hali ya kuwa maudhui hayo yameleta matokeo ya utafiti huu. Majedwali yametumika katika kubainisha na kufafanua mofu mbalimbali ambishi na nyambulishi zinazounda kitenzi cha Kisambaa. Vilevile mofu zinazoathiriana zinapokaa pamoja kuunda kitenzi zimefafanuliwa kwa njia ya majedwali. Uwasilishwaji wa data umefanywa kwa kuongozwa na malengo na maswali ya utafiti huu. Aidha, uchambuzi, uchunguzi na uwasilishwaji wa data ya utafiti huu umefanywa kwa kuongozwa na nadharia ya Umbo Upeo. Mofu za aina zote zinazounda vitenzi vya Kisambaa na namna zinavyoathiriana zimechambuliwa na kuchunguzwa kwa kuzingatia mashartizuizi yanayotawala mofu katika kitenzi cha lugha hii.

### 3.5 Maadili ya utafiti

Katika lugha, maadili ni mwenendo unaokubalika katika ufanyaji wa jambo. Katika utafiti, maadili ni uwajibikaji kitabia kuhusu haki za wale wote unaokutana nao katika utafiti katika kuzingatia madhumuni na malengo ya utafiti na namna ya kuyatumia matokeo ya utafiti kwa uadilifu ili yaweze kuwa na faida kwa jamii. Mukuthuria (2010) anaeleza kuwa lengo la kuzingatia maadili ya utafiti ni

kuhakikisha kuwa shughuli ya utafiti au michakato yote na hatua zote hazitakuwa na madhara wala hali ya udhalilishaji kwa watu wote walioshirikishwa katika utafiti.

Masuala ya maadili katika utafiti huu, pia yalizingatiwa kama ambavyo mtafiti alipaswa kuyazingatia. Kwa kuwa utafiti huu ulihusisha watu binafsi wa kutoka maeneo yaliyotafitiwa, kabla mtafiti hajaanza kukusanya data aliomba barua kutoka Chuo Kikuu cha Huria cha Tanzania kilichomtambulisha mtafiti katika maeneo aliyofika. Mtafiti alipofika katika eneo la utafiti alijitambulisha kwa viongozi wa kata na vijiji kwa kuonesha kibali ambapo viongozi nao walimtambulisha kwa watoa taarifa. Aidha, kabla ya kuanza kazi, mtafiti aliomba ridhaa ya kushiriki kwa kila mtoa taarifa ambapo kwa wale waliokataa kushiriki mtafiti aliwaacha. Hii ni kwa sababu Fouka na Mantzorou (2011) anaeleza kuwa ni bora zaidi watoa taarifa za utafiti kushiriki kwa ridhaa yao badala ya kulazimishwa. Kwa mintarafu ya kulinda maadili ya utafiti, watoa taarifa walioshiriki katika utafiti huu ni wale walioridhia kwa hiari yao kushiriki katika mahojiano yaliyofanywa na mtafiti.

Kwa sababu katika tafiti za kiisimu mtafiti lazima aulize maswali mengi ili kupata data ya kutosha ya lugha inayochunguzwa, wakati mwingine maswali yanaweza kuwa kero kwa watoa taarifa wengine na kujiona kama wanapotezewa muda. Hivyo basi, mtafiti analazimika kujenga ushirikiano wa karibu na watoa taarifa wake. Kwa hiyo, mtafiti alizingatia maadili ya jamii hususan tabia njema ili kujenga ushirikiano wa karibu kutoka kwa watoa taarifa. Vilevile, mtafiti alizingatia suala la usiri na faragha kwa watoa taarifa, ambapo aliwaahidi na kuwahakikishia watoa taarifa kuwa data watakazozitoa zitatumika kwa malengo ya utafiti huu tu. Kwa kulinda ahadi hii ya usiri baina ya mtafiti na watoa taarifa wake, katika matokeo yote ya utafiti huu

hakuna urejeleaji wa jina la mtoa taarifa uliofanywa katika uwasilishaji na uchambuzi wa data.

Kwa ujumla, masuala ya maadili ya utafiti yalizingatiwa katika utafiti huu. Hivyo, uzingativu wa maadili ya utafiti ulisaidia mchakato wa ukusanyaji wa data kufanyika bila vikwazo vikubwa. Mtafiti aliweza kufika maeneo yote ya utafiti kwa kujiamini kwani alikuwa na kibali kilichomruhusu kufanya utafiti katika maeneo aliyoyateua kufanya utafiti.

### 3.6 Uthabiti na ukubalifu wa utafiti

Uthabiti na ukubalifu ni dhana za msingi zinazotumiwa katika uchambuzi wa data za utafiti. Uthabiti na ukubalifu hutofautisha kati ya utafiti uliofikia kiwango na usio fikia kiwango kutokana na matokeo ya utafiti. Kothari (2009) anaeleza kuwa uthabiti wa utafiti unahusu usahihi na ukweli wa matokeo ya utafiti kisayansi. Utafiti thabiti lazima uoneshe uhalisia uliopo katika mazingira kwa kupima kitu halisi kinachostahiki kupimwa. Katika utafiti huu, mbinu za ukusanyaji wa data kama vile usomaji wa kazi tangulizi na mahojiano zimehakikishwa usahihi wake. Mbinu hizo zilihakikishwa ili kuona uthabiti na uhalisi wa data ambapo mbinu zaidi ya moja ilitumika kwa ajili ya kukamilisha mbinu nyingine pale ambapo data iliyokusudiwa haikujitosheleza.

Katika kuthibitisha hilo, matokeo yaliyopatikana kutokana na mbinu zilizotumika hayakupishana sana baina ya mbinu moja na nyingine. Kwa mfano, matokeo ya mbinu Kwa muhtasari, mbinu za utafiti na sampuli zilithibitisha uthabiti na hali

halisi ya kile kilichopo katika mazingira halisi ya utafiti. Kwa ufupi, tunaweza kusema kuwa mbinu zilizotumika na sampuli iliyoteuliwa vimechangia kupata matokeo thabiti na yenye kukubalika. Hii ni kwa sababu matokeo yanakaribia kufanana na sampuli haikubadilika kiasi kwamba tumeweza kutoa hitimisho kwa mujibu wa matokeo ya data hizo.

### 3.7 Muhtasari wa sura

Katika sura hii tumebainisha mbinu za utafiti zilizotumika kufikia malengo ya utafiti huu. Mbinu zilizotumika kukusanyia data ya utafiti huu zimeainishwa na kufafanuliwa, watoa taarifa walivyopatikana, eneo lililofanyiwa utafiti katika Tarafa ya Mlalo. Vilevile, sura hii imebainisha namna uchanganuzi wa data ulivyofanyika wakati wa uwasilishaji wa data za utafiti huu na namna mtafiti alivyozingatia maadili ya utafiti pamoja na uthibiti na ukubalifu wa data.

# SURA YA NNE

# UCHAMBUZI, UWASILISHAJI WA DATA NA MJADALA WA MATOKEO

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inahusu uchambuzi, uwasilishaji wa data na mjadala wa matokeo ya utafiti. Data ya utafiti huu imekusanywa kutoka kwa watoa taarifa kwa njia ya mahojiano. Data hiyo inahusu vitenzi vya Kisambaa vyenye mofu ambishi na nyambulishi. Mofu ambishi na nyambulishi zinazounda vitenzi hivyo zimechambuliwa na kubainishwa. Vilevile, mofu hizo zimechunguzwa kwa mwongozo wa nadharia ya Umbo Upeo kwa namna mofu moja inavyoathiri mofu nyingine katika umbo la kitenzi kinachohusika. Katika uchambuzi na uchunguzi huo ndipo mashartizuizi yanyoongoza uambikwaji wa mofu katika lugha ya Kisambaa yamebainishwa.

Mbali na utangulizi, sura hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza inabainisha mofu mbalimbali zinazounda kitenzi cha Kisambaa pamoja na mofimu zake. Sehemu ya pili ni ufafanuzi wa namna mofu hizo zinavyoathiriana yaani mofu ambishi na mofu nyambulishi, pale zinapokaa pamoja kuunda kitenzi cha Kisambaa. Katika sehemu hii, mofu zinafafanuliwa namna zinavyoathiriana kimofolojia au kimofofonolojia kwa kubainisha mashartizuizi yanayotawala mfuatano wa mofu wakati wa uambikaji wa mofu hizo. Katika sehemu ya tatu ni muhtasari wa sura.

## 4.2 Mofu na mofimu katika kitenzi cha Kisambaa

Sehemu hii inajikita katika kujibu swali la kwanza la utafiti ambalo limechagizwa na lengo la kwanza la utafiti ambalo lilikuwa linataka kubainisha mofu ambishi na nyambulishi pamoja na mofimu zake zinazounda kitenzi cha lugha ya Kisambaa. Kama lugha nyingine za Kibantu, kitenzi cha lugha ya Kisambaa ni aina ya maneno

ambayo ina sifa kuu inayotofautisha aina hii na aina nyingine za maneno katika Kisambaa. Sifa hiyo inahusu kitenzi kuwa na uwezo wa kubeba taarifa mbalimbali (Bearth, 2003). Katika muktadha huo, maumbo yanayobeba taarifa hizo ambayo ndiyo vijenzi vya vitenzi hujulikana kama mofu na taarifa zinazobebwa na mofu hizo huitwa mofimu. Mofu hizo huambishwa au kunyambulishwa katika mzizi wa kitenzi ili kuunda vitenzi vyenye maumbo mbalimbali. Katika utafiti huu, mofu zinazoambikwa katika mzizi wa kitenzi cha Kisambaa tumeziita “mofu ambishi” na “mofu nyambulishi”. Mofu hizi kwa mujibu wa lugha ya Kisambaa zinabainishwa kama ifuatavyo:

### 4.2.1 Mofu ambishi katika kitenzi cha Kisambaa

Data za utafiti huu, zinabainisha kuwa kitenzi cha Kisambaa hubeba mofu ambishi ambazo kidhima kila mofu inawakilisha mofimu kulingana na mazingira inamotokea. Mofu ambishi ni mofu ambazo zinaambikwa kabla ya mzizi wa neno ambazo zinatokana na kitendo cha kuambisha mofu katika mzizi wa kitenzi (Gawasike, 2012).  Tafiti tangulizi pia zinabainisha kuwa, katika lugha nyingi za Kibantu kama vile Kilangi (Dunham, 2002), Kishona (Mkanganwi, 2002), Kihehe (Okoa, 2012) na Runyakitara (Katushemererwe, 2012) vitenzi vyake vinapokea mofu ambishi ambazo ni mofu za mofimu ya nafsi, ukanushi, njeo, mtendwa na nyinginezo. Pamoja na hayo, katika kubainisha mfuatano wa mofu katika vitenzi vya lugha za Kibantu, Nurse (2008) amependekeza ruwaza ya mfuatano wa mofu ambayo lugha nyingi za Kibantu hufuata ruwaza hiyo. Mfuatano huo unabainishwa katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 4.1: Mfuatano wa Mofu katika Lugha za Kibantu**

| **Idadi** | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mofimu** | Tangulizi (Ukanushi) | Nafsi | Ukanushi$_2$ | Njeo/Hali | Yambwa | Mzizi na vinyambulishi | Tamati | Irabu ishilizi |

**Chanzo**: Nurse (2008:231) Tafsiri ya Mtafiti.

Kwa hiyo, kutokana na mfuatano huo wa mofu katika lugha za Kibantu, lugha ya Kisambaa ina mfuatano ufuatao wa mofu ambazo zinaambikwa kabla ya mzizi:

**Jedwali 4.2: Mofu Ambishi katika Kisambaa**

| **MOFIMU** | **Ukanushi$_1$** | **Nafsi** | **Ukanushi$_2$** | **Njeo** | **Yambwa** | **Masharti** | **Ujirejezi** | **MZIZI** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **MOFU AMBISHI** | {ka-}<br>{ku-}<br>{ke-}<br>{si-}<br>{se-} | {ni-}<br>{u-}<br>{wa-}<br>{a-}<br>{ti-}<br>{mwa-}<br>{mu-}<br>{m-}<br>{wa-} | {-she-} | {-a-}<br>{-ta-}<br>{-i-}<br>{-za-}<br>{-Ø-}<br>{-a-}<br>{ne-}<br>{nee-} | {-ni-}<br>{-ku-}<br>{-ti-}<br>{-mi-}<br>{-m-}<br>{-mu-}<br>{-wa-}<br>{-ha-}<br>{-chi-}<br>{-vi-}<br>{-u-}<br>{-ya-} | {-ki-} | {-ki-} | |

**Chanzo:** Data za Uwandani na Besha (1993)

Aidha, Kaoneka (2009: 49-50) amebainisha pia mfuatano wa mofu katika vitenzi vya Kisambaa kama ifuatavyo.

| **Idadi** | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mofimu** | Knsh$_1$ | Nafsi | Nj/Hali | Knsh$_2$ | Isoukomo | Ymbw | Mz | Nymb | I |

**Chanzo**: Kaoneka (2009:49) Tafsiri ya mtafiti

Hata hivyo, katika mfuatano huo wa Kaoneka (ameshatajwa) haujajumuisha mofu ya masharti na mofu ya ujirejezi ambazo zimebainishwa katika data ya utafiti huu. Pamoja na hayo, mofu ambishi zilizobainishwa katika jedwali 4.2 ambazo ni mofu zinazopatikana kabla ya mzizi wa kitenzi katika muundo wa vitenzi vya Kisambaa, hazitokei kwa wakati mmoja katika umbo moja la kitenzi. Upo mfuatano mahususi katika lugha ya Kisambaa kutokana na mashartizuizi ya lugha hii. Data

zinadhihirisha kuwa katika mfuatano huo ndipo mofu hizo zinapoathiriana. Vilevile, kutoka katika data zilizobainishwa katika jedwali 4.2, mofu ya ukanushi nafasi ya kwanza ambayo inaonekana mwanzoni mwa jedwali huzitangulia mofu nyingine katika muundo wa kitenzi cha Kisambaa. Maumbo ya vitenzi vyenye mofu hiyo yanabainishwa katika MF. 19 ufuataO.

**MF. 19**

i. Kemuavye (hamtatoa) - ke- mu- avy- e

Knsh- Nfs- Mz- $M_i$

ii. Kaaize (hatakuja) - ka- a- iz- e

Knsh- Nfs- Mz- $M_i$

iii. Kuawa (hutoki) - ku-aw-a

Knsh- Mz- $M_i$

iv. Sija (sili) – si-j-a

Knsh- Mz- $M_i$

v. Senije (sitakula) – se- ni – j –e

Knsh- Nfs- Mz- $M_i$

Katika mfano wa 13 (i-v) hapo juu tunabaini kuwa, mofu ya ukanushi nafasi ya kwanza hufuatiwa na mofu ya nafsi. Mofu ambishi nyingine katika mfuatano huo kwa mujibu wa data ni mofu ya mofimu ya ukanushi nafasi ya pili. Mofu hii inatanguliwa na mofu ya nafsi katika umbo la kitenzi cha Kisambaa. Pamoja na hayo mofu ya mofimu ya ukanushi nafasi ya kwanza, mofu ya mofimu ya nafsi na mofu

ya mofimu ya ukanushi nafasi ya pili hazifuatani katika umbo moja la kitenzi cha Kisambaa. Mofu hiyo inabainishwa katika vitenzi vifuatavyo.

**MF. 20.**

i. Nishezaiza (nisije) – ni-she-za-iz-a

Nfs-Knsh-Nj-Mz- $M_i$

ii. Ushezawaeta (usiwalete) – u- she –za- wa-et-a

Nfs-Knsh-Nj-Ymbw- Mz- $M_i$

iii. Mshezatijata (msitukanyage) – m-she-za-ti-jat-a

Nfs-Knsh-Nj- Ymbw-Mz- $M_i$

iv. Tishighuluiyewo (tusionunua) – ti-shi-ngul-iye-wo

Nfs-Knsh-Mz-Nj-Rjsh

v. Mshizutiyewo (msiovuta) – m-shi- zut-iye-wo

Nfs-Knsh-Mz-Nj-Rjsh

Katika mfano wa 20 (i-v) hapo juu tunabaini kuwa, mofu ya mofimu ya ukanushi nafasi ya pili, mofu ya mofimu ya nafsi, mofu ya mofimu ya njeo, mofu ya yambwa na mofu ya urejeshi ndizo zinazoweza kuambishwa pamoja katika umbo moja la kitenzi cha Kisambaa.

Mfuatano mwingine wa mofu ambishi katika muundo wa kitenzi cha Kisambaa uliopatikana katika data za utafiti huu ni mofu ya mofimu ya nafsi, mofu ya mofimu ya masharti, mofu ya mofimu ya ukanushi na mofu ya mofimu ya ujirejezi kufuatana

pamoja kama viambishi awali vinavyounda vitenzi vya Kisambaa. Tazama MF.21 ufuatao.

**MF. 21**

i. akishekieta (asipojileta) - a-ki-she-ki-et-a

Nfs-Shrt-Knsh-Rjz-Mz- $M_i$

ii. akishekighulia (asipojinunulia)- a-ki-she-ki-ghul-i-a

Nfs-Shrt-Knsh-Rjz-Mz-Tdea- $M_i$

iii. mukishekishaghua (msipojichagua) – m-ki-she-ki-shaghu-a

Nfs-Shrt-Knsh-Rjz-Mz- $M_i$

Katika mfano wa 15 (i-iii) hapo juu, tunaona namna mofu ya ukanushi inavyoweza kuambatana na mofu nyingine ili kuunda vitenzi katika Kisambaa. Vilevile katika lugha ya Kisambaa, kitenzi kinaweza kuundwa kwa mfuatano wa mofu ya nafsi, njeo na mofu ya yambwa. Vitenzi vyenye tabia hiyo vinafafanuliwa katika mfano ufutao.

**MF. 22**

i. wazamhaka (walimuogesha) - wa-za-m-hak-a

Nfs-Nj-Ymbw-Mz- $M_i$

ii. utawaeta (unawaleta) – u-ta-wa-et-a

Nfs-Nj-Ymbw-Mz- $M_i$

iii. naachimzwika (ninakimvalisha) – na-a-chi-m-zwik-a

Nfs-Nj-$Ymbw_1$-$Ymbw_2$-Mz- $M_i$

Hivyo, data katika mfano wa 16 (i-iii) hapo juu zinabainisha namna mofu zinavyoweza kuandamana kuunda vitenzi katika Kisambaa. Vilevile, katika

mfuatano huo, tunaona kuwa mofu yambwa mbili zinaweza kuambishwa katika kitenzi kimoja, mfuatano huu pia umebainishwa na Riedel (2009). Hivyo basi, katika mfuatano na mpangilio huo wa mofu zinapoambishwa katika mzizi wa kitenzi ili kuunda vitenzi vya Kisambaa, mofu hizo huweza kuathiriana. Kutokana na kuathiriana huko baadhi ya mofu maumbo yake huweza kubadilika au nafasi ya utokeaji wa mofu kubadilika.

### 4.2.2 Mofu nyambulishi katika kitenzi cha Kisambaa

Data za utafiti huu zimebainisha kuwa lugha ya Kisambaa ina tabia ya uundaji wa vitenzi vipya vyenye maana panuzi kwa njia ya unyambulishaji wa mofu. Unyambulishaji wa mofu katika vitenzi unaelezwa kuwa ni mchakato wa uundaji wa maneno ambapo vitenzi vipya huundwa vyenye maana panuzi (Ngonyani, 2003; Massamba, 2004). Besha (1993) amebainisha mofu za unyambulishi za utendea {-i-} na {-e-}, mofu za usababishi (utendeshi) {-ez-} na {-iz-}, mofu za ufanyikaji sana {-ish-}, {-esh-}, {-iz-} na {-ez-}, mofu ya utendana {-an-}, mofu za utendeka {-ik-} na {-ek-}, mofu za utendwa {-ighw-} na {-w-} pamoja na mofu ya ubadilifu {-u-} katika kitenzi cha Kisambaa. Aidha, Kaoneka (2009:57-75) amebainisha mofu nyambulishi katika lugha ya Kisambaa ambazo zinaonekana katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 4.3: Mofu Nyambulishi katika Kitenzi cha Kisambaa**

| | Utendea | Utendwa | Utendeka | Utendeshi | Ufanyikaji sana | Utendana |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **MZIZI** | {-i-}<br>{-e-} | {-w-}<br>{-ighw-} | {-ek-}<br>{-ik-} | {-esh-}<br>{-ish-}<br>{-sh-}<br>{-s-} | {-ish-}<br>{-esh-}<br>{-ez-}<br>{-iz-} | {-an-} |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | {-z-}<br>{-y-} | | |

**Chanzo:** Kaoneka (2009:57-75)

Mofu zilizobainishwa katika jedwali Na. 4.3 hapo juu zimetokana na data alizozipata Kaoneka (ameshatajwa). Hata hivyo, kutokana na data za utafiti huu kuna baadhi ya mofu nyambulishi ambazo watafiti waliotangulia hawajazishighulikia. Kwa hiyo, jedwali lifuatalo linabainisha mofu nyambulishi mbalimbali ambazo zimepatikana kutoka katika data za utafiti huu.

**Jedwali 4.4: Mofu Nyambulishi katika Kitenzi cha Kisambaa**

| | Utendea | Utendwa | Utendeka | Utendeshi | Ufanyajisana | Utendana | Ubadilifu | Urejeshi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **MZIZI** | {-e-}<br>{-i-}<br>{-eez-}<br>{-iiz-} | {-w-}<br>{-lw-}<br>{-ighw-} | {-ek-}<br>{-ik-}<br>{-k-} | {-esh-}<br>{-ish-}<br>{-ez-}<br>{-iz-}<br>{-z-}<br>{-s-}<br>{-y-} | {-ish-}<br>{-esh-}<br>{-iz-}<br>{-ez-} | {-an-} | {-u-}<br>{-o-} | {-ye-}<br>{-wo-} |

**Chanzo:** Data za Uwandani

Data za utafiti huu zinaonesha mofu nyambulishi za urejeshi {-ye-} na {-wo-} kama katika vitenzi **ajieye** na **waiziewo** ambazo hazijashughulikiwa na watafiti waliotangulia. Vilevile kuna baadhi ya alomofu ambazo watafiti waliotangulia hawakuzibainisha ambazo ni pamoja na mofu za utendea {-eez-} na {iiz-} kama katika vitenzi **tozeeza** 'shikia', **hozeeza** 'pozea' na **fishiiza** 'fichia' **, gwishiiza** 'angushia'**, fingiiza** 'zibia'**, ishiiza** 'lishia'. Mofu za utendwa {-lw-} kama katika

kitenzi **inulwa** ‘inuliwa’, **hitulwa** ‘geuzwa’. Pamoja na hayo, mofu ya {-ez-} na {-iz-} ni maumbo ya kitenzi cha Kisambaa ambayo huonesha utendeshi au ufanyikaji sana wa tendo linalohusika. Katika utendeshi, mofu hizi zinaunda vitenzi kama {-ez-} katika **kemeza** ‘liza’, **koeza** ‘koza’, **memeza** ‘jaza’ na {-iz-} katika **jatiza** ‘tembeza’, **viniza** ‘chezesha’, **imiza** ‘limisha’. Katika ufanyaji sana, mofu {-ez-} inaunda vitenzi kama **shongoeza** ‘ chonga sana’, **okoeza** ‘opoa sana’, **ghoshoeza** ‘tengeneza sana’ na mofu {-iz-} inaunda vitenzi kama **ghubikiza** ‘funika sana’, **haghiiza** ‘fagia sana’, **ghambiiza** ‘eleza sana’. Mofu hizi pia zinaambikwa baada ya mzizi wa kitenzi na zinaunda vitenzi vya Kisambaa vyenye fahiwa mpya tofauti na ya kitenzi cha awali. Mofu nyambulishi zilizobainishwa katika jedwali Na. 4.5 zinaunda kitenzi cha Kisambaa kama ifuatavyo.

Katika jedwali namba 4.5, mofu nyambulishi katika Kisambaa zinaonekana namna zinavyounda vitenzi mbalimbali vya Kisambaa kama wanavyoeleza Kihore na wenzake (2003) kuwa viambishi nyambulishi vinapachikwa katika vitenzi ili kuunda vitenzi vipya. Mfano, katika kitenzi cha Kisambaa **fisha** (ficha), kikinyambulishwa kwa mofu ya utendea {-i-} kinapatikana kitenzi **fishia** (fichia) ambacho kina maana ya kumfichia mtu kitu au jambo fulani. Kitenzi hiki pia kikinyambulishwa kwa mofu ya kutendeka {-ik-} kinapatikana kitenzi **fishika** (fichika) chenye maana ya uwezekano wa kitu au jambo fulani kufichwa. Hivyo mofu nyambulishi katika kitenzi cha Kisambaa zina dhima ya kuunda vitenzi vipya mbalimbali na hivyo kufanikisha mawasiliano kwa wazungumzaji wa Kisambaa.

**Jedwali 4.5: Mofu Nyambulishi Zinavyounda Kitenzi cha Kisambaa**

| **Kitenzi** | **Tendea** | **Tendwa** | **Tendeka** | **Tendana** | **Ufanyaji sana** | **Ubadilifu** | **Urejeshi** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| haka ‘oga’ | hak**i**a ‘ogea’ | hak**w**a ‘ogeshwa’ | hak**ik**a ‘ogeka’ | hak**an**a ‘ogeshana’ | hak**ish**a ‘ogasana’ | | ahakiye**ye** ‘aliyeoga’ |
| ghula ‘nunua’ | ghul**i**a ‘nunulia’ | ghul**w**a ‘nunuliwa’ | ghul**ik**a ‘nunulika’ | ghuli**an**a ‘nunuliana’ | ghul**ish**a ‘nunua sana’ | | waghuliye**wo** ‘walionunua’ |
| usha (*ondoa*) | ush**i**a (*ondolea*) | ush**w**a (*ondoshwa*) | ush**ik**a (*ondoka*) | ushi**an**a (*ondoleana*) | | | |
| ghooka (*simama*) | ghook**e**a (*simamia*) | ghook**ew**a (*simamiwa*) | ghook**ek**a (*simamishika*) | ghoosh**an**a (*simamishana*) | ghook**esh**a ‘simama sana’ | | |
| shenga (*kata*) | sheng**e**a (*katia*) | sheng**w**a (*katwa*) | sheng**ek**a (*katika*) | sheng**an**a (*katana*) | sheng**esh**a ‘kata sana | | tishengiye**wo** ‘tuliokata’ |
| fisha (*ficha*) | fish**i**a (*fichia*) | fish**w**a (*fichwa*) | fish**ik**a (*fichika*) | fish**an**a (*fichana*) | fish**ish**a ‘ficha sana’ | | wafishiye**wo** ‘walioficha’ |
| haghia (*fagia*) | haghi**i**a (*fagilia*) | haghi**w**a (*fagiwa*) | haghi**ik**a (*fagilika*) | haghi**an**a (*fagiana*) | haghiiza | | |

**Chanzo:** Data za Uwandani

Matokeo ya utafiti huu pia yanathibitisha kuwa, mofu nyambulishi ni mofu zinazotokea mbele au baada ya mzizi wa kitenzi. Tabia ya vitenzi vya lugha za Kibantu kubeba mofu nyambulishi ambayo imebainishwa katika matokeo ya utafiti huu uliochunguza mofu za kitenzi cha lugha ya Kisambaa, inajitokeza pia katika tafiti nyingine za lugha mbalimbali za Kibantu kama vile Kiswahili (Kihore na wenzake,

2003; Chomi, 2013), Chasu (Mreta, 1998)**,** Kinyamwezi (Lodhi, 2002), Kikuria (Charwi, 2011) na Kikinga (Gawasike, 2011). Mofu hizo zinawakilisha mofimu ya kutenda, kutendeka, kutendwa, kutendana, urejeshi na kadhalika. Mofimu hizi wanaisimu wengine kama Mgullu (1999) na Salesio na wenzake (2016) wameziita kauli za vitenzi. Hata hivyo, katika utafiti huu mofu hizi zimebainishwa kama mofu nyambulishi ambazo huunda vitenzi vipya kwa kupanua maana za vitenzi vya Kisambaa ama kubadili kategoria ya neno.

### 4.3 Kuathiriana kwa mofu katika kitenzi cha Kisambaa

Sehemu hii inajikita katika kujibu swali la pili la utafiti huu ambalo limechagizwa na lengo mahususi la pili. Lengo mahususi hilo lilitaka kuchanganua namna mofu zinavyoathiriana zinapokaa pamoja wakati wa kuunda kitenzi katika lugha ya Kisambaa. Data za utafiti huu zinabainisha kuwa mofu ambishi na mofu nyambulishi zinapoambikwa katika mizizi wa kitenzi cha Kisambaa huunda vitenzi mbalimbali. Hali hiyo pia imeelezwa na Kihore na wenzake (2003) na Gawasike (2012) kuwa uambikaji ni mchakato mmojawapo wa kuunda maneno katika lugha.

Katika mchakato wa uambikaji wa mofu kwenye mzizi wa kitenzi, mofu zinazounda kitenzi zinaathiriana. Tafiti za awali zinaonesha kuwa mofu zinaweza kuathiriana kimofolojia, kifonolojia, kisintaksia na hata kisemantikia. Mathalani katika lugha ya Shimalila, Mwashota (2016) amebainisha namna mofu ya njeo inavyoathiriwa kifonolojia na mofu nyingine ambazo zinaambishwa pamoja nayo katika kitenzi. Vilevile, katika lugha ya Runyambo, Rugemarila (1993) ameonesha athari za kimofofonolojia za mofu ya njeo ya wakati uliopita timilifu {**-a-**} na {**-ir-**}. Mofu

hizi zinapoambikwa katika kitenzi huathiri mofu ishilizi ambayo hubadilika kwa {**-e**} badala ya {**-a**}.

Hivyo, data za utafiti huu zinabainisha kuwa, katika lugha ya Kisambaa mofu zinapoambikwa katika mzizi wa kitenzi ili kuunda vitenzi mbalimbali zinaathiriana. Mofu hizo zinaathiriana kimofolojia au kimofofonolojia. Kutokana na athari hizo za kimofolojia au kimofofonolojia, mofu hupokea mabadiliko mbalimbali ya kiumbo, yaani umbo la mofu kubadilika, kudondoshwa kwa mofu katika umbo la kitenzi kinachobeba mofu hizo, kubadilishwa nafasi ya utokeaji au mofu kutofuatana na mofu nyingine katika umbo la kitenzi kinachohusika. Kuathiriana huko kwa mofu wakati zinapoambikwa ili kuunda kitenzi cha Kisambaa kunabainishwa katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 4.6: Kuathiriana kwa Mofu katika Kitenzi cha Kisambaa**

| **Kitenzi** | **Kitenzi kilichoambikwa** | **Mofu iliyoathiriwa** |
|---|---|---|
| u-za-ng'und-a<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$<br>(*umelima*) | ku-ng'und-iye<br>Knsh-Mz- $M_i$<br>(*hukulima*) | Mofu Nafsi na Njeo |
| ja (*kula*) | ne-ti-j-e<br>Nj-Nfs-Mz- $M_i$<br>(*tutakula*) | Mofu ishilizi |
| do-**ighw**-a (guswa) | do-**e**-**w**-a (gusiwa)<br>Mz-Tdea-Tdw- $M_i$ | Mofu ya utendwa |
| hono-**lw**-a (futwa) | hono-**e**-**w**-a (futiwa)<br>Mz-Tdea-Tdw- $M_i$ | Mofu ya utendwa |

**Chanzo:** Data za Uwandani

Data katika jedwali Na. 4.6 hapo juu zinaeleza kuwa mofu ya mofimu ya nafsi na mofu ya mofimu ya njeo zinaathiriwa kimofolojia na mofu ya mofimu ya ukanushi

katika kitenzi **kungundiye** (*hukulima*), mofu hizo zinadondoshwa. Vilevile katika vitenzi vilivyonyambulishwa kwa mofu nyambulishi za utendwa {-ighw-} na {-lw-} katika vitenzi **doighwa** (*guswa*) na **honolwa** (*futwa*), mofu hizo zinaathiriwa kimofolojia na mofu ya mofimu ya utendea {-**e**-} inaponyambulishwa pamoja na mofu hizo katika umbo la kitenzi. Mofu hizo za mofimu ya utendwa zinabadilika kiumbo na kuchukua umbo {-w-} pekee. Hivyo data zinathibitisha kuwa kuathiriana kwa mofu kunatokea katika mofu ambishi na mofu nyambulishi.

Kuathiriana kimofolojia au kimofofonolojia kwa mofu ambishi na nyambulishi zinazounda vitenzi vya Kisambaa kumefafanuliwa kwa kudhihirisha mashartizuizi (MASHA-ZU) yanayotakiwa kufuatwa katika lugha hii wakati wa uambishaji na unyambulishaji wa mofu mbalimbali. Katika nadharia ya Umbo Upeo mhimili wa usambamba unaweza kueleza mwingiliano wa viwango vya sarufi kwa kutumia kigezo cha nguvu ya shartizuizi la kiwango fulani katika kukidhi vigezo vya ukubalifu wa umbo linaposhindanishwa na shartizuizi la kiwango kingine katika hatua moja ya mpangilio wa MASHA-ZU hayo (McCarthy na Cohn, 1998). Hivyo, maumbo ya mofu ambayo yameathiriwa na mofu nyingine kutokana na michakato ya kimofofonolojia yametathminiwa katika hatua moja ya mpangilio wa mashartizuizi katika uambishaji na unyambulishaji wa mofu katika vitenzi vya Kisambaa.

Udhihirishaji wa mashartizuizi yanayoongoza uambikaji wa mofu katika kitenzi cha Kisambaa, unajibu swali la tatu la utafiti huu lililochagizwa na lengo mahususi la tatu. Lengo mahususi hilo lilitaka kudhihirisha mashartizuizi yanayotawala uambikaji wa mofu katika kitenzi cha Kisambaa. MASHA-ZU hayo ni mashartizuizi

ya uadilifu na utangamano kutokana na kwamba nadharia ya Umbo Upeo inaruhusu uzalishaji wa maumbotokeo usio na kikomo. Hivyo, MASHA-ZU haya ya uadilifu na utangamano yanaondoa udhahania katika kulipata umbotokeo lililofikia upeo wa ukubalifu kwa kuwepo mshabaha baina ya umboghafi na umbotokeo.

Aidha, mashartizuizi haya yanahitaji kwamba umbotokeo ambalo linakubalika katika lugha inayohusika lifanane kwa namna fulani na umboghafi lililoingizwa (Massamba, 2011). Hivyo katika uchanganuzi wa namna mofu zinapofuatana katika lugha ya Kisambaa zinaweza kuathiriana, maumbotokeo yaliyozalishwa na kutathminiwa kwa vigezo vya MASHA-ZU yana mshabaha na maumboghafi. Mashartizuizi hayo ya utangamano ni FIKI UKO, TEGE na SHABI ambayo yametumiwa kupata maumbo ya vitenzi yanayoundwa kwa mofu ambishi na mofu nyambulishi zinazoathiriana yanayokubalika katika sarufi ya lugha ya Kisambaa. MASHA-ZU haya yanafafanuliwa kama ifuatavyo.

**FIKI UKO** (Fikia Ukomo wa Utangamano wa sifa za kimofolojia): Shartizuizi hili katika uchanganuzi wa mfuatano wa mofu zinazounda vitenzi vya Kisambaa na namna zinavyoathiriana linahitajia kwamba, vitenzi vinavyozalishwa viwe na mofu zenye utangamano na mofu zilizomo katika maumboghafi. Kwahiyo, shartizuizi hili linazuia udondoshaji wa mofu yoyote iliyomo katika umboghafi. Baadhi ya vitenzi vinavyoundwa na mofu mbalimbali vinakiuka sharti hili kwa kudondosha baadhi ya mofu. Mfano katika vitenzi vyenye mofu ya ukanushi, yaani vitenzi kanushi, mofu ya njeo na mofu ya nafsi zinadondoshwa kama katika kitenzi **aaja** ‘anakula’ ( a-a-j-a ; Nfs-Nj-Mz-Mi) **kaja** ‘hali’ (ka-j-a; Knsh-Mz-Mi). Katika kitenzi hicho kutokana na

kuambishwa mofu ya ukanushi {ka-} mofu ya nafsi {a-} na mofu ya njeo {-a-} zinadondoshwa.

**TEGE** (Tegemea sifa za kimofolojia): Shartizuizi hili katika uambikaji wa mofu na namna zinavyoathiriana linahitajia kwamba, mofu zilizomo katika umbotokeo zitegemee zile zilizomo katika umboghafi. Shartizuizi hili linazuia uchopezi wa mofu katika umbotokeo tofauti na zile zilizomo katika umboghafi. Katika shartizuizi hili, kuna baadhi ya vitenzi ambavyo ili maumbo yake yaweze kukubalika katika sarufi ya Kisambaa, yanahitaji kuchopeka mofu fulani. Mfano maumbo ya vitenzi yenye mofu ya urejeshi yanachopeka mofu ya njeo ya wakati uliopita ambayo inatokea baada ya mzizi wa kitenzi. Tabia ya vitenzi vyenye umbo hili ni tofauti na vitenzi vingi vya Kisambaa ambapo mofu ya njeo inaambishwa kabla ya mzizi wa kitenzi. Kitenzi hicho ni kama **aiziyeye** 'aliyekuja' (a-iz-iye-ye; Nfs-Mz-Nj-Rjsh). Hivyo katika kitenzi hicho mofu ya njeo imeathiriwa na mofu ya urejeshi ili kuunda kitenzi cha lugha ya Kisambaa chenye urejeshi.

**SHABI** (Shabihiana mofu): Hili ni shartizuizi ambalo katika uundaji wa vitenzi vya Kisambaa kwa uambishaji na unyambulishaji wa mofu linahitajia kwamba, sifa za kimofolojia za mofu katika umbotokeo zishabihiane na sifa za kimofolojia za mofu katika umboghafi. Yaani sifa za mofu zinazounda vitenzi katika maumbotokeo kama nafasi ya mofu njeo katika kitenzi kinachozalishwa ishabihiane na nafasi ya mofu njeo katika umboghafi.

Pamoja na hayo, MASHA-ZU hayo ya utangamano yamebainishwa pamoja na MASHA-ZU ya uziada ambayo yameundwa kutokana na mfuatano na muathiriano

wa mofu katika maumbo ya vitenzi yanayohusika. Kwa mujibu wa maelezo ya Massamba (2011), mashartizuizi ya uziada ni masharti ambayo katika sarufi ya lugha inayohusika kunahitajika kufanyika mabadiliko fulani kwenye maumboghafi ili kuyafanya maumbotokeo yake yakubalike katika sarufi ya lugha hiyo. Hivyo, katika sarufi ya lugha ya Kisambaa, ili kuambika mofu mbalimbali katika vitenzi kunahitajika mabadiliko fulani kwenye maumbo ya vitenzi hivyo ili viweze kukubalika katika sarufi ya lugha hii.

Pamoja na hayo, uchanganuzi wa namna mofu katika kitenzi cha Kisambaa zinavyoathiriana kimofolojia au kimofofonolojia katika mchakato wa uambikaji wa mofu hizo umefanywa kwa kutumia majedwali yenye visanduku ambapo kila kisanduku kinakaliwa na shartizuizi moja. Katika majedwali hayo, maumboghafi yameoneshwa pamoja na mfuatano wa mofu katika maumbo hayo ya vitenzi. MASHA-ZU katika majedwali hayo yamepangwa kulingana na unguvu wa kila shartizuizi katika uambikaji wa mofu ili kuunda vitenzi vya Kisambaa.

Aidha, kwa kuzingatia misingi ya nadharia ya Umbo Upeo kipengele cha usambamba kimezingatiwa katika uchanganuzi wa mofu na namna zinavyoathiriana katika maumbo ya vitenzi vya Kisambaa. Usambamba umezingatiwa kwani uzalishaji wa wa maumboshindani mbalimbali na tathmini ya maumboshindani hayo ili kupata umbo lililofikia upeo wa ukupalifu kwa kuzingatia vigezo vya MASHA-ZU katika mpangilio wa MASHA-ZU umefanyika kwa pamoja na katika hatua moja. Hivyo katika utafiti huu mashartizuizi yamebainishwa ili kuchanganua maumbo mbalimbali ya vitenzi vya Kisambaa kwa kuchunguza namna mofu zinavyoathiriana kimofolojia au kimofofonolojia katika maumbo ya vitenzi hivyo.

### 4.3.1 Kuathiriana kwa mofu ambishi katika kitenzi cha Kisambaa

Data za utafiti huu zinaonesha kuwa, mofu zinapoambishwa katika kitenzi cha Kisambaa huathiriana kimofolojia au kimofofonolojia. Mofu hizi ni zile zinazoambikwa mwanzoni mwa mzizi wa kitenzi katika lugha ya Kisambaa. Mofu ambishi zinazoathiriwa zinapoandamana na mofu ambishi nyingine katika umbo la kitenzi ni pamoja na mofu ya mofimu ya njeo, mofu ishilizi, mofu ya mofimu ya nafsi na mofu ya mofimu ya ukanushi. Mofu hizi zinaathiriwa na mofu ya mofimu ya ukanushi, mofu ya mofimu ya njeo kwa kudondoshwa, kubadilika kwa umbo la mofu na kubadilika kwa nafasi ya utokeaji ya mofu husika katika umbo la kitenzi cha lugha ya Kisambaa. Hata hivyo, katika lugha ya Kisambaa data zinabainisha kuwa maumbo ya vitenzi kanushi, yaani vitenzi vyenye mofu ya ukanushi na maumbo ya vitenzi yakinishi (vitenzi visivyo na mofu ya ukanushi) ndio yenye mofu zinazoathiriana.

Kwa hiyo, katika uchunguzi na uchambuzi wa namna mofu ambishi zinavyoathiriana kimofolojia au kimofofonolojia, vitenzi vilivyotumika ni vitenzi katika hali ya uyakinishi na vitenzi katika hali ya ukanushi ambapo mofu mbalimbali zimefafanuliwa namna zinavyojitokeza katika maumbo ya vitenzi. Mpangilio wa MASHA-ZU katika lugha ya Kisambaa unaoongoza uambishaji wa mofu katika vitenzi hivyo, pia umebainishwa. Mofu ambishi zinazoathiri na kuathiriwa katika umbo la kitenzi zinabainishwa katika vipengele vifuatavyo.

#### 4.3.1.1 Mofu ya nafsi katika kitenzi yakinishi

Mofu ya nafsi katika lugha ya Kisambaa kwenye maumbo ya vitenzi yakinishi inaambishwa kama katika mfano ufuatao.

**MF. 23**

| **Kitenzi** | **Umbo** |
|---|---|
| nitajata ‘ninatembea’ | ni-ta-jat-a |
| | Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |
| nitahaghia ‘ninafagia’ | ni-ta-haghi-a |
| | Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |
| tizajata ‘tulitembea’ | ti-za-jat-a |
| | Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |
| tizahaghia ‘tulifagia’ | ti-za-haghi-a |
| | Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |
| utajata ‘unatembea’ | u-ta-jat-a |
| | Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |
| utahaghia ‘unafagia’ | u-ta-haghi-a |
| | Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |
| mwaajata ‘mlitembea’ | mwa-a-jat-a |
| | Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |
| mwaahaghia ‘mlifagia’ | mwa-a-haghi-a |
| | Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |
| azajata ‘alitembea’ | a-za-jat-a |
| | Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |
| azahaghia ‘alifagia’ | a-za-haghi-a |
| | Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |
| newajate ‘watatembea’ | ne-wa-jat-e |
| | Nj-Nfs-Mz-$M_i$ |
| newahaghie ‘watafagia’ | ne-wa-haghi-e |
| | Nj-Nfs-Mz-$M_i$ |

Katika mfano wa 23 hapo juu, vitenzi vimeambishwa mofu ya nafsi ya kwanza umoja {ni-}, nafsi ya kwanza wingi {ti-}, nafsi ya pili umoja {u-}, nafsi ya pili wingi {mwa-}, nafsi ya tatu umoja {a-} na nafsi ya tatu wingi {wa-}. Data ya vitenzi kumi (10) katika vitenzi kumi na mbili (12) vilivyooneshwa katika mfano huo

zinaonesha kuwa katika lugha ya Kisambaa mofu ya nafsi inatangulia katika kitenzi na ikifuatiwa na mofu ya njeo. Hata hivyo mofu ya nafsi inapoambishwa pamoja na mofu ya njeo ya wakati ujao nafasi ya mofu ya nafsi inabadilika. Hivyo mofu ya njeo ya wakati ujao inaathiri kimofolojia mofu ya nafsi ambapo mfuatano wa mofu hizo unabadilika, badala ya mofu nafsi kuitangulia mofu njeo, katika muktadha huu mofu ya njeo ya wakati ujao inaitangulia mofu ya nafsi katika umbo la kitenzi. Kama inavyoonekana katika umbo la kitenzi **newajate** 'watatembea'. Hivyo basi, mashartizuizi yanayoongoza uambishaji wa mofu ya nafsi katika kitenzi yakinishi cha Kisambaa ni haya hapa chini.

Mashartizuizi: **$T^{yknsh}$ Nfs{#-}- {Nj-}»FIKI UKO»TEGE»SHABI**

**$T^{yknsh}$ Nfs{#-}- {Nj-}**: Shartizuizi hili linaeleza kuwa katika kitenzi yakinishi mofu ya nafsi inaambishwa mwanzoni mwa kitenzi na kufuatiwa na mofu ya njeo.

Tuangalie seti ya MASHA-ZU yanayoongoza uambishaji wa mofu ya nafsi katika kitenzi yakinishi cha Kisambaa.

**Jedwali 4.7: Seti ya MASHA-ZU. Umboghafi: nitajata 'ninatembea'**

| | ni-ta-jat-a<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ | **SETI YA MASHA-ZU** | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Maumbotokeo** | $T^{yknsh}$ Nfs{#-}- {Nj-} | FIKI UKO | TEGE | SHABI |
| a | na-jat-a<br>Nfs-Mz- $M_i$ | !* | ** | | * |
| b | n-jat-a<br>Nfs-Mz- $M_i$ | !* | ** | | * |
| c | ta-jat-a<br>Nj-Mz- $M_i$ | !* | ** | * | * |
| d | ☞ni-ta-jat-a<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ | | | | |

**Chanzo**: Data za Uwandani

Katika jedwali Na. 4.7 tunaona kuna maumbotokea (a) hadi (d) (ingawa yanaweza kuzalishwa mengi zaidi ya hayo). Katika orodha ya maumbotokeo hayo, umbotokeo (a) limekiuka sharti lenye nguvu kabisa kwa mofu ya nafsi kutofuatiwa na mofu ya njeo ingawa mofu ya nafsi ndiyo imetangulia katika kitenzi hicho. Umbo hili pia limevunja shartizuizi la uadilifu FIKI UKO linalohitajia kwamba kila mofu iliyoko katika umboghafi ijitokeze katika umbotokeo kwa kudondosha mofu ya njeo, pia halijavunja TEGE kwa umbo hili limetegemea mofu zilizomo katika umboghafi. Vilevile sifa za kimofolojia hazishabihiani katika umbotokeo hili na umboghafi hivyo kuvunja shartizuizi la SHABI. Hata hivyo, kutokana na umbotokeo (a) kuvunja shartizuizi lenye nguvu kabisa linakosa sifa ya kuwa umbo lililofikia upeo wa ukubalifu hata kama lingekuwa halijavunja MASHA-ZU mengine katika mpangilio msonge wa MASHA-ZU hayo.

Umbotokeo (b) nalo haliwezi kushinda kwa kuwa limevunja shartizuizi lenye nguvu kabisa kwa mofu ya nafsi kutokufuatiwa na mofu ya njeo, japokuwa umbo hili halijavunja shartizuizi la TEGE kwani mofu zilizomo katika umbo hili zimo pia katika umboghafi. Umbo hili pia limevunja shartizuizi linalozuia kudondoshwa kwa mofu yoyote iliyomo katika umboghafi (FIKI UKO) na limevunja pia shartizuizi la TEGE kwa kuwa mofu katika umbo hili hazijategemea mofu katika umboghafi. Umbotokeo (c) pia limekiuka mashartizuizi yote likiwemo lenye nguvu kabisa linalohitajia mofu ya nafsi itangulie ikifuatiwa na mofu ya njeo, katika umbo hilo hamna mofu ya nafsi. Kutokana na umbo hili kuvunja shartizuizi lenye nguvu kabisa mashartizuizi mengine yanakosa umuhimu japokuwa pia yamevunjwa. Umbotokeo (d) ndio limefikia upeo wa ukubalifu kwa kukidhi seti nzima ya MASHA-ZU bila kuvunja shartizuizi lenye nguvu kabisa pamoja na MASHA-ZU mengine katika seti

hiyo. Alama ya mkono (☞) inaonesha kukubalika kwa umbo hilo katika sarufi ya lugha ya Kisambaa.

Kama tulivyoona katika mfano wa 17, nafasi ya mofu ya nafsi inaathiriwa kimofolojia na mofu ya njeo ya wakati ujao kama katika kitenzi **newajate** ‘watatembea’ na **newahaghie** ‘watafagia’. Mashartizuizi yanayoongoza uambishaji wa mofu ya nafsi katika kitenzi yakinishi chenye mofu ya njeo ya wakati ujao ni haya yafuatayo.

Mashartizuizi: **$T^{yknsh}${# Nj$_{jao}$-}- {Nfs-}»FIKI UKO»TEGE»SHABI**

**$T^{yknsh}${# Nj$_{jao}$-}- {Nfs-}** : Shartizuizi hili linatuambia kuwa katika kitenzi yakinishi chenye mofu ya njeo ya wakati ujao, mofu ya njeo inatangulia ikifuatiwa na mofu ya nafsi.

MASHAZU hayo yanawasilishwa katika seti ya MASHAZU ifuatayo.

**Jedwali 4.8: Seti ya MASHA-ZU. Umboghafi: newajate ‘watatembea’**

| | ne-wa-jat-e<br>Nj-Nfs-Mz- $M_i$ | **SETI YA MASHA-ZU** | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Maumbotokeo** | $T^{yknsh}${#Nj$_{jao}$-}- {Nfs-} | FIKI UKO | TEGE | SHABI |
| a | ne-jat-e<br>Nj-Mz- $M_i$ | !* | ** | | * |
| b | wa-ne-jat-a<br>Nfs-Nj-Mz- $M_i$ | !* | ** | * | * |
| c | wa-jat-e<br>Nfs-Mz- $M_i$ | !* | ** | | * |
| d | ☞ne-wa-jat-e<br>Nj-Nfs-Mz- $M_i$ | | | | |

**Chanzo**: Data za Uwandani

Katika jedwali Na. 4.8 hapo juu, kuna maumbotokeo (a) hadi (d) ambayo yamezalishwa na mchakato wa ZALI. Katika orodha hiyo, umbotokeo (a) limevunja shartizuizi lenye nguvu kabisa kwa mofu ya njeo kutokufuatiwa na mofu ya nafsi, katika umbo hilo mofu ya nafsi haipo kabisa. Vilevile umbo hili limevunja FIKI

UKO shartizuizi linalohitajia kila mofu katika umboghafi itokee katika umbotokeo, umbo hli limedondosha mofu ya nafsi. Limevunja pia SHABI, sharti ambalo linahitajia mshabaha wa sifa za kimofolojia katika umboghafi na umbotokeo ambapo katika umbo hilo utokeaji wa mofu haushabihiani na umboghafi. Pamoja na hayo, katika jedwali hilo inaonekana kuwa umbotokeo hili halijavunja TEGE kwani mofu zilizomo katika umbo hili zimo pia katika umboghafi. Hata hivyo umbotokeo (a) halijashinda kutokana na kuvunja MASHA-ZU mengi likiwemo shartizuizi lenye nguvu kabisa.

Umbotokeo (b) nalo limevunja shartizuizi lenye nguvu kabisa kwa kubadilisha nafsi ya utokeaji ya mofu ya njeo na mofu ya nafsi kwani katika umbo hilo mofu ya nafsi imetangulia badala ya mofu ya njeo. Umbo hili pia limekiuka shartizuizi la FIKI UKO kwa kubadili umbo la mofu ishilizi, shartizuizi hili linahitajia kila mofu katika umboghafi itokee katika umbotokeo. Aidha limekiuka MASHA-ZU hafifu ya TEGE na SHABI kutokana na kutokuwepo mshabaha baina ya umbotokeo na umboghafi. Umbo hili pia halijashinda.

Umbotokeo (c) nalo limekiuka shartizuizi lenye nguvu kabisa kwa mfuatano wa mofu njeo na mofu ya nafsi ambapo mofu ya nafsi haijatanguliwa na mofu ya njeo. Limekiuka pia FIKI UKO kutokana na kudondosha mofu ya njeo na limekiuka SHABI. Hata hivyo, umbotokeo hili halijashinda ingawa linaonekana kutokuvunja TEGE ambalo ni shartizuizi hafifu katika mpangilio wa MASHA-ZU ya uambishaji wa mofu ya nafsi katika kitenzi yakinishi chenye mofu ya njeo ya wakati ujao. Umbo (d) ndio umbo la kitenzi yakinishi chenye mofu ya njeo ya wakati ujao ambalo limefikia upeo wa ukubalifu kwa kuwa na mfuatano wa mofu unaokubalika.

Umbo hili halijavunja shartizuizi lenye nguvu kabisa pamoja na MASHA-ZU mengine katika seti ya mashartizuizi hayo.

#### 4.3.1.2 Mofu ya nafsi katika kitenzi kanushi

Data za utafiti huu pia zinadhihirisha kuwa, mofu ya nafsi katika kitenzi chenye mofu ya ukanushi inaweza kuambikwa kama ifuatavyo.

**MF. 24**

| **Kitenzi yakinishi** | **Kitenzi Kanushi** | **Umbo** |
|---|---|---|
| nizaighaa ‘nilipeleka’ | siighae ‘sikupeleka’ | si-igha-e |
| | | Knsh-Mz- $M_i$ |
| nizafisha ‘nilificha’ | sifishiye ‘sikuficha’ | si-fish-iye |
| | | Knsh-Mz- $M_i$ |
| tizaighaa ‘tulipeleka’ | ketiighae ‘hatukupeleka’ | ke-ti-igha-e |
| | | Knsh-$Nfs_{2W}$-Mz-$M_i$ |
| tizafisha ‘tulificha’ | ketifishiye ‘hatukuficha’ | ke-ti-fish-iye |
| | | Knsh-$Nfs_{2W}$-Mz-$M_i$ |
| utaighaa ‘unapeleka’ | kuighaa ‘hupeleki’ | ku-igha-a |
| | | Knsh-Mz- $M_i$ |
| utafisha ‘unaficha’ | kufisha ‘hufichi’ | ku-fish-a |
| | | Knsh- Mz-$M_i$ |
| muzaighaa ‘mlipeleka’ | kemuighae ‘hamkupeleka’ | ke-mu-igha-e |
| | | Knsh-$Nfs_{2W}$-Mz- $M_i$ |
| muzafisha ‘mlificha’ | kemufishiye ‘hamkuficha’ | ke-mu-fish-iye |
| | | Knsh-$Nfs_{2W}$-Mz-$M_i$ |
| aaighaa ‘anapeleka’ | kaighaa ‘hapeleki’ | ka-igha-a |
| | | Knsh-Mz- $M_i$ |
| aafisha ‘anaficha’ | kafisha ‘hafichi’ | ka-fish-a |
| | | Knsh-Mz-$M_i$ |
| waaighaa ‘wanapeleka’ | kewaighaa ‘hawapeleki’ | ke-wa-igha-a |
| | | Knsh-$Nfs_{3W}$-Mz- $M_i$ |
| waafisha ‘wanaficha’ | kewafishiye ‘hatukuficha’ | ke-wa-fish-iye |
| | | Knsh-$Nfs_{3W}$-Mz-$M_i$ |

Katika mfano wa 24 hapo juu, kuna vitenzi yakinishi ambavyo vinaundwa kwa mofu mbalimbali ikiwemo mofu ya nafsi, vitenzi hivyo vimeambishwa mofu ya ukanushi na maumbo yake yamebainishwa. Katika maumbo hayo ya vitenzi kumi na mbili (12) vyenye mofu ya ukanushi tunaona namna mofu ya nafsi inavyojitokeza. Mofu ya nafsi ya kwanza umoja {ni-} inadondoshwa kama katika kitenzi **siighae** na **sifishiye** lakini mofu ya nafsi ya kwanza wingi {ti-} haidondoshwi katika kitenzi kanushi. Vivyo hivyo, kwa mofu ya nafsi ya pili umoja {u-}na mofu ya nafsi ya pili wingi {mu-} ambapo mofu ya nafsi ya pili umoja inadondoshwa na mofu ya nafsi ya pili wingi haidondoshwi katika kitenzi kanushi.

Pamoja na hayo, katika data hizo, mofu ya nafsi ya tatu umoja katika kitenzi kanushi inadondoshwa hali ya kuwa mofu ya nafsi ya tatu wingi katika kitenzi kanushi haidondoshwi. Hivyo, katika data hizo mofu ya ukanushi inaathiri kimofolojia mofu ya nafsi kwa kuidondosha ndipo umbo la kitenzi liweze kukubalika katika sarufi ya lugha ya Kisambaa. Kwa hiyo, uambishaji huo wa mofu ya nafsi katika vitenzi vyenye mofu ya ukanushi unaongozwa na mashartizuizi yafuatayo.

#### 4.3.1.2.1 MASHA-ZU ya mofu ya nafsi ya kwanza umoja katika kitenzi kanushi

Data zinaonesha kuwa uambishaji wa mofu ya nafsi ya kwanza umoja katika kitenzi chenye mofu ya ukanushi unaongozwa na MASHA-ZU haya:

Mashartizuizi: **$T^{Knsh}$ {Ø$Nfs_{1U}$-} »FIKI UKO»TEGE»SHABI**

**$T^{Knsh}$ {Ø$Nfs_{1U}$-}:** Shartizuizi hili linatuambia kuwa katika kitenzi chenye mofu ya ukanushi, mofu ya nafsi ya kwanza umoja inadondoshwa. Hapa shartizuizi hili ndio

lenye nguvu kabisa likifuatiwa na FIKI UKO, TEGE na SHABI katika mpangilio wa mashartizuizi haya yanayofafanua tabia ya vitenzi vya Kisambaa.

**Jedwali 4.9: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: Siighae 'Sikupeleka'**

| | si-igha-e<br>Knsh-Mz- $M_i$ | **SETI YA MASHA-ZU** | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Maumbotokeo** | $T^{Knsh}$ {ØNfs$_{1U}$-} | FIKI UKO | TEGE | SHABI |
| a | si-ni-igha-e<br>Knsh-Nfs-Mz- $M_i$ | !* | | * | * |
| b | si-igha-a<br>Knsh-Mz-Mi | | ** | * | * |
| c | ni-si-igha-e<br>Nfs-Knsh-Mz- $M_i$ | !* | ** | | * |
| d | ☞si-igha-e<br>Knsh-Mz- $M_i$ | | | | |

**Chanzo**: Data za Uwandani

Katika jedwali Na. 4.9 hapo juu, tunaona umbotokeo (a) linavunja shartizuizi linalohitajia mofu ya nafsi idondoshwe, linavunja pia shartizuizi la TEGE linalohitajia mofu katika umbotokeo zitegemee mofu katika umboghafi, hapa kuna uchopezi wa mofu ya nafsi. Umbotokeo hili limevunja pia shartizuizi la SHABI kwa kutokuwepo mshabaha wa sifa za kimofolojia katika umbotokeo na umboghafi. Hivyo kutokana na kuvunja MASHA-ZU hayo likiwemo shartizuizi lenye nguvu kabisa, Umbotokeo (a) halijashinda ingawa halijavunja shartizuizi la FIKI-UKO.

Umbotokeo (b) limekidhi shartizuizi lenye nguvu kabisa linalohitajia kudondoshwa kwa mofu ya nafsi. Hata hivyo, umbo hili halijafikia upeo wa ukubalifu katika Kisambaa kutokana na kuvunja shartizuizi la FIKI-UKO linalohitajia kila mofu katika umboghafi ijitokeze katika umbotokeo, umbo hili limebadili mofu ishilizi

kuwa {-a} badala ya {-e} iliyomo katika umboghafi. Umbo hili pia limevunja shartizuizi la linalohitajia mofu katika umbotokeo zitegemee zile zilizomo katika umboghafi. Aidha, umbotokeo hili limevunja shartizuizi hafifu la SHABI.

Umbotokeo (c) limevunja sharizuizi linahitajia mofu ya nafsi idondoshwe, limevunja pia shartizuizi la uadilifu linalotuambia kwamba ili kufikia umbo lenye ukubalifu, kila mofu katika umboghafi ijitokeze katika umbotokeo na kuzuia uchopezi wa mofu, umbo hili limechopeka mofu ya nafsi. Vilevile, umbo hili limevunja shartizuizi linalohitajia mshabaha wa sifa za kimofolojia katika umboghafi na umbotokeo. Hivyo umbo hili halijafikia upeo wa ukubalifu japokuwa halijavunja shartizuzi la TEGE. Umbo (d) katika orodha ya maumbotokeo (a) hadi (d) ndio limefikia upeo wa ukubalifu kwa kutokuvunja shartizuizi lenye nguvu pamoja na mashartizuizi mengine. Umbo hili ndio linalobainisha uambishaji wa mofu katika vitenzi kanushi ambavyo vinadondosha mofu ya nafsi ya kwanza umoja kutokana na athari za mofu ya ukanushi kimofolojia katika mofu ya nafsi.

#### 4.3.1.2.2 MASHA-ZU ya mofu ya nafsi ya kwanza wingi katika kitenzi kanushi

Mashartizuizi yafuatayo yanabainisha tabia ya vitenzi kanushi vya Kisambaa vyenye mofu ya nafsi ya kwanza wingi.

Mashartizuizi: **$T^{Knsh}$ {#Knsh-$Nfs_{1W}$-} »FIKI UKO»TEGE»SHABI**

**$T^{Knsh}$ {#Knsh-$Nfs_{1W}$-}:** Sharti hili linahitajia kwamba mofu ya ukanushi ndio inaambishwa mwanzoni mwa kitenzi ikifuatiwa na mofu ya nafsi ya kwanza wingi katika kitenzi kanushi. Shartizuizi hili ndio lenye nguvu kabisa na katika maumbo shindani umbo ambalo halitavunja shartizuizi hili ndio litakuwa limeshinda kwa

kuwa limefikia upeo wa ukubalifu kulingana na sarufi ya lugha ya Kisambaa.

**Jedwali 4.10: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: ketiighae 'hatukupeleka'**

| | ke-ti-igha-e<br>Knsh-Nfs-Mz- $M_i$ | **SETI YA MASHA-ZU** | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Maumbotokeo** | $T^{Knsh}$ {#Knsh-$Nfs_{1W}$-} | FIKI UKO | TEGE | SHABI |
| a | ☞ke-ti-igha-e<br>Knsh-Nfs-Mz- $M_i$ | | | | |
| b | ti-ke-igha-a<br>Nfs-Nj-Mz- $M_i$ | !* | ** | * | * |
| c | ke-igha-e<br>Knsh-Mz- $M_i$ | !* | ** | | * |
| d | ti-igha-e<br>Nfs-Mz- $M_i$ | !* | ** | | * |

**Chanzo**: Data za Uwandani

Katika jedwali Na. 4.10 hapo juu, tunaona orodha ya maumbotokeo (a) hadi (d). Katika orodha hiyo umbotokeo (a) limefikia upeo wa ukubalifu kwa mofu ya ukanushi kuitangulia mofu ya nafsi na kila mofu katika umboghafi imejitokeza katika umbotokeo, yaani hakuna udondoshaji wa mofu inayohitajika kuwemo katika umbo hili. Vilevile umbo hili limekidhi shartizuizi linalohitajia mofu katika umbotokeo zitegemee mofu katika umboghafi na limekidhi pia shartizuizi linalohitajia mshabaha wa sifa za kimofolojia kati ya umboghafi na umbotokeo. Umbotokeo (b) halijashinda kutokana na kukiuka shartizuizi lenye nguvu kabisa linalohitajia mofu ya ukanushi itangulie mofu ya nafsi ambapo katika umbo hilo hakuna mofu ya ukanushi. Umbo hili pia limevunja shartizuizi linalofuata FIKI UKO kwani sio kila mofu katika umboghafi imejitokeza katika umbotokeo. Aidha, umbo hili limevinja shartizuizi la TEGE na SHABI.

Pamoja na hayo, umbotokeo (c) halijafikia upeo wa ukubalifu kwani limekiuka shartizuizi lenye nguvu kabisa, limevunja shartizuizi la FIKI UKO na limevunja shartizuizi la SHABI. Hata hivyo, umbo hili halijavunja shartizuizi linalohitajia mofu katika umbotokeo zitegemee mofu katika umboghafi. Umbotokeo (d) nalo halijashinda baada ya kutathminiwa na TATHI kwani limevunja shartizuzi lenye nguvu kabisa linalohitajia mofu ya ukanushi itangulie mofu ya nafsi, pia limevunja shartizuizi linahotijia kila mofu katika umboghafi ijitokeze pia katika umbotokeo ambapo mofu ya ukanushi iliyomo katika umboghafi haijajitokeza katika umbotokeo. Vilevile, umbo hili halijavunja shartizuizi la TEGE ambalo ni hafifu lakini limevunja pia shartizuizi la SHABI.

#### 4.3.1.2.3 MASHA-ZU ya mofu ya nafsi ya pili umoja katika kitenzi kanushi

Data zinaeleza kuwa, katika uambishaji wa mofu ya nafsi ya pili umoja pamoja na mofu ya ukanushi katika kitenzi kanushi mashartizuizi yanatuambia kuwa, mofu ya nafsi inadondoshwa. Mashartizuizi haya yanapangiliwa kama ifuatavyo.

Mashartizuizi: **$T^{Knsh}$ {ØNfs$_{2U}$-} »FIKI UKO»TEGE»SHABI**

Shartizuizi **$T^{Knsh}$ {ØNfs$_{2U}$-}** ndio lenye nguvu kabisa linalohitaji kudondoshwa kwa mofu ya nafsi ya pili umoja. **FIKI UKO** ndio linafuatia likihitajia kila mofu katika umboghafi ijitokeze katika umbotokeo. **TEGE** linatuambia kuwa kila mofu katika umbotokeo itegemee mofu zilizomo katika umboghafi na **SHABI** linalohitaji kushabihiana kwa sifa za kimofolojia katika umboghafi na umbotokeo.

**Jedwali 4.11: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: kuighaa 'hupeleki'**

| | ku-igha-a<br>Knsh-Mz- $M_i$ | **SETI YA MASHA-ZU** | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Maumbotokeo** | $T^{Knsh}$ {ØNfs$_{2U}$-} | FIKI UKO | TEGE | SHABI |
| a | ☞ku-igha-a<br>Knsh-Mz- $M_i$ | | | | |
| b | igha-a<br>Mz- $M_i$ | !* | ** | | * |
| c | ke-igha-a<br>Knsh-Mz- $M_i$ | | ** | * | * |

**Chanzo**: Data za Uwandani

Katika jedwali hilo, umbotokeo (a) limefikia upeo wa ukubalifu kwa kuwa halijavunja shartizuizi lolote likiwemo shartizuizi la juu kabisa. Shartizuizi hili la juu kabisa linahitajia mofu ya nafsi ya pili umoja idondoshwe katika kitenzi chenye mofu ya ukanushi. Umbo hili pia limekidhi mashartizuizi mengine katika seti ya MASHA-ZU yanayoongoza uambishaji wa mofu katika kitenzi kanushi. Umbotokeo (b) limekiuka shrtizuizi lenye nguvu kabisa ambapo umbotokeo hili halina mofu ya ukanushi. Vilevile, umbo hili limekiuka shartizuizi linalohitajia kila mofu katika umboghafi ijitokeze katika umbotokeo na linavunja shartizuizi la SHABI. Umbotokeo hili halijashinda kwa kufikia upeo wa ukubalifu japokuwa halijavunja shartizuizi la TEGE kwani shartizuzi hili ni hafifu katika seti ya MASHA-ZU hayo.

#### 4.3.1.2.4 MASHA-ZU ya mofu ya nafsi ya pili wingi katika kitenzi kanushi

Data zinatuambia kuwa mofu ya nafsi ya pili wingi inapoambishwa katika kitenzi pamoja na mofu ya ukanushi, mofu ya ukanushi inaambishwa mwanzoni mwa kitenzi na kufuatiwa na mofu ya nafsi. Mashartizuizi katika uambishaji wa mofu hizi ni haya:

Mashartizuizi: **$T^{Knsh}$ {#Knsh-Nfs$_{2W}$-} »FIKI UKO»TEGE»SHABI**

**$T^{Knsh}$ {#Knsh-Nfs$_{2W}$-}** sharti hili linahitajia mofu ya ukanushi iambishwe mwanzoni mwa kitenzi ikifuatiwa na mofu ya nafsi.

**Jedwali 4.12: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: kemuighae 'hamkupeleka'**

| | ke-mu-igha-e Knsh-Nfs-Mz-$M_i$ | **SETI YA MASHA-ZU** | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Maumbotokeo** | $T^{Knsh}\{\#Knsh\text{-}Nfs_{2W}\text{-}\}$ | FIKI UKO | TEGE | SHABI |
| a | ☞ke-mu-igha-e Knsh-Nfs-Mz-$M_i$ | | | | |
| b | ke-ti-igha-e Knsh-Nfs-Mz-$M_i$ | !* | ** | * | * |
| c | mu-igha-e Nfs-Mz-$M_i$ | !* | ** | | * |

**Chanzo**: Data za Uwandani

Katika jedwali Na. 4.12 hapo juu, kuna orodha ya maumbotokeo (a) hadi (c). Umbotokeo (a) limefikia upeo wa ukubalifu kwa kutokukiuka shartizuizi lenye nguvu kabisa, pamoja na mashartizuizi mengine katika seti ya MASHA-ZU hayo. Kwa hiyo, umbo hili lina mfuatano wa mofu unaokubalika katika lugha ya Kisambaa kwani mofu ya ukanushi imetangulia na kufuatiwa na mofu ya nafsi ya pili wingi. Umbotokeo (b) halijafikia upeo wa ukubalifu kwani limevunja shartizuizi muhimu na lenye nguvu kabisa linalohitajia mofu ya ukanushi itangulie ikifuatiwa na mofu ya nafsi ya pili wingi katika kitenzi kanushi. Katika umbo hilo mofu ya ukanushi imefuatiwa na mofu ya nafsi ya kwanza wingi.

Aidha, umbo hili limevunja mashartizuizi mengine ambayo ni shartizuizi linalohitajia kila mofu iliyomo katika umboghafi ijitokeze pia katika umbotokeo na sharti jingine linahitajia mofu katika umbotokeo zitegemee mofu katika umboghafi. Vilevile umbo hili limevunja shartizuizi linalohitajia mshabaha wa sifa za kimofolojia katika ya umboghafi na umbotokeo. Umbotokeo (c) nalo halijafikia upeo wa ukubalifu kwa kuwa limekiuka shartizuizi lenye nguvu kabisa kwa mofu ya nafsi kutokutanguliwa na mofu ya ukanushi. Limevunja pia shartizuizi la FIKI UKO

ambapo mofu ya ukanushi imedondoshwa na limevunja shartizuizi la SHABI. Hata hivyo, umbo hili halijavunja TEGE kwani mofu zilizomo katika umbo hili zimetegemea mofu katika umboghafi.

#### 4.3.1.2.5 MASHA-ZU ya mofu ya nafsi ya tatu umoja katika kitenzi kanushi

Katika uambishaji wa mofu kwenye vitenzi vya Kisambaa kuna sharti kwamba mofu ya nafsi ya tatu umoja inapoambishwa pamoja na mofu ya ukanushi, mofu ya nafsi inadondoshwa. Hivyo mofu ya ukanushi inaathiri mofu ya nafsi ya tatu umoja kimofolojia kwa kudondoshwa. Mashartizuizi katika lugha ya Kisambaa yanayotawala uambishaji wa mofu hizi yanawasilishwa hapa chini.

Mashartizuizi: **$T^{Knsh}$ {ØNfs$_{2U}$-} »FIKI UKO»TEGE»SHABI**

**$T^{Knsh}$ {ØNfs$_{2U}$-}** ndio shartizuizi lenye nguvu kabisa ambalo linahitaji kudondoshwa kwa mofu ya nafsi. Shartizuizi hili likivunjwa kitenzi kinachohusika hakikubaliki katika sarufi ya lugha ya Kisambaa.

**Jedwali 4.13: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: kaighaa 'hapeleki'**

| | ka-igha-a<br>Knsh-Mz-M$_i$ | **SETI YA MASHA-ZU** | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Maumbotokeo** | $T^{Knsh}$ {ØNfs$_{2U}$-} | FIKI UKO | TEGE | SHABI |
| a | ☞ka-igha-a<br>Knsh-Mz-M$_i$ | | | | |
| b | ke-igha-a<br>Knsh-Mz-M$_i$ | | | * | * |
| c | ke-a-igha-a<br>Knsh-Nfs-Mz-M$_i$ | !* | ** | * | * |
| d | ka-a-igha-a<br>Knsh-Nfs-Mz-M$_i$ | !* | ** | * | * |

**Chanzo**: Data za Uwandani

Umbotokeo (a) katika jedwali hapo juu halijavunja shartizuizi lenye nguvu kabisa

linalohitajia mofu ya nafsi ya tatu umoja idondoshwe katika umbo la kitenzi chenye mofu ya ukanushi. Umbo hili pia limekidhi shartizuizi linalohitajia kuwa kila mofu katika umboghafi ijitokeze katika umbotokeo, halijavunja shrtizuizi linalohitajia mofu katika umbotokeo zitegemee mofu katika umboghafi, pamoja na shartizuizi hafifu la uadilifu linalohitajia uwepo wa mshabaha wa sifa za kimofolojia kati ya umbotokeo na umboghafi. Hivyo basi, umbo hili limeshinda kwani ndio lililofikia upeo wa ukubalifu kulingana na vigezo vilivyotathminiwa katika seti ya MASHA-ZU.

Umbotokeo (b) nalo halijakiuka shartizuizi lenye nguvu kabisa kwa kuidondosha mofu ya nafsi ya tatu umoja, pia umbo hili halijavunja shartizuizi linalohitajia kila mofu katika umboghafi itokee katika umbotokeo. Umbo hili linakubalika katika sarufi ya lugha ya Kisambaa. Hata hivyo, umbotokeo hili halijashinda katika muktadha wa umboghafi kwani limevunja shartizuizi linalohitajia mofu katika umbotokeo zitegemee mofu katika umboghafi ambapo sharti hili linazuia uchopezi wa mofu. Katika umbo hili mofu ya ukanushi {ke-} ndiyo imeambishwa badala ya {ka-} iliyomo katika umboghafi. Hivyo kutokana na kuvunja shartizuizi hilo umbo hili pia limevunja shartizuizi linalohitajia sifa za kimofolojia kushabihiana katika ya umboghafi na umbotokeo.

#### 4.3.1.2.6 MASHA-ZU ya mofu ya nafsi ya tatu wingi katika kitenzi kanushi

Mashartizuizi katika uambishaji wa mofu ya nafsi ya tatu wingi na mofu ya ukanushi yanatuambia kuwa mofu ya ukanushi inaambikwa mwanzoni mwa kitenzi ikifuatiwa na mofu ya nafsi. Hivyo katika muktadha huu, mofu ya nafsi haijaathriwa na mofu

ya ukanushi. Mashartizuizi katika uambishaji wa mofu hizo yanapangiliwa kama ifuatavyo.

Mashartizuizi: **$T^{Knsh}$ {#Knsh-$Nfs_{3W}$-} »FIKI UKO»TEGE»SHABI**

**$T^{Knsh}$ {#Knsh-$Nfs_{3W}$-}** shartizuizi hili katika vitenzi vyenye tabia hii ndio lenye nguvu kabisa ambalo linahitajia mofu ya nafsi itokee baada ya mofu ya ukanushi. Umbo la kitenzi kanushi ambalo linaambishwa mofu ya nafsi ya tatu wingi likivunja sharti hili litakuwa halijafikia upeo wa ukubalifu.

**Jedwali 4.14 : Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: kewaighaa 'hawapeleki'**

| | ke-wa-igha-a<br>Knsh-Nfs-Mz-$M_i$ | **SETI YA MASHA-ZU** | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Maumbotokeo** | $T^{Knsh}$ {#Knsh-$Nfs_{3W}$-} | FIKI UKO | TEGE | SHABI |
| a | ☞ke-wa-igha-a<br>Knsh-Nfs-Mz-$M_i$ | | | | |
| b | ke-igha-a<br>Knsh-Mz-$M_i$ | !* | ** | | * |
| c | wa-ke-igha-a<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ | !* | ** | | * |
| d | wa-igha-a<br>Nfs-Mz-$M_i$ | !* | ** | | * |

**Chanzo**: Data za Uwandani

Katika jedwali hilo Na. 4.14 hapo juu, umbotokeo (a) limefikia upeo wa ukubalifu kwa kuwa halijavunja shartizuizi lenye nguvu kabisa linalohitajia mofu ya ukanushi itangulie katika umbo la kitenzi ikifuatiwa na mofu ya nafsi ya tatu wingi. Umbo hili

pia halijavunja shartizuizi linalofuata katika mpangilio msonge wa MASHA-ZU hayo ambalo linahitajia kila mofu katika umboghafi ijitokeze katika umbotokeo. Aidha halijavunja shartizuizi la TEGE pamoja na shartizuizi la SHABI.

Umbotokeo (b) halijafikia upeo wa ukubalifu kwani limekiuka shartizuizi linalohitajia mofu ya ukanushi itangulie katika umbo la kitenzi ikifuatiwa na mofu ya nafsi ya tatu wingi ambapo umbo hili halina mofu ya nafsi. Vilevile limevunja shartizuizi la FIKI UKO kwa kudondosha mofu ya nafsi ya tatu wingi na limevunja shartizuizi la SHABI japokuwa halijavunja shartizuizi hafifu la TEGE. Umbo (c) nalo limevunja shartizuizi lenye nguvu kwa umbo hilo kuokutanguliwa na mofu ya ukanushi na mofu hiyo kufuatiwa na mofu ya nafsi ya tatu umoja. Limevunja pia FIKI UKO na SHABI. Umbo hili pia halijafikia upeo wa ukubalifu japokuwa halijavunja shartizuizi la TEGE kwani hili ni shartizuizi hafifu katika mpangilio wa MASHA-ZU hayo.

Umbotokeo (d) pia halijashinda kwani limevunja shartizuizi lenye nguvu kabisa kwa kutokuambishwa kwa mofu ya ukanushi ambayo inatakiwa itangulie na ifuatiwe na mofu ya nafsi ya tatu wingi. Umbo hili limevunja mashartizuizi ya FIKI UKO na SHABI lakini halijavunja shartizuizi la TEGE.

#### 4.3.1.3 Mofu ya jjeo katika kitenzi yakinishi

Katika kitenzi cha lugha ya Kisambaa mofu ya njeo inaambishwa kama inavyoonekana katika mfano ufuatao.

**MF. 25**

| **Kitenzi** | **Umbo** |
|---|---|
| atashenga ‘anakata’ | a-ta-sheng-a |
| | Nfs-Nj-Mz- $M_i$ |
| utaghula ‘unanunua’ | u-ta-ghul-a |
| | Nfs-Nj-Mz- $M_i$ |
| wazashenga ‘walikata’ | wa-za-shenga-a |
| | Nfs-Nj-Mz- $M_i$ |
| muzaghula ‘mlinunua’ | mu-za-ghul-a |
| | Nfs-Nj-Mz- $M_i$ |
| ashenga ‘anakata’ | a-sheng-a |
| | Nfs-Ø-Mz- $M_i$ |
| aghula ‘ananunua’ | a-ghul-a |
| | Nfs-Ø-Mz- $M_i$ |
| netishenge ‘tutakata’ | ne-ti-sheng-e |
| | Nj-Nfs-Mz- $M_i$ |
| netighule ‘tutanunua’ | ne-ti-ghul-e |
| | Nj-Nfs-Mz- $M_i$ |

Katika data hizo za vitenzi nane (8), maumbo ya vitenzi yanabainisha kuwa mofu ya njeo katika vitenzi yakinishi vya Kisambaa inaambishwa pamoja na mofu ya nafsi, aidha mofu hii inaweza kudondoshwa lakini udondoshaji huo hauondoi dhana ya njeo katika kitenzi.

#### 4.3.1.3.1 MASHA-ZU ya mofu ya wakati uliopo katika kitenzi yakinishi

Katika maumbo ya vitenzi yakinishi vya Kisambaa mofu ya njeo ya wakati uliopo inatanguliwa na mofu ya nafsi. Maumbo ya vitenzi yakinishi vyenye mofu ya njeo ya wakati uliopo yanabainishwa katika jedwali namba 4.15

**Jedwali 4.15: Mofu ya Wakati Uliopo katika Kitenzi Yakinishi**

| **Kitenzi** | **Umbo** |
|---|---|
| a**ta**shenga (anakata) | a-ta-sheng-a<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |
| wa**a**shenga (wanakata) | wa-a-sheng-a<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |
| wa**a**uka (wanaondoka) | wa-a-uk-a<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |
| a**ta**uka (anaondoka) | a-ta-uk-a<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |
| u**ta**vika (unaomba) | u-ta-vik-a<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |
| mwa**a**vika (mnaomba) | mwa-a-vik-a<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |
| mwa**a**heta (mnapeta) | mwa-a-het-a<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |
| a**a**heta (anapeta) | a-a-het-a<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |
| ta**a**iza (tunakuja) | ta-a-iz-a<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |
| mu**ta**iza (mnakuja) | mu-ta-iz-a<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |

**Chanzo:** Data za Uwandani

Katika jedwali Na. 4.15 hapo juu, maumbo ya vitenzi kumi (10) yaliyoorodheshwa yanaonesha mfuatano wa mofu ya nafsi na mofu ya njeo ya wakati uliopo ambapo mofu ya nafsi inatangulia mofu ya njeo. Mpangilio wa MASHA-ZU katika uambishaji wa mofu ya njeo ya wakati uliopo katika vitenzi yakinishi vya Kisambaa ni huu ufuatao.

Mashartizuizi: **$T^{yknsh}$ Nfs {#-}- {$Nj_{po}$-}»FIKI UKO»TEGE»SHABI**

**$T^{yknsh}$ Nfs {#-}- {$Nj_{po}$-}** : Shartizuizi hili linatuambia kuwa katika kitenzi yakinishi chenye mofu ya njeo ya wakati uliopo, mofu ya nafsi inatangulia ikifuatiwa na mofu ya njeo ya wakati uliopo.

MASHAZU hayo yanawasilishwa katika jedwali la seti ya MASHAZU lifuatalo.

**Jedwali 4.16: Seti ya MASHA-ZU. Umboghafi: Atashenga 'Anakata'**

| | a-ta-sheng-a<br>Nfs-Nj-Mz- $M_i$ | **SETI YA MASHA-ZU** | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Maumbotokeo** | $T^{yknsh}$ Nfs {#-}- {$Nj_{po}$-} | FIKI UKO | TEGE | SHABI |
| a | a-te-sheng-a<br>Nfs-Nj-Mz- $M_i$ | | | * | * |
| b | ta-sheng-a<br>Nj-Mz- $M_i$ | !* | ** | | * |
| c | ☞a-ta-sheng-a<br>Nfs-Nj-Mz- $M_i$ | | | | |

**Chanzo**: Data za Uwandani

Katika orodha ya maumbotokeo (a) – (c), umbo tokeo (a) halijafikia upeo wa ukubalifu japokuwa halijavunja shartizuizi lenye nguvu kabisa linalohitajia mofu ya nafsi itangulie ikifuatiwa na mofu ya njeo ya wakati uliopo. Umbo hili limevunja shartizuizi linatuambia kwamba ili kupata umbo la kitenzi linalokubalika katika Kisambaa kila mofu katika umboghafi itokee katika umbotokeo kwani mofu ya njeo ya wakati uliopo {-ta-} imedondoshwa na kuambishwa mofu ya njeo nyingine. Umbo hili pia limevunja shartizuizi linalohitajia mofu katika umbotokeo zitegemee mofu katika umboghafi pamoja na shartizuizi linalotuambia kwamba kuwe na mshabaha wa sifa za kimofolojia za mofu katika umboghafi na umbotokeo.

Umbotokeo (b) nalo halijfikia upeo wa ukubalifu kwa kuvunja shartizuizi lenye nguvu kabisa ambapo katika mfuatano wa mofu zinazounda kitenzi hicho mofu ya njeo ya wakati uliopo haijatanguliwa na mofu ya nafsi. Pia limevunja shartizuizi linalohitajia kila mofu katika umboghafi ijitokeze katika umbotokeo. Vilevile katika umbo hili hakuna mshabaha wa sifa za kimofolojia katika umboghafi na umbotokeo. Hata hivyo, umbotokeo (b) halijavunja shartizuizi hafifu linalohitaji mofu katika umbotokeo zitegemee mofu katika umboghafi. Umbotokeo (c) ndio limekidhi vigezo vya MASHA-ZU katika seti ya mashartizuizi ya uambishaji wa mofu ya njeo ya

wakati uliopo katika vitenzi yakinishi vya Kisambaa.

#### 4.3.1.3.2 MASHA-ZU ya mofu ya wakati uliopita katika kitenzi yakinishi

Katika maumbo ya kitenzi yakinishi cha Kisambaa mofu ya njeo ya wakati uliopita inatanguliwa na mofu ya nafsi. Maumbo ya vitenzi hivyo yanaoneshwa katika jedwali Na. 4.17.

**Jedwali 4.17: Mofu ya Wakati Uliopita katika Kitenzi Yakinishi**

| Kitenzi | Umbo la Kitenzi |
|---|---|
| a**te**oka (alichoma) | a-te-ok-a<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |
| wa**te**uza (walirudisha) | wa-te-uz-a<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |
| m**za**bua (mlifika) | m-za-bu-a<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |
| ti**za**zua (tulivua) | ti-za-zu-a<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |
| a**a**ighaa (alipeleka) | a-a-igha-a<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |
| mwa**a**dosa (mlifuata) | mwa-a-dos-a<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |
| a**i**ighae (amepeleka) | a-i- igha- e<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |
| u**i**ghoshoe (umetengeneza) | u-i-ghosho-e<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |
| mu**i**dosize (mmefuata) | mu –i- dos – ize<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |
| wa**i**ashize (wameacha) | wa-i-ash-ize<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |
| wa**i**ghuliye (wamenunua) | wa-i-ghul-iye<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |
| ti**i**haghiye (tumefagia) | ti-i-hagh-iye<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |
| wa**a**gona (walilala) | wa-a-gona-a<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |

**Chanzo:** Data za Uwandani

Katika data hizo za vitenzi kumi na tatu (13), mofu ya nafsi inaonekana kujitokeza mwanzoni mwa kitenzi ikifuatiwa na mofu ya njeo ya wakati uliopita. MASHA-ZU yanayoongoza uambishaji wa mofu ya njeo ya wakati uliopita yanafafanuliwa kama

ifuatavyo.

Mashartizuizi: **T$^{yknsh}$ Nfs {#-}- {Nj$_{pita}$-}»FIKI UKO»TEGE»SHABI**

**T$^{yknsh}$ Nfs {#-}- {Nj$_{pita}$-}** : Shartizuizi hili linatuambia kuwa katika kitenzi yakinishi chenye mofu ya njeo ya wakati uliopita, mofu ya nafsi inatangulia ikifuatiwa na mofu ya njeo ya wakati uliopita.

MASHAZU hayo yanawasilishwa katika jedwali la seti ya MASHAZU lifuatalo.

**Jedwali 4.18: Seti ya MASHA-ZU. Umboghafi: mzabua 'mlifika'**

| | m-za-bu-a<br>Nfs-Nj-Mz-M$_i$ | **SETI YA MASHA-ZU** | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Maumbotokeo** | T$^{yknsh}$ Nfs {#-}- {Nj$_{pita}$-} | FIKI UKO | TEGE | SHABI |
| a | mwa-bu-a<br>Nfs-Mz-M$_i$ | !* | ** | | * |
| b | mu-za-bu-a<br>Nfs-Nj-Mz- M$_i$ | | | * | * |
| c | ☞m-za-bu-a<br>Nfs-Nj-Mz- M$_i$ | | | | |

**Chanzo**: Data za Uwandani

Katika maumbotokeo yaliyoorodheshwa katika jedwali Na. 4.18, umbo (a) limevunja shartizuizi lenye nguvu kabisa na limevunja shartizuizi linalohitajia kila mofu katika umboghafi ijitokeze katika umbotokeo pamoja na sharti linalohitajia pawepo na mshabaha wa sifa za kimofolojia katika umboghafi na umbotokeo. Hivyo, umbo hili halijashinda japokuwa halijavunja shartizuizi linalohitajia mofu katika umbotokeo zitegemee mofu katika umboghafi.

Umbotokeo (b) halijavunja shartizuizi lenye nguvu kabisa linalohitajia mofu ya nafsi itangulie ikifuatiwa na mofu ya njeo ya wakati uliopita katika kitenzi yakinishi. Katika Kisambaa, mofu ya nafsi ya pili wingi inaweza kuwa {mu-} au {m-} (Besha,

1993; Peterson, 2007). Hivyo umbo hilo linakubalika pia katika Kisambaa. Hata hivyo, umbo hili halijashinda kwani limevunja mashartizuizi mengine hafifu. Limevunja sharti linalohitajia mofu katika umbotokeo zitegemee mofu katika umboghafi ambapo umbo hili limechopeka mofu {mu-}, pia limevunja shartizuizi linalohitajia mshabaha wa sifa za kimofolojia katika umboghafi na umbotokeo.

Umbotokeo (c) ndio limeshinda katika maumbotokeo yaliyoorodheshwa. Umbo hili halijavunja mashartizuizi yote likiwemo shartizuizi lenye nguvu kabisa, alama ya mkono ndiyo inayobainisha kuwa umbo hili ndio lililofikia upeo wa ukubalifu. Pamoja na hayo, katika maumbo ya vitenzi yakinishi vyenye mofu ya njeo ya wakati uliopita timilifu {-i-}, mofu ishilizi inaonekana kubadilika umbo lake. Mofu hiyo badala ya kuwa na umbo{-a} ina umbo {-e}, {-iye} au {-ize} kama inavyoonekana katika vitenzi sita (6) kati ya kumi na tatu (13) vilivyoorodheshwa kwenye jedwali Na. 4.17. Vitenzi hivyo ni **aiighae**, **muidosize, uighoshoe, waiashize, tiihaghiye** na **waighuliye**. Hivyo mofu ishilizi katika maumbo ya vitenzi hivyo imeathiriwa kimofofonolojia na mofu ya njeo ya wakati uliopita timilifu. Mashartizuizi katika uambishaji wa mofu ya njeo ya wakati uliopita timilifu yanatuambia kuwa ili upate umbo la kitenzi cha Kisambaa chenye mofu ya wakati uliopita timilifu, mofu ishilizi katika kitenzi hicho iwe {-e},{-iye} au {-ize}. Mpangilio wa MASHA-ZU katika uambishaji wa mofu hiyo ni:

Mashartizuizi: **$T^{yknsh}$ $Nj_{pita}${-i-} {$M_i$(e, iye-ize}»FIKI UKO»TEGE»SHABI**

**$T^{yknsh}$ $Nj_{pita}${-i-} {$M_i$(e, iye-ize}**: Shartizuizi hili linatuambia kwamba katika umbo la kitenzi yakinishi chenye mofu ya njeo ya wakati uliopita {-i-}, mofu ishilizi itakuwa {-e}, {-iye} au {-ize}.

MASHAZU hayo yanawasilishwa katika jedwali la seti ya MASHAZU lifuatalo.

**Jedwali 4.19: Seti ya MASHA-ZU. Umboghafi: muidosize ‘mmefuata’**

| | mu –i- dos – ize Nfs-Nj-Mz-$M_i$ | **SETI YA MASHA-ZU** | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Maumbotokeo** | $T^{yknsh}Nj_{pita}${-i-} {$M_i$(e, iye-ize} | FIKI UKO | TEGE | SHABI |
| a | ☞mu-i-dos-ize Nfs-Nj-Mz-$M_i$ | | | | |
| b | mu-i-dos-a Nfs-Nj-Mz- $M_i$ | !* | ** | * | * |
| c | mu-dos-ize Nfs-Mz- $M_i$ | !* | ** | | * |

**Chanzo**: Data za Uwandani

Katika orodha ya maumbotokeo hayo, umbotokeo (a) ndio limeshinda kwa kukidhi vigezo vya mashartizuizi yote likiwemo shartizuizi lenye nguvu kabisa linalohitaji mofu ishilizi kuwa {-e}, {-iye} au {-ize} katika kitenzi chenye mofu ya njeo ya wakati uliopita timilifu {-i-}. Umbotokeo (b) halijafikia upeo wa ukubalifu kwa kuwa limevunja shartizuizi lenye nguvu kabisa kwa mofu ishilizi kuwa {-a} badala ya {-e}, {-iye} au {-ize}. Aidha umbo hili pia limevunja sharti linalohitajia kila mofu katika umboghafi ijitokeze katika umbotokeo. Umbo hili vilevile limevunja mashartizuizi hafifu ya TEGE na SHABI. Umbotokeo (c) nalo halijashinda kwa kuvunja shartizuizi lenye nguvu na mashartizuizi mengine ya FIKIUKO na SHABI japokuwa halijavunja shartizuizi la hafifu la TEGE linalohitajia mofu katika umbotokeo zitegemee mofu katika umboghafi.

#### 4.3.1.3.3 MASHA-ZU ya mofu ya wakati ujao katika kitenzi yakinishi

Katika maumbo ya kitenzi yakinishi, data zinaonesha kuwa mofu ya njeo ya wakati ujao inaambishwa kabla ya mofu ya nafsi. Tabia hii ya kitenzi cha Kisambaa inabainisha kuwa mofu ya njeo ya wakati ujao inaathiri mofu ya nafsi kimofolojia

kwa kubadilisha nafasi ya mofu ya nafsi katika umbo la kitenzi. Kwa hiyo, katika lugha ya Kisambaa kuna sharti kwamba mofu ya njeo ya wakati ujao ndiyo inayotangulia katika umbo la kitenzi na kufuatiwa na mofu ya nafsi. Maumbo ya vitenzi vya Kisambaa vyenye tabia hii yanaoneshwa katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 4.20: Mofu ya Wakati Ujao katika Kitenzi Yakinishi**

| **Kitenzi** | **Umbo** |
|---|---|
| netishange (tutachanga) | **ne**-ti-shang-e<br>Nj-Nfs-Mz- $M_i$ |
| neaghule (atanunua) | **ne**-a-ghul-e<br>Nj-Nfs-Mz- $M_i$ |
| nenibee (nitabeza) | **ne**-ni-be-e<br>Nj-Nfs-Mz- $M_i$ |
| newaghue (watachukua) | **ne** –wa- ghu-e<br>Nj-Nfs-Mz- $M_i$ |
| nemuuke (mtaondoka) | **ne**-mu-uk-e<br>Nj-Nfs-Mz- $M_i$ |
| neewaete (wataleta) | **nee**-wa-et-e<br>Nj-Nfs-Mz- $M_i$ |
| neeaize (atakuja) | **nee**-a-iz-e<br>Nj-Nfs-Mz- $M_i$ |

**Chanzo:** Data za Uwandani

Katika jedwali 4.20 hapo juu, vitenzi saba (7) vilivyoorodheshwa zinaonesha kuwa katika maumbo ya vitenzi yakinishi vya Kisambaa, mofu ya njeo ya wakati ujao inaambikwa mwanzoni mwa kitenzi ikifuatiwa na mofu ya nafsi. Mpangilio wa MASHA-ZU katika uambishaji wa mofu ya njeo ya wakati ujao katika vitenzi vya Kisambaa unafafanuliwa hapa chini.

Mashartizuizi: $\mathbf{T^{yknsh}}$ $\mathbf{Nj_{jao}}$ **{#-}- {Nfs-}»FIKI UKO»TEGE»SHABI**

**T$^{yknsh}$ Nj$_{jao}$ {#-}- {Nfs-}**: Shartizuizi hili linahitajia kwamba, katika umbo la kitenzi yakinishi mofu ya njeo ya wakati ujao iambishwe mwanzoni mwa kitenzi ikifuatiwa na mofu ya nafsi.

MASHAZU hayo yanawasilishwa katika jedwali la seti ya MASHAZU lifuatalo.

**Jedwali 4.21: Seti ya MASHA-ZU. Umboghafi: newaghue 'watachukua'**

| | ne –wa- ghu-e<br>Nj-Nfs-Mz- M$_i$ | **SETI YA MASHA-ZU** | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Maumbotokeo** | T$^{yknsh}$ Nj$_{yo}$ {#-}- {Nfs-} | FIKI UKO | TEGE | SHABI |
| a | ☞ ne –wa- ghu-e<br>Nj-Nfs-Mz- M$_i$ | | | | |
| b | wa-ne-ghu-a<br>Nfs-Nj-Mz- M$_i$ | !* | | | |
| c | wa-ghu-e<br>Nfs-Mz- M$_i$ | !* | ** | | * |
| d | wa-nee-ghu-a<br>Nfs-Nj-Mz- M$_i$ | !* | ** | * | * |

**Chanzo**: Data za Uwandani

Katika maumbotokeo (a) – (d) katika jedwali Na. 4.21 hapo juu, umbotokeo (a) limefikia upeo wa ukubalifu kwa kuwa halijavunja shartizuizi lenye nguvu kabisa linalohitajia mofu ya njeo ya wakati ujao itangulie na kufuatiwa na mofu ya nafsi. Umbo hili pia halijavunja mashartizuizi mengine hafifu. Umbotokeo (b) halijafikia upeo wa ukubalifu kwa kuwa limevunja shartizuizi lenye nguvu kabisa ambapo mofu ya njeo haijatangulia na kufuatiwa na mofu ya nafsi. Umbo hili halijavunja mashartizuizi mengine katika seti ya MASHA-ZU hayo lakini haliwezi kushinda kwa sababu limevunja shartizuizi lenye nguvu ambalo halivumiliki.

Umbotokeo (c) nalo limevunja shartizuizi lenye nguvu kabisa kwa kutoambisha mofu ya njeo ya wakati ujao ambayo inaitangulia mofu ya nafsi. Limekiuka pia shartizuizi linalohitajia kila mofu katika umboghafi ijitokeze katika umbotokeo na kuzuia udondoshaji wa mofu, katika umbo hilo mofu ya njeo imedondoshwa. Umbo hili vilevile limevunja shartizuizi la SHABI kwa kutokuwepo kwa mshabaha wa sifa za kimofolojia za mofu katika umboghafi na umbotokeo. Hata hivyo, umbo hili halijavunja shartizuizi la TEGE lakini haliwezi kushinda kwa kuwa limevunja shartizuizi lenye nguvu na mashartizuizi mengine hafifu.

Umbotokeo (d) pia limevunja shartizuizi lenye nguvu kabisa kwani katika umbo hilo mofu ya nafsi ndiyo imetangulia mofu ya njeo. Umbo hili pia limevunja shartizuizi la FIKIUKO kwa kuongeza mofu {nee-} ambayo haipo katika umboghafi na limevunja sharti la TEGE linalohitajia mofu katika umbotokeo zitegemee mofu katika umboghafi na kuzuia uchopekaji. Katika umbo hili mofu ya njeo {nee-} imechopekwa. Katika umbo hili pia hakuna mshabaha wa sifa za kimofolojia za mofu na umboghafi hivyo, limevinja shartizuizi la SHABI. Kwa hiyo, umbo hili halijafikia upeo wa ukubalifu.

#### 4.3.1.4 Mofu ya njeo katika kitenzi kanushi

Katika kitenzi yakinishi cha lugha ya Kisambaa, mofu ya njeo haidondoshwi ila hudondoshwa ikiwa kudondoshwa kwake kunabainisha njeo fulani kama ilivyo katika njeo ya wakati uliopo hali ya kuendelea. Maumbo ya vitenzi vyenye tabia hiyo yanabainishwa katika mfano ufuatao.

**MF. 26**

**Mofu Kapa {Ø} ya Njeo ya Wakati Uliopo**

| **Kitenzi** | **Umbo** |
|---|---|
| tiiza (tunakuja) | ti- Ø-iz-a<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |
| nieta (ninaleta) | ni- Ø-et-a<br>Nfs-Nj-Mz- $M_i$ |
| muonda (mnatafuta) | mu-Ø-ond-a<br>Nfs-Nj-Mz- $M_i$ |
| ughula (unanunua) | u- Ø-ghul-a<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |

Hata hivyo katika mfano wa 26 hapo juu tunabaini vitenzi vyenye mofu ya ukanushi, mofu ya njeo inaathiriwa na mofu ya ukanushi kimofolojia kwa kudondoshwa. Kuathiriana huko kwa mofu katika maumbo ya vitenzi vya Kisambaa kunatawaliwa na mashartizuizi ya uambishaji wa mofu ya ukanushi na mofu ya njeo katika kitenzi cha Kisambaa. Mashartizuizi hayo ndiyo yanayoruhusu maumbo ya vitenzi vilivyoambishwa mofu ya njeo na mofu ya ukanushi yakubalike katika sarufi ya lugha ya Kisambaa. Maumbo hayo ni yale yaliyofikia upeo wa ukubalifu kutokana na kufikia vigezo vya MASHA-ZU hayo.

#### 4.3.1.4.1 MASHA-ZU ya mofu ya njeo ya wakati uliopo katika kitenzi kanushi

Katika maumbo ya vitenzi vya Kisambaa vyenye ukanushi, MASHA-ZU ya lugha hii yanatuambia kuwa ukitaka kupata umbo linalokubalika basi mofu ya njeo idondoshwe. Maumbo hayo yanabainishwa katika jedwali Na. 4.22.

**Jedwali 4.22: Mofu ya Njeo ya Wakati Uliopo katika Kitenzi Kanushi**

| **Kitenzi Yakinishi** | **Umbo** | **Kitenzi Kanushi** | **Umbo** |
|---|---|---|---|
| naashezigha ‘ninacheza’ | na-a-shezigh-a Nfs-Nj-Mz- $M_i$ | sishezigha ‘sichezi’ | si-shezigh-a Knsh-Mz- $M_i$ |
| titashezigha ‘tunacheza’ | ti-ta-shezigh-a Nfs-Nj-Mz- $M_i$ | ketishezigha ‘hatuchezi’ | ke-ti-shezigh-a Knsh-Nfs-Mz- $M_i$ |
| mtaja ‘mnakula’ | m-ta-j-a Nfs-Nj-Mz- $M_i$ | kemuja ‘hamli’ | ke-mu-j-a Knsh-Nfs-Mz- $M_i$ |
| mwaajata ‘mnatembea’ | mwa-a-jat-a Nfs-Nj-Mz- $M_i$ | kemujata ‘hamtembei’ | ke-mu-jat-a Knsh-Nfs-Mz- $M_i$ |
| aaja ‘anakula’ | a-a-j-a Nfs-Nj-Mz- $M_i$ | kaja ‘hali’ | ka-j-a Knsh-Mz- $M_i$ |
| wataghula ‘wananunua’ | wa-ta-ghul-a Nfs-Nj-Mz- $M_i$ | kewaghula ‘hawanunui’ | ke-wa-ghul-a Knsh-Nfs-Mz- $M_i$ |

**Chanzo**: Data za Uwandani

Data hizo za vitenzi sita (6) katika jedwali 4.22 zinabainisha maumbo ya vitenzi kanushi ambapo mofu ya njeo inadondoshwa. Mashartizuizi yanayoongoza mfuatano huu wa mofu katika kitenzi kanushi ni:

Mashartizuizi: **$T^{Knsh}$ {ØNj$_{po}$-} »FIKI UKO»TEGE»SHABI**

**$T^{Knsh}$ {ØNj$_{po}$-}** sharti hili linahitajia kwamba katika kitenzi chenye mofu ya ukanushi mofu ya njeo ya wakati uliopo idondoshwe.

**Jedwali 4.23: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: ketishezigha ‘hatuchezi’**

| | ke-ti-shezigh-a Knsh-Nfs-Mz- $M_i$ | **SETI YA MASHA-ZU** | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Maumbotokeo** | $T^{Knsh}$ {ØNj$_{po}$-} | FIKI UKO | TEGE | SHABI |
| a | ke-shezigh-a Knsh-Mz- $M_i$ | | ** | | * |
| b | ☞ke-ti-shezigh-a Knsh-Nfs-Mz- $M_i$ | | | | |
| c | ti-shezigh-a Nfs-Mz- $M_i$ | !* | ** | | * |
| d | ke-ti-ta-shezigh-a Knsh-Nfs-Nj-Mz- $M_i$ | !* | ** | * | * |

**Chanzo**: Data za Uwandani

Katika jedwali Na. 4.23 hapo juu tunaona kuna maumbotokeo (a) hadi (d) (ingawa yanaweza kuundwa mengi zaidi ya hayo). Katika orodha ya maumbotokeo hayo, umbotokeo (a) halijavunja shartizuizi lenye nguvu kabisa kwani katika umbo hilo hakuna mofu ya njeo ambayo ilihitaji kudondoshwa. Umbo hili limevunja shartizuizi linalohitajia kila mofu katika umboghafi ijitokeze katika umbotokeo kwani mofu ya nafsi imedondoshwa. Pia halijavunja shartizuizi hafifu la TEGE kwani mofu katika umbotokeo zimetegemea mofu katika umboghafi. Hata hivyo, umbo hili pia limevunja shartizuizi linalohitajia kuwepo kwa mshabaha wa sifa za kimofolojia katika umboghafi na umbotokeo. Hivyo, umbo hili halijafikia upeo wa ukubalifu kwa kuvunja mashartizuizi mengine.

Umbotokeo (b) limekidhi seti nzima ya MASHA-ZU bila kuvunja shartizuizi lolote na hivyo, limekubalika kuwa ndio umbotokeo lililofikia upeo wa ukubalifu. Umbotokeo (c) limevunja shartizuizi lenye nguvu kabisa kwa kutokuambisha mofu ya ukanushi. Vilevile limevunja shartizuizi la FIKI UKO kwa kudondosha mofu ya ukanushi na limevunja shartizuizi linalohitajia mshabaha wa sifa za kimofolojia katika umboghafi na umbotokeo. Hata hivyo, umbo hilo halijafikia upeo wa ukubalifu ingwa halijavunja shartizuizi hafifu la TEGE kwani limevunja mashartizuizi yenye nguvu.  Umbotokeo (d) nalo limevunja shartizuizi lenye nguvu kabisa kwa kutoidondosha mofu ya njo na hivyo halijafikia upeo wa ukubalifu.

#### 4.3.1.4.2 MASHA-ZU ya mofu ya wakati uliopita katika kitenzi kanushi

Katika maumbo ya vitenzi vya Kisambaa mofu ya ukanushi na mofu ya njeo ya wakati uliopita inaathiriwa kimofolojia kwa kudondoshwa. Kwa hiyo mofu ya ukanushi na mofu ya njeo ya wakati uliopita hazifuatani katika umbo la kitenzi cha

Kisambaa. Maumbo ya vitenzi vyenye tabia hii yanaoneshwa katika Jedwali 4.24.

**Jedwali 4.24: Mofu ya Njeo ya Wakati Uliopita katika Kitenzi Kanushi**

| Kitenzi Yakinishi | Umbo | Kitenzi Kanushi | Umbo |
|---|---|---|---|
| naashezigha ‘nilicheza’ | na-a-shezigh-a Nfs-Nj-Mz- I | sishezighe ‘sikucheza’ | si-shezigh-e Knsh-Mz- $M_i$ |
| tizashezigha ‘tulicheza’ | ti-za-shezigh-a Nfs-Nj-Mz- $M_i$ | ketishezighe ‘hatukucheza’ | ke-ti-shezigh-e Knsh-Nfs-Mz- $M_i$ |
| mzaja ‘mlikula’ | m-za-j-a Nfs-Nj-Mz- $M_i$ | kemujiye ‘hamkula’ | ke-mu-j-iye Knsh-Nfs-Mz- $M_i$ |
| muzaghula ‘mlinunua’ | mu-za-ghul-a Nfs-Nj-Mz- $M_i$ | kemughuliye ‘hamkununua’ | ke-mu-ghul-iye Knsh-Nfs-Mz- $M_i$ |
| waitozize ‘wameshika’ | a-i-toz-ize Nfs-Nj-Mz- $M_i$ | kewatozize ‘hawakushika’ | ke-wa-toz-ize Knsh-Nfs-Mz- $M_i$ |
| waijatiye ‘wametembea’ | wa-i-jat-iye Nfs-Nj-Mz- $M_i$ | kewajatiye ‘hawakutembea’ | ke-wa-jat-iye Knsh-Nfs-Mz- $M_i$ |

**Chanzo**: Data za Uwandani

Data za vitenzi sita (6) katika jedwali 4.24 hapo juu zinaeleza kuwa katika umbo la kitenzi kanushi mofu ya njeo ya wakati uliopita inadondoshwa, yaani mofu ya ukanushi katika kitenzi cha Kisambaa haiambatani na mofu ya njeo ya wakati uliopita. Hata hivyo, kwa kuwa mofu ya njeo ya wakati uliopita inadondoshwa, maumbo ya vitenzi pia yanapokea mabadiliko mengine ambayo ni kubadilika kwa umbo la mofu ishilizi. Mofu ishilizi katika vitenzi vya Kisambaa vyenye tabia hii inaathiriwa kimofofonolojia, hivyo inabeba umbo {-e}, {-iye} au {-ize}. Mofu ishilizi hizi {-e}, {-iye} na {-ize} zinabeba pia dhana ya njeo ndio sababu katika ubainishaji wa mofu ya njeo ya wakati uliopita Besha (1985) ameionesha mofu {-iye} na {-ize} kama mofu ya njeo ya wakati uliopita. Hivyo basi, katika MASHA-ZU ya uambishaji wa mofu ya njeo katika vitenzi kanushi vya Kisambaa, mofu ya njeo inaambikwa kabla ya mzizi, lakini kutokana na kuathiriwa kimofolojia kwa mofu ya njeo katika kitenzi chenye tabia hii, mofu ya njeo ya wakati uliopita inajibainisha katika mofu ishilizi ambayo inaambikwa baada ya mzizi wa kitenzi.

MASHA-ZU yanayohitajiwa kuzingatiwa katika uambishaji wa mofu ya njeo ya wakati uliopita katika vitenzi kanushi ni haya yafuatayo.

Mashartizuizi: **$T^{Knsh}$ {Ø$Nj_{pita}$-} {-$M_i$($Nj_{pita}$)}»FIKI UKO»TEGE»SHABI**

**$T^{Knsh}$ {Ø$Nj_{pita}$-} {-$M_i$($Nj_{pita}$)}** shartizuizi hili linahitajia kwamba katika vitenzi vyenye mofu ya ukanushi, mofu ya njeo ya wakati uliopita idondoshwe, pia katika mofu ishilizi ndipo mofu hiyo ya njeo ya wakati uliopita inajitokeza.

**Jedwali 4.25: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: kewatozize 'hawakushika'**

| | ke-wa-toz-ize<br>Knsh-Nfs-Mz-$Nj_{pita}$ | **SETI YA MASHA-ZU** | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Maumbotokeo** | $T^{Knsh}$ {Ø$Nj_{pita}$-}{-$M_i$($Nj_{pita}$)} | FIKI UKO | TEGE | SHABI |
| a | ke-toz-a<br>Knsh-Mz-Nj | !* | ** | * | * |
| b | ☞ke-wa-toz-ize<br>Knsh-Nfs-Mz-$Nj_{pita}$ | | | | |
| c | ke-i-wa-toz-ize<br>Knsh-Ymb-Nfs-Mz-$Nj_{pita}$ | | | * | * |
| d | ke-za-toz-ize<br>Knsh-Nj-Mz-$Nj_{pita}$ | !* | ** | * | * |

**Chanzo**: Data za Uwandani

Katika maumbotokeo yaliyozalishwa (a) hadi (d) katika jedwali 4.25 hapo juu, umbotokeo (a) limekiuka shartizuizi lenye nguvu kabisa kwa kutoambisha mofu ishilizi {-ize} ambayo ndiyo inabeba wakati uliopita. Vilevile, umbo hili limevunja MASHA-ZU mengine yote katika seti ya mashartizuizi. Kwa hiyo, umbo hili halijafikia upeo wa ukubalifu. Umbo tokeo (b) limefikia upeo wa ukubalifu kwa kutokuvunja shartizuizi lenye nguvu kabisa pamoja na mashartizuizi mengine.

Umbotokeo (c) halijavunja shartizuizi lenye nguvu kabisa kwa kuidondosha mofu ya njeo na kuambisha mofu ishilizi ya njeo ya wakati uliopita. Vilevile, umbo hili halijavunja sharti jingine lenye nguvu linalohitajia kila mofu katika umboghafi ijitokeze katika umbotokeo. Hata hivyo, umbo hili halijashinda kwani limevunja

mashartizuizi mengine hafifu likiwemo shartizuizi linalozuia uchopezi wa mofu, katika umbo hili mofu ya yambwa imechopekwa. Umbotokeo (d) nalo limevunja shartizuizi lenye nguvu kabisa pamoja na mashartizuizi mengine katika seti ya MASHA-ZU kwa hiyo halijafikia upeo wa ukubalifu.

#### 4.3.1.4.3 MASHA-ZU ya mofu ya njeo ya wakati ujao katika kitenzi kanushi

Katika kitenzi kanushi cha Kisambaa mofu ya njeo ya wakati ujao inaathriwa kimofolojia kwa kudondoshwa katika umbo la kitenzi. Kuathiriwa huko kwa mofu ya njeo ya wakati ujao kunaonekana katika maumbo ya vitenzi vya Kisambaa yaliyoonyeshwa katika Jedwali Na. 4.26.

**Jedwali 4.26: Mofu ya Njeo ya Wakati Ujao katika Kitenzi Kanushi**

| Kitenzi Yakinishi | Umbo | Kitenzi Kanushi | Umbo |
|---|---|---|---|
| neaime ‘atalima’ | ne-a-im-e<br>Nj-Nfs-Mz- $M_i$ | keaime ‘hatalima’ | ke-a-im-e<br>Knsh-Nfs-Mz- $M_i$ |
| netiite ‘tutaenda’ | ne-ti-it-e<br>Nj-Nfs-Mz- $M_i$ | ketiite ‘hatutaenda’ | ke-ti-it-e<br>Knsh-Nfs-Mz- $M_i$ |
| neewauye ‘watarudi’ | nee-wa-uy-e<br>Nj-Nfs-Mz- $M_i$ | kewauye ‘hawatarudi’ | ke-wa-uy-e<br>Knsh-Nfs-Mz- $M_i$ |
| neauze ‘atarudisha’ | ne-a-uz-e<br>Nj-Nfs-Mz- $M_i$ | keauze ‘hatarudisha’ | ke-a-uz-e<br>Knsh-Nfs-Mz- $M_i$ |
| nemuje ‘mtakula’ | ne-mu-j-e<br>Nj-Nfs-Mz- $M_i$ | kemuje ‘hamtakula’ | ke-mu-j-e<br>Knsh-Nfs-Mz- $M_i$ |
| neeaighae ‘atapeleka’ | nee-a-igha-e<br>Nj-Nfs-Mz- $M_i$ | keaighae ‘hatapeleka’ | ke-a-igha-e<br>Knsh-Nfs-Mz- $M_i$ |
| neemtoze‘mtashika’ | nee-m-toz-e<br>Nj-Nfs-Mz- $M_i$ | kemtoze ‘hamtashika’ | ke-m-toz-e<br>Knsh-Nfs-Mz- $M_i$ |

**Chanzo**: Data za Uwandani

Katika data hizo za vitenzi saba (7) vilivyorodheshwa katika jedwali 4.26 tunaona namna ambavyo katika maumbo ya vitenzi kanushi mofu ya njeo ya wakati ujao inadondoshwa. Mashartizuizi ya lugha ya Kisambaa yanayoongoza uambishaji huo wa mofu katika vitenzi hivyo ni haya hapa chini.

Mashartizuizi: **$T^{Knsh}$ {ØNj$_{jao}$-} »FIKI UKO»TEGE»SHABI**

**$T^{Knsh}$\{ØNj$_{jao}$-\}** shartizuizi hili linahitajia kwamba mofu ya njeo ya wakati ujao idondoshwe katika kitenzi chenye ukanushi. Hivyo katika muktadha huu, mofu ya ukanushi inaathiri mofu ya njeo kimofolojia. Maumbo ya vitenzi yenye kukidhi vigezo vya shartizuizi hili ndiyo yenye kufikia upeo wa ukubalifu katika sarufi ya lugha ya Kisambaa.

**Jedwali 4.27: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: kewauye 'hawatarudi'**

| | ke-wa-uy-e<br>Knsh-Nfs-Mz-$M_i$ | **SETI YA MASHA-ZU** | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Maumbotokeo** | $T^{Knsh}$\{ØNj$_{jao}$-\} | FIKI UKO | TEGE | SHABI |
| a | ke-a-uy-e<br>Knsh-Nfs-Mz-$M_i$ | | ** | * | * |
| b | ☞ke-wa-uy-e<br>Knsh-Nfs-Mz-$M_i$ | | | | |
| c | ke-ne-wa-uy-e<br>Knsh-Nj-Nfs-Mz-$M_i$ | !* | ** | * | * |
| d | ke-wa-uy-a<br>Knsh-Nfs-Mz-$M_i$ | | ** | * | * |

**Chanzo**: Data za Uwandani

Katika orodha ya maumbotokeo (a) hadi (d), umbotokeo (a) halijavunja shartizuizi lenye nguzu kabisa kwa kuidondosha mofu ya njeo ya wakati ujao. Pamo na hilo, umbo hili halijashinda kwa kuwa limavunja mashartizuizi mengine. Limevunja shartizuizi linalohitajia kila mofu katika umboghafi ijitokeze katika umbotokeo na kuzuia udondoshaji wa mofu kwa kuidondosha mofu ya nafsi ya tatu wingi. Pia limevunja shartizuzi linalohitajia mofu katika umbotokeo zitegemee mofu katika umboghafi na kuzuia uchopezi wa mofu ambapo mofu ya nafsi ya tatu umoja imechopekwa. Umbotokeo (b) ndio limefikia upeo wa ukubalifu kwa kutokuvunja shartizuzi lolote katika seti ya MASHA-ZU.

Umbotokeo (c) halijashinda kwa kuwa limevunja shartizuizi lenye nguvu kabisa kwa kutokudondosha mofu ya njeo ya wakati ujao. Pia limevunja mashartizuizi mengine

yenye nguvu na hafifu. Umbotokeo (d) halijavunja shartizuizi lenye nguvu kabisa linalohitajia mofu ya njeo idondoshwe ili kupata kitenzi kanushi katika wakati ujao. Hata hivyo, umbo hili halijafikia upeo wa ukubalifu kwani limevunja shartizuzi lenye nguvu kwa kudondosha mofu ishilizi {-e}. limevunja pia shartizuizi linalohitajia mofu katika umbotokeo zitegemee mofu katika umboghafi.

#### 4.3.1.5 Mofu ya masharti katika kitenzi yakinishi

Mofu ya masharti {-ki-} katika maumbo ya vitenzi yakinishi vya Kisambaa inaambishwa kabla ya mzizi, hata hivyo mofu ya masharti inazuia kuambatana na baadhi ya mofu. Maumbo ya vitenzi yenye mofu hii yanabainishwa katika jedwali 4.28.

**Jedwali 4.28: Mofu ya Mofimu ya Masharti katika Kitenzi Yakinishi**

| **Kitenzi** | **Umbo** | **Kitenzi** | **Umbo la Kitenzi** |
|---|---|---|---|
| aaiza ‘anakuja’ | a-a-iz-a<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ | a**ki**iza (akija) | a-ki-iz-a<br>Nfs-Shrt-Mz- $M_i$ |
| nizajata<br>‘nilitembea’ | ni-za-jat-a<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ | ni**ki**jata (nikitembea) | ni-ki-jat-a<br>Nfs-Shrt-Mz- $M_i$ |
| newaje ‘watakula’ | ne-wa-j-e<br>Nj-Nfs-Mz-$M_i$ | wakija (wakila) | wa-ki-j-a<br>Nfs-Shrt-Mz- $M_i$ |
| newaime<br>‘watalima’ | ne-wa-im-e<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ | wa**ki**ima (wakilima) | wa-ki-im-a<br>Nfs-Shrt-Mz- $M_i$ |
| wateghula<br>‘walinunua’ | wa-te-ghul-a<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ | wakighula (wakinunua) | wa-ki-ghul-a<br>Nfs-Shrt-Mz- $M_i$ |
| tizafuka<br>‘tulichimba’ | ti-za-fuk-a<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ | ti**ki**fuka (tukichimba) | ti-ki-fuk-a<br>Nfs-Shrt-Mz- $M_i$ |
| mzawaeta<br>‘mliwaleta’ | m-za-et-a<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ | mkieta (mkileta) | m-ki-et-a<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ |
| waabonda<br>‘walivuna’ | wa-a-bond-a<br>Nfs-Nj-Mz-$M_i$ | m**ki**bonda (mkivuna) | m-ki-bond-a<br>Nfs-Shrt-Mz- $M_i$ |

**Chanzo:** Data za Uwandani

Katika orodha ya vitenzi nane (8) vilivyobainishwa katika jedwali 4.28 utafiti huu unabainisha kuwa maumbo ya vitenzi vyenye mofu ya masharti, mofu ya njeo haifuatani na mofu ya masharti. Kwa hiyo, mofu ya njeo katika kitenzi yakinishi chenye mofu ya masharti inaathiriwa kimofolojia na mofu ya masharti kwa kudondoshwa. Mashartizuizi ya lugha ya Kisambaa yanayotakiwa kufuatwa ili kupata umbo la kitenzi yakinishi chenye mofu ya masharti ni haya yafuatayo.

Mashartizuizi: **T$^{Yknsh}$ {-Shrt}-{ØNj-} »FIKI UKO»TEGE»SHABI**

**T$^{Yknsh}$ {-Shrt}-{ØNj-}** shartizuizi hili linahitajia kwamba ili kupata umbo la kitenzi yakinishi chenye mofu ya masharti basi mofu ya njeo isiambatane na mofu ya masharti. Kwa hiyo, mofu ya njeo inadondoshwa katika vitenzi vyenye maumbo hayo.

**Jedwali 4.29: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: wakiima 'wakilima'**

| | wa-ki-im-a<br>Nfs-Shrt-Mz- $M_i$ | **SETI YA MASHA-ZU** | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Maumbotokeo** | T$^{Yknsh}$ {-Shrt}-{ØNj-} | FIKI UKO | TEGE | SHABI |
| a | ☞wa-ki-im-a<br>Nfs-Shrt-Mz- $M_i$ | | | | |
| b | wa-ki-za-im-a<br>Nfs-Shrt-Nj-Mz- $M_i$ | !* | ** | * | * |
| c | wa-a-ki-im-a<br>Nfs-Nj-Shrt-Mz- $M_i$ | !* | ** | * | * |
| d | wa-te-im-a<br>Nfs-Nj-Mz- $M_i$ | !* | ** | * | * |

**Chanzo**: Data za Uwandani

Katika jedwali 4.29 hapo juu, umbotokeo (a) limekidhi mashartizuizi yote likiwemo shartizuizi lenye nguvu kabisa. kwa hiyo, umbotokeo hili limefikia upeo wa ukubalifu. Umbotokeo (b) limekiuka shartizuizi lenye nguvu kabisa kwa kuambisha

mofu ya njeo baada ya mofu ya masharti ambapo shartizuizi linahitajia kwamba umbotokeo lidondoshe mofu ya njeo. Vilevile, umbo hili limevunja mashartizuizi mengine, hivyo halijafikia upeo wa ukubalifu. Umbotokeo (c) pia limekiuka shartizuizi lenye nguvu kabisa kwa kuambisha mofu ya njeo kabla ya mofu ya masharti. Umbotokeo (d) pia limevunja shartizuizi lenye nguvu kabisa kwa kuambisha mofu ya njeo na kudondosha mofu ya masharti. Hivyo, maumbotokeo (c) na (d) pia hayajafikia upeo wa ukubalifu.

#### 4.3.1.6 Mofu ya masharti katika kitenzi kanushi

Data za utafiti huu zinaonesha kuwa mofu ya ukanushi inaweza kuambishwa pamoja na mofu ya masharti, kwa hiyo mofu ya masharti inaambishwa katika kitenzi kanushi cha Kisambaa. Hata hivyo, katika uambishaji huo wa mofu ya masharti katika kitenzi kanushi, mofu hiyo ya masharti inaathiri kimofolojia mofu za ukanushi {ka-}, {ke-}, {si-} na{ ku-}. Katika maumbo ya vitenzi vyenye mofu ya ukanushi na mofu ya masharti, mofu ya masharti inambatana na mofu ya ukanushi {-she-} tu.

Hivyo, katika uambishaji wa mofu ya masharti katika kitenzi kanushi kuna mashartizuizi ya lugha ya Kisambaa ambayo yanahitaji mofu ya masharti ifuatane na mofu ya ukanushi {-she-}. Kama tulivyoona Kisambaa kina mofu mbalimbali za ukanushi ambazo ni {ka-}, {ke-}, {si-},{ ku-} na {-she-}, hivyo mofu ya masharti inakubali kuambatana na mofu {-she-} na si nyinginezo katika maumbo ya vitenzi kanushi vya Kisambaa. Maumbo ya vitenzi kanushi vyenye mofu ya masharti yanabainishwa katika jedwali Na. 4.30.

**Jedwali 4.30: Mofu ya Mofimu ya Masharti katika Kitenzi Kanushi**

| Kitenzi Kanushi | Umbo | Kitenzi Knsh chenye Shrt | Umbo |
|---|---|---|---|
| kashama "hahami' | ka-sham-a<br>Knsh- Mz –$M_i$ | akisheshama<br>'asipohama' | a-ki-she-sham-a<br>Nfs-Shrt-Knsh-Mz- $M_i$ |
| kueta'huleti' | ku-et-a<br>Knsh- Mz –$M_i$ | ukisheeta 'usipoleta' | u-ki-she-et-a<br>Nfs-Shrt-Knsh-Mz- $M_i$ |
| keaime 'hatalima' | ke-a-im-e<br>Knsh-Nfs- Mz –$M_i$ | akisheima 'asipolima' | a-ki-she-im-a<br>Nfs-Shrt-Knsh-Mz- $M_i$ |
| siavya 'sitoi' | si-avy-a<br>Knsh- Mz –$M_i$ | nikisheavya<br>'nisipotoa' | ni-ki-she-avy-a<br>Nfs-Shrt-Knsh-Mz- $M_i$ |
| kewauza<br>'hawarudishi' | ke-wa-uz-a<br>Knsh- Nfs-Mz –$M_i$ | wakisheuza<br>'wasiporudisha' | wa-ki-she-uz-a<br>Nfs-Shrt-Knsh-Mz- $M_i$ |
| kuawa 'hutoki' | ku-aw-a<br>Knsh- Mz –$M_i$ | ukisheawa<br>'usipotoka' | u-ki-she-aw-a<br>Nfs-Shrt-Knsh-Mz- $M_i$ |
| kemudodoa<br>'hamuokoti' | ke-mu-dodo-a<br>Knsh- Nfs-Mz –$M_i$ | mkishedodoa<br>'msipookota' | m-ki-she-dodo-a<br>Nfs-Shrt-Knsh-Mz- $M_i$ |
| kawaitange<br>'hakuwaita' | ka-wa-itang-e<br>Knsh-Ymbw-Mz –<br>$M_i$ | akishewaitanga<br>'asipowaita' | a-ki-she-wa-itang-a<br>Nfs-Shrt-Knsh-Ymbw-<br>Mz- $M_i$ |
| kaondiye | ka-ond-iye<br>Knsh- Mz –$M_i$ | akisheonda<br>'asipotafuta' | a-ki-she-ond-a<br>Nfs-Shrt-Knsh-Mz- $M_i$ |
| kewashenga<br>'hawakati' | ke-wa-sheng-a<br>Knsh- Nfs-Mz –$M_i$ | wakisheshenga<br>'wasipokata' | wa-ki-she-sheng-a<br>Nfs-Shrt-Knsh-Mz- $M_i$ |

**Chanzo:** Data za Uwandani

Katika data hizo za vitenzi kumi (10) vilivyoorodheshwa katika jedwali 4.30 hapo juu, tunabaini kuwa maumbo ya vitenzi kanushi ambayo hayajaambishwa kwa mofu ya masharti yana mofu mbalimbali za ukanushi katika Kisambaa. Vilevile maumbo ya vitenzi kanushi ambayo yameambishwa pia kwa mofu ya masharti yana mofu {-she-} ya ukanushi. Kwa hivyo, katika lugha ya Kisambaa, mofu ya masharti inaathiri mofu ya ukanushi kimofolojia katika maumbo ya vitenzi. Mashartizuizi

yanayotawala mfuatano huu wa mofu katika uambishaji ili kuunda vitenzi vya Kisambaa ni haya yafuatayo.

Mashartizuizi: **$T^{Knsh}$ {-Shrt}-{$Knsh_{she}$-} »FIKI UKO»TEGE»SHABI**

**$T^{Knsh}$ {-Shrt}-{$Knsh_{she}$-}** shartizuizi hili katika lugha ya Kisambaa linahitajia kwamba, katika kitenzi kanushi mofu ya masharti ifuatiwe na mofu ya ukanushi {-she-}. Kwa hiyo maumbo ya vitenzi yenye tabia hii ndio yanayokubalika katika sarufi ya lugha ya Kisambaa.

**Jedwali 4.31: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: akisheshama 'asipohama'**

| | a-ki-she-sham-a<br>Nfs-Shrt-Knsh-Mz- $M_i$ | **SETI YA MASHA-ZU** | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Maumbotokeo** | $T^{Knsh}$ {-Shrt}-{$Knsh_{she}$-} | FIKI UKO | TEGE | SHABI |
| a | a-ki-ka-sham-a<br>Nfs-Shrt-Knsh-Mz- $M_i$ | !* | ** | * | * |
| b | a-ki-sham-a<br>Nfs-Shrt-Mz- $M_i$ | !* | ** | | * |
| c | a-ki-ke-sham-a<br>Nfs-Shrt-Knsh-Mz- $M_i$ | !* | ** | * | * |
| d | ☞a-ki-she-sham-a<br>Nfs-Shrt-Knsh-Mz- $M_i$ | | | | |

**Chanzo**: Data za Uwandani

Katika maumbotokeo (a) hadi (d) yaliyozalishwa katika jedwali Na. 4.31, umbotokeo (a) halijafikia upeo wa ukubalifu kwani limevunja shartizuizi lenye nguvu kabisa linalohitajia mofu ya masharti ifuatane na mofu ya ukanushi {-she-}. Umbo hili limeambikwa mofu ya ukanushi {-ka-}. Vilevile umbotokeo (a) limevunja mashartizuizi mengine yote katika seti ya MASHA-ZU kwenye jedwali hili. Umbotokeo (b) pia halijashinda kwa kukiuka shartizuizi lenye nguvu kabisa. Pia limekiuka shartizuizi linalohitajia kila mofu katika umboghafi ijitokeze katika umbotokeo ambapo mofu ya ukanushi {-she-} katika umboghafi haijajitokeza katika umbotokeo. Umbo hili pia limevunja shartizuizi linalohitajia sifa za kimofolojia katika umboghafi na umbotokeo zishabihiane.

Umbotokeo (c) nalo halijashinda kwa kuvunja shartizuizi lenye nguvu kabisa kwa kuambika mofu ya ukanushi {-ke-} badala ya {-she-}. Vilevile umbotokeo hili limevunja mashartizuizi mengine yote katika seti ya MASHA-ZU hayo. Umbotokeo (d) ndio limefikia upeo wa ukubalifu kwani mofu ya masharti imeambata na mofu ya ukanushi {-she-} katika umbo la kitenzi. Pamoja na hayo umbotokeo (d) halijavunja mashartizuizi mengine hafifu.

#### 4.3.1.7 Mofu ya ujirejezi katika kitenzi yakinishi

Katika maumbo ya vitenzi yakinishi vya Kisambaa ambavyo vimeambishwa pia kwa mofu ya ujirejezi, mofu hii ya ujirejezi inakubali kuambatana na mofu ya nafsi na mofu ya njeo. Maumbo ya vitenzi hivi yanaoneshwa katika jedwali Na. 4.32.

**Jedwali 4.32: Maumbo ya Vitenzi vyenye Mofu ya Ujirejezi**

| **Kitenzi** | **Umbo la Kitenzi** |
|---|---|
| aa**ki**usha 'anajitoa' | a-a-ki-ush-a<br>Nfs-Nj-Jrjz-Mz- $M_i$ |
| wata**ki**fisha 'wanajificha' | wa-ta-ki-fish-a<br>Nfs-Nj-Jrjz-Mz- $M_i$ |
| muza**ki**eta 'mlijileta' | mu-za-ki-et-a<br>Nfs-Nj-Jrjz-Mz- $M_i$ |
| neti**ki**tae 'tutajihesabu' | ne-ti-ki-ta-e<br>Nj-Nfs-Jrjz-Mz- $M_i$ |
| tii**ki**avize 'tumejitoa' | ti-i-ki-av-ize<br>Nfs-Nj-Jrjz-Mz- $M_i$ |
| neti**ki**nyooshe 'tutajinyoosha' | ne-ti-ki-nyoosh-e<br>Nj-Nfs-Jrjz-Mz- $M_i$ |
| aa**ki**toa 'alijipiga' | a-a-ki-to-a<br>Nfs-Nj-Jrjz-Mz- $M_i$ |

**Chanzo:** Data za Uwandani

Katika data hizo za vitenzi saba (7) kwenye jedwali Na. 4.32, tunaona namna mofu ya ujirejezi inavyoambatana na mofu ya nafsi na mofu ya njeo ili kuunda vitenzi nyenye maumbo yanayokubalika katika lugha ya Kisambaa. Hivyo, katika uambishaji wa mofu ya ujirejezi kuna sharti kuwa mofu hiyo iambatane na mofu ya

nafsi na mofu ya njeo. Tuone mpangilio wa MASHA-ZU ya uambishaji wa mofu ya ujirejezi katika kitenzi cha Kisambaa.

Mashartizuizi: **$T^{Yknsh}$ {#Nfs-Nj}- {Jrjz}»FIKI UKO»TEGE»SHABI**

**$T^{Yknsh}$ {#Nfs-Nj}-{Jrjz}** shartizuizi hili linahitajia kwamba katika kitenzi yakinishi mofu ja ujirejezi inatakiwa itanguliwe na mofu ya nafsi na mofu ya njeo ili kupata umbo linalokubalika katika lugha ya Kisambaa.

**Jedwali 4.33: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: muzakieta 'mlijileta'**

| | mu-za-ki-et-a<br>Nfs-Nj-Jrjz-Mz- $M_i$ | **SETI YA MASHA-ZU** | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Maumbotokeo** | $T^{Yknsh}${#Nfs-Nj}-{Jrjz} | FIKI UKO | TEGE | SHABI |
| a | za-ki-et-a<br>Nj-Jrjz-Mz- $M_i$ | !* | ** | * | * |
| b | mu-ki-et-a<br>Nfs-Shrt-Mz- $M_i$ | !* | ** | | * |
| c | m-za-ki-et-a<br>Nfs-Nj-Jrjz-Mz- $M_i$ | | ** | * | * |
| d | ☞mu-za-ki-et-a<br>Nfs-Nj-Jrjz-Mz- $M_i$ | | | | |

**Chanzo**: Data za Uwandani

Data katika jedwali 4.33 hapo juu zinaonesha kuwa, katika orodha ya maumbotokeo (a) hadi (d), umbotokeo (a) halijashinda kwa kuvunja mashartizuizi yote, yenye nguvu na hafifu. Umbotokeo (b) nalo halijashinda kwani limevunja mashartziuzi yote yakiwemo yenye nguvu. Umbotokeo (c) halijafikia upeo wa ukubalifu ingawa halijavunja shartizuizi lenye nguvu kabisa linalohitajia mofu ya ujirejezi itanguliwe na mofu ya nafsi pamoja na mofu ya njeo. Hivyo, katika Kisambaa umbo hilo linakubalika lakini umbotokeo hili limevunja mashartizuizi mengine. Limevunja sharti linalohitajia kila mofu katika umboghafi ijitokeze katika umbotokeo ambapo mofu {mu-} ya nafsi ya pili wingi imejitokeza kama mofu {m-} ya nafsi ya pili wingi. Vilevile, umbo hili limevunja shartizuizi linalohitajia mofu katika umbotokeo zitegemee mofu katika umboghafi ambapo mofu ya nafsi katika umbotokeo

haijategemea mofu ya nafsi katika umboghafi. Umbotokeo (d) ndio limefikia upeo wa ukubalifu kwa kutokukiuka shartizuizi lenye nguvu kabisa pamoja na mashartizuizi mengine.

### 4.3.1.8 Mofu ya ujirejezi katika kitenzi kanushi

Katika maumbo ya vitenzi vyenye mofu ya ukanushi, mofu ya ujirejezi inaambatana na mofu ya ukanushi {ka-}, {si-}, {ku-},{ke-} na {-she-}. Hata hivyo, katika kitenzi chenye mofu ya njeo ya wakati uliopita na mofu ya ujirejezi, mofu hizi zinaathiri kimofolojia mofu ya ukanushi {-she-}. Mofu hiyo ya ukanushi {-she-} inaathiriwa kwa kutokuandamana na mofu ya ujirejezi katika kitenzi chenye mofu ya njeo ya wakati uliopita. Maumbo ya vitenzi vyenye mofu ya ukanushi pamoja na mofu ya ujirejezi ni haya yafuatayo.

**Jedwali 4.34: Mofu ya Mofimu ya Ujirejezi katika Kitenzi Kanushi**

| **Kitenzi** | **Kitenzi chenye Jrjz** | **Umbo** |
|---|---|---|
| aa**ki**fisha ‘anajificha’ | kakifisha ‘hajifichi’ | ka-ki-fish-a<br>Knsh- Jrjz-Mz-$M_i$ |
| wata**ki**fisha ‘wanajificha’ | kewakifisha ‘hawajifichi’ | ke-wa-ki-fish-a<br>Knsh-Nfs- Jrjz-Mz-$M_i$ |
| uza**ki**fisha‘ulijificha’ | kukifishiye ‘hujajificha’ | ku-ki-fish-iye<br>Knsh- Jrjz-Mz-$M_i$ |
| naa**ki**fisha ‘nilijificha’ | sikifishiye ‘sijajificha’ | si-ki-fish-iye<br>Knsh- Jrjz-Mz-$M_i$ |
| Tiza**ki**fisha ‘tulijificha’ | ★tishekifishe ‘tusijifiche’ | ti-she-ki-fish-e<br>Nfs- Knsh-Jrjz-Mz-$M_i$ |
| muta**k**ighulia ‘mnajinunulia’ | kemukighulia ‘hamjinunulii’ | ke-mu-ki-ghul-i-a<br>Knsh-Nfs- Jrjz-Mz-Tdea-$M_i$ |
| muta**ki**ghulia ‘mnajinunulia’ | ★mushekinguliye ‘msijinunulie’ | mu-she-ki-ghul-iye<br>Nfs- Knsh-Jrjz-Mz-$M_i$ |
| waza**ki**tea ‘walijileta’ | wakishekieta ‘wasipojileta’ | wa-ki-she-ki-et-a<br>Nfs- Knsh-Jrjz-Mz-$M_i$ |
| waa**ki**eta ‘wanajileta’ | kewakieta ‘hawajileti’<br>★wakishekieta ‘wasipojileta’ | ke-wa-ki-et-a<br>Knsh- Jrjz-Mz-$M_i$ |

**Chanzo:** Data za Uwandani

Katika jedwali 4.34 hapo juu, maumbo ya vitenzi saba (7) vyenye ukanushi yanaonesha namna mofu ya ujirejezi inavyoambikwa ambapo inaambata na mofu za ukanushi {ka-}, {si-}, {ku-} na {ke-}. Umbo lenye mofu ya ujirejezi na mofu ya

ukanushi {-she-} lina alama ★ kwa maana ya kwamba umbo hili halina mfuatano unaokubalika katika sarufi ya lugha ya Kisambaa.

Vilevile umbo hilo halitoi maana ya kitenzi kama inavyojitokeza katika kitenzi yakinishi. Katika kitenzi yakinishi **tizakifisha** (tulijificha) kinaeleza tendo katika wakati uliopita, hali ya kuwa ukanushi **tishekifishe** (tusijifiche), tendo linaloelezwa ni la wakati uliopo. Vivyo hivyo kwa kitenzi **mushekinguliye** na **wakishekieta**. Hivyo basi, mfuatano wa mofu ya ukanushi {-she-} na mofu ya ujirejezi katika muktadha huo haukubaliki. Katika lugha ya Kisambaa, kwenye maumbo ya vitenzi kanushi vyenye mofu ya ujirejezi, mofu ya ukanushi {-she-} haifuatani na mofu ya njeo ya wakati uliopita. Mashartizuizi yanayoongoza uambishaji wa mofu hizi ni:

Mashartizuizi: **$T^{Knsh}$ {#Knsh$_{ka,ke,si,ku}$}-{-Jrjz}-{Nj$_{pita}$} »FIKI UKO»TEGE»SHABI**

**$T^{Knsh}$ {#Knsh$_{ka,ke,si,ku}$}-{-Jrjz}-{Nj$_{pita}$}** shartizuizi hili linatuambia kuwa katika vitenzi kanushi, mofu ya ujirejezi inatanguliwa na mofu ya ukanushi {ka-, ke-, si-, au ku} ikifuatiwa na mofu ya njeo ya wakati uliopita. Hivyo, maumbo ya vitenzi vinavyoundwa na mofu hizo za ukanushi zikifuatiwa na mofu ya ujirejezi pamoja na mofu ya njeo ya wakati uliopita ndiyo yanayokubalika katika sarufi ya Kisambaa.

**Jedwali 4.35: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: ketikifishiye 'hatujajificha'**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | ke-ti- ki-fish-iye<br>Knsh-Nfs- Jrjz-Mz- Nj$_{pita}$ | **SETI YA MASHA-ZU** | | | |
| | **Maumbotokeo** | $T^{Knsh}${# **Knsh$_{ka,ke,si,ku}$**}-{-Jrjz}-{Nj$_{pita}$} | FIKI UKO | TEGE | SHABI |
| a | ti-she-za-ki-fish-a<br>Nfs-Knsh-Nj$_{pita}$-Jrjz-Mz-M$_{i}$ | !* | ** | * | * |
| b | ta-she-a-ki-fish-a<br>Nfs-Knsh-Nj$_{pita}$-Jrjz-Mz-M$_{i}$ | !* | ** | * | * |
| c | ti-she-i-ki-fish-e<br>Nfs-Knsh-Nj$_{pita}$-Jrjz-Mz-M$_{i}$ | !* | ** | * | * |
| d | ☞ ke-ti- ki-fish-iye<br>Knsh-Nfs- Jrjz-Mz-Nj$_{pita}$ | | | | |

**Chanzo:** Data za Uwandani

Katika orodha ya maumbotokeo katika jedwali Na. 4.35, umbotokeo (a) halijafikia upeo wa ukubalifu kwa kuvunja shartizuizi lenye nguvu kabisa linalohitajia mofu ya ujirejezi itanguliwe na mofu ya ukanushi {{ka-, ke-, si- au ku} } ikifuatiwa na mofu ya ujirejezi pamoja na mofu ya njeo ya wakati uliopita. Umbo hili pia, limevunja mashartizuizi mengine katika seti ya MASHA-ZU. Umbotokeo (b) pia limevinja shartizuizi lenye nguvu kabisa kwa mofu ya ujirejezi kutanguliwa na mofu ya ukanushi {-she-} na mofu ya njeo ya wakati uliopita. Hivyo umbo hili halijafikia upeo wa ukubalifu. Umbotokeo (c) pia halijafikia upeo wa ukubalifu kwani limekiuka shartizuizi lenye nguvu kabisa pamoja na mashartizuizi mengine katika seti ya MASHA-ZU hayo. Umbotokeo (d) ndio limefikia upeo wa ukubalifu. Umbo hili halijavunja shartizuizi lenye nguvu kabisa linalohitajia mofu ya ujirejezi itanguliwe na mofu ya ukanushi {{ka-, ke-, si-, au ku} ambapo katika umbo hili kumeambishwa mofu ya ukanushi {ke-}. Vilevile umbo hili halijavunja mashartizuizi mengine katika seti ya MASHA-ZU hayo.

### 4.3.2 Kuathiriana kwa mofu nyambulishi

Kwa mujibu wa data za utafiti huu, mofu zinaponyambulishwa katika mzizi wa kitenzi cha Kisambaa haziathiri mofu ambishi ambazo zinatangulia kabla ya mzizi wa kitenzi. Mfuatano huo wa mofu ambishi na mofu nyambulishi katika umbo la kitenzi cha Kisambaa unathibitishwa katika Jedwali 4.36.

**Jedwali 4.36: Mofu Ambishi na Nyambulishi katika Umbo la Kitenzi**

| **Kitenzi** | **Mofu Ambishi** | **Mzizi** | **Mofu Nyambulishi** | **Mofu Yakinishi** |
|---|---|---|---|---|
| waamtoesha (walimpiga sana) | wa- a- m- | -to- | -esh- | -a |
| vizajika (vimelika) | vi-za- | -j- | -ik- | -a |
| muimkemeze (mumemliza) | mu- i-m- | -kem- | -ez- | -e |
| titamhakisha (tunamuogesha sana) | ti-ta- m- | -hak- | -ish- | -a |
| wazaitangiwa | wa-za- | -itang- | -i-w- | -a |

**Chanzo:** Data za Uwandani

Hata hivyo, ingawa mofu nyambulishi haziathiri mofu ambishi katika maumbo ya vitenzi vya Kisambaa, mofu hizi nyambulishi zinaathiriana kimofolojia au kimofofonolojia pale zinapofuatana zaidi ya moja katika umbo la kitenzi. Kaoneka (2009) anaeleza mfuatano wa mofu nyambulishi nne (4) katika kitenzi cha Kisambaa. Hata hivyo, Kaoneka (ameshatajwa) anaendelea kufafanua kuwa katika mfuatano wa mofu nyambulishi zaidi ya moja katika kitenzi, mofu iliyo karibu sana na kitenzi ndiyo inayokubali au kukataa kufuatana na mofu nyambulishi nyinginezo. Aidha, katika kubainisha mfuatano wa mofu nyambulishi zaidi ya moja katika kitenzi hakuna nadharia moja inayoweza kukidhi kueleza mfuatano huo (Rugemalira, 1993; Kaoneka, 2009).

Kwa mujibu wa maelezo ya Kaoneka (ameshatajwa) ametumia Kielelezo cha Kimofolojia cha Hyamna (2003) (Hyman Templatic Morphology - CARP) na nadharia ya Kanuni Tazamishi ya Baker (1985) (Mirror Principle) katika kubainisha na kufafanua mfuatano wa mofu nyambulishi katika vitenzi vya Kisambaa. Kwa kutumia Kielelezo cha Hyman, Kaoneka (ameshatajwa) amebainisha mfuatano wa mofu nyambulishi mbili, tatu na nne. Mofu nyambulishi hizo zinazoweza kufuatana kwa kutumia utaratibu wa Hyman (ameshatajwa) ni **Utendeshi-Utendea**, **Utendeshi- Kutendana**, **Utendea- Kutendana**, **Utendeshi-Utendwa**, **Usababishi-Utendea-Kutendana** na **Utendeshi-Utendea-Ufanyikaji sana-Kutendana**.

Hata hivyo, kwa kutumia utaratibu huo imeshindikana kufanya uchanganuzi wa mfuatano wa mofu nyambulishi za **Kutendana- Utendea** ambao ni mfuatano wa mofu unaokubalika katika vitenzi vya Kisambaa. Kwa hiyo, kwa kutumia Kanuni Tazamishi ya Baker, Kaoneka (ameshatajwa) amebainisha mfuatano wa mofu

nyambulishi ya **Kutendana- Utendea** na **Utendea- Kutendana**. Aidha, lugha ya Kisambaa imeonesha upekee wa mfuatano wa mofu nyambulishi nne katika kitenzi ambazo ni **Utendeshi-Ufanyikaji sana-Utendea-Kutendana** na **Ufanyikaji sana-Utendeshi- Utendea- Kutendana**. Mfuatano huo unaoneshwa katika mfano ufuatao.

**MF. 27**

| **Kitenzi** | **Umbo** |
|---|---|
| memezesheana ‘jazishiana sana’ | mem-ez-esh-e-an-a |
| | Mz-Sbsh-Fnysn-Tdea-Tdna-$M_i$ |
| ighutishiziana ‘shibishiana sana’ | ighut-ish-iz-i-an-a |
| | Mz -Fnysn- Sbsh -Tdea-Tdna-$M_i$ |

Data hizo kutoka kwa Kaoneka (ameshatajwa) zinabainisha namna vitenzi vya Kisambaa vinavyoweza kupokea mofu nyambulishi nne. Aidha, katika utafiti huu, kwa kutumia nadharia ya Umbo Upeo mfuatano wa mofu umebainishwa ambapo mashartizuizi ya lugha ya Kisambaa katika unyambulishaji wa mofu zaidi ya moja katika kitenzi yamedhihirishwa na kufafanuliwa.

Pamoja na hayo, katika mfuatano wa mofu nyambulishi kwenye kitenzi cha Kisambaa, mofu hizo zinaathiriana kimofolojia au kimofofonolojia. Kuathiriana huko kwa mofu nyambulishi kunatokea baina ya mofu ipi itangulie na ipi ifuate, pia mofu yenye umbo gani inatakiwa kufuatana na mofu ipi. Vilevile kuathiriana kwa mofu nyambulishi kunatokea kwa mofu ipi inayotangulia inaruhusu mofu nyingine zipi zaidi ya moja zifuatane nayo. Kwa hiyo, namna mofu nyambulishi katika vitenzi vya Kisambaa zinavyofuatana na kuathiriana kimofolojia au kimofofonolojia kunaelezwa kwa kutumia MASHA-ZU ya lugha ya Kisambaa yanayoongoza

mfuatano wa mofu hizo. Mfuatano huo wa mofu nyambulishi na namna zinavyoathiriana unabainishwa katika vipengele vifuatavyo.

### 4.3.2.1 MASHA-ZU ya mfuatano wa mofu ya utendea na utendwa

Data zinaeleza kuwa, mofu nyambulishi ya mofimu ya utendea na utendwa zinapokuwa pamoja katika kitenzi, mofu ya utendea hutangulia mofu ya utendwa na haiwezi kuwa kinyume chake. Vilevile, mofu ya utedwa inaathiriwa kimofofonolojia na mofu ya utendea kutokana na mfuatano wa mofu hizo katika umbo la kitenzi cha Kisambaa. Kutokana na kuathiriana huko, mofu ya utendwa katika mazingira hayo inakuwa na umbo moja tu la {-w-} ambapo alomofu nyingine za utendwa /-lw-/ na /-ighw-/ zinaathiriwa na kubadilika katika umbo la {-w-} kama inavyodhihirishwa katika Jedwali 4.37.

**Jedwali 4.37: Mofu Nyambulishi ya Utendea Kuathiri Mofu ya Utendwa**

| Kitenzi | Umbo katika Utendwa | Umbo katika Utendea na Utendwa |
|---|---|---|
| doa (gusa) | do-**ighw**-a (guswa) | do-**e**-**w**-a (gusiwa) |
| binda (maliza) | bind-**ighw**-a (malizwa) | bind-**i**-**w**-a (maliziwa) |
| usha (ondoa) | ush-**ighw**-a (ondoshwa) | ush-**i**-**w**-a (ondolewa) |
| honoa (futa) | hono-**lw**-a (futwa) | hono-**e**-**w**-a (futiwa) |
| mosoa (nyofoa) | moso-**lw**-a (nyofolewa) | moso-**e**-**w**-a (nyofolewa) |
| dumua ( kata) | dumu-**lw**-a (katwa) | dumu-**i**-**w**-a (katiwa) |
| gwisha (angusha) | gwish-**w**-a (angushwa) | gwish-**i**-**w**-a (angushiwa) |
| haka (oga) | hak-**w**-a (ogeshwa) | hak-**i**-**w**-a (ogeshewa) |
| eka (acha) | ek-**w**-a (achwa) | ek-**e**-**w**-a (achiliwa) |
| dumua (kata) | dumu-**lw**-a (katwa) | ☆dumu-i-lw-a (katiwa) |
| honoa (futa) | hono-**lw**-a (futwa) | ☆hono-i-lw-a (futiwa) |
| toza (shika) | toz-**ighw**-a (shikwa) | ☆toz-e-ighw-a (shikiliwa) |
| ete (lete) | et-**ighw**-a (letwa) | ☆et-e-ighw-a |

**Chanzo:** Data za Uwandani

Katika jedwali 4.37 hapo juu, maumbotokeo ya vitenzi yenye alama ☆ hayakubaliki katika lugha ya Kisambaa kwa kuwa yamekiuka mashartizuizi yanayotawala mfuatano wa mofu nyambulishi katika mzizi wa kitenzi. Maumbo hayo yanabeba

mofu nyambulishi ya mofimu ya utendea na utendwa ambapo mofu ya mofimu ya utendwa ina maumbo /-lw-/ na /-ighw-/. MASHA-ZU yanayoongoza mfuatano huo katika lugha ya Kisambaa ni haya yafuatayo.

Mashartizuizi: **T({#Tdea}-{-Tdw$_w$}) »FIKI UKO»TEGE»SHABI**

**T({#Tdea}-{-Tdw$_w$})** shartizuizi hili katika mfuatano wa mofu nyambulishi ya utendea na utendwa linatuambia kuwa, katika vitenzi vya Kisambaa vyenye tabia hii, mofu ya utendea itangulie ikifuatiwa na mofu ya utendwa yenye umbo {-w-}. Mpangilio wa MASHA-ZU **T({#Tdea}-{-Tdw$_w$}) »FIKI UKO»TEGE»SHABI** unaoneshwa katika jedwali Na. 4.38.

**Jedwali 4.38: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: doewa 'gusiwa'**

| | do-e-w-a<br>Mz-Tdea-Tdw-M$_i$ | **SETI YA MASHA-ZU** | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Maumbotokeo** | T({#Tdea}-{-Tdw$_w$}) | FIKI UKO | TEGE | SHABI |
| a | do-e-ighw-a<br>Mz-Tdea-Tdw-M$_i$ | !* | ** | * | * |
| b | do-w-e-a<br>Mz-Tdw- Tdea-M$_i$ | !* | ** | * | * |
| c | do-i-lw-a<br>Mz-Tdea-Tdw-M$_i$ | !* | ** | * | * |
| d | ☞do-e-w-a<br>Mz-Tdea-Tdw-M$_i$ | | | | |

**Chanzo**: Data za Uwandani

Umbotokeo (a) katika jedwali Na. 4.38 hapo juu limekiuka shartizuizi lenye nguvu linalohitajia mofu ya utendea kufuatana na mofu ya utendwa {-w-} kwa umbo hili kunyambulishwa kwa mofu ya utendwa {-ighw-}. Umbo hili pia limekiuka shartizuizi lenye nguvu FIKI UKO kwa mofu {-w-} iliyomo katika umboghafi kutojitokeza katika umbotokeo. Vilevile limevunja shartizuizi hafifu linalohitajia mofu katika umbotokeo zitegemee mofu katika umboghafi, katika umbo hili mofu ya utendwa {-ighw-} imechopekwa. Aidha, katika umbo hili hakuna mshabaha wa sifa

za kimofolojia za mofu katika umbotokeo na umboghafi. Hivyo basi, umbotokeo (a) halijafikia upeo wa ukubalifu.

Umbotokeo (b) nalo limevunja shartizuizi lenye nguvu kabisa kwa mofu ya utendea kutokuitangulia mofu ya utendwa ambapo katika umbo hili mofu ya utendwa imeitangulia mofu ya utendea. Umbo hili pia limevunja mashartizuizi mengine katika seti ya MASHA-ZU hivyo, halijafikia upeo wa ukubalifu. Umbotokeo (c) pia limekiuka shartizuizi lenye nguvu kabisa kwa mofu ya utendwa kuwa {-lw-} ambayo inazuiwa kufuatana na mofu ya utendea katika vitenzi vya Kisambaa. Umbotokeo hili halijafikia upeo wa ukubalifu katika sarufi ya Kisambaa. Umbotokeo (d) ndio limefikia upeo wa ukubalifu kwa kutokukiuka mashartizuizi katika seti ya MASHA-ZU hayo likiwemo shartizuizi lenye nguvu kabisa. Hivyo, umbo hili ndio limeshinda katika orodha ya maumbotokeo yaliyozalishwa.

#### 4.3.2.2 MASHA-ZU ya mfuatano wa mofu ya utendea na kutendana

Vilevile data zinaeleza kuwa mofu nyambulishi ya mofimu ya utendea na ya mofimu ya kutendana zinapofuatana katika kitenzi kimoja, mofu ya kutendea inatangulia mofu ya kutendana na si vinginevyo kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 4.39.

**Jedwali 4.39: Mofu Nyambulishi za Mofimu ya Utendea na Kutendana**

| Kitenzi | Umbo katika utendea | Umbo katika kutendea na kutendana |
|---|---|---|
| asha (tupa) | ash-i-a (tupia) | ash-i-an-a (tupiana) |
| ghoshoa (tengeneza) | ghosho-e-a (tengenezea) | ghosho-e-an-a (tengenezeana) |
| zwika (vaa) | zwik-i-a (valia) | zwik-i-an-a (valiana) |
| honoa (futa) | hono-e-a (futia) | hono-e-an-a (futiana) |
| bonda (bonda) | bond-e-a (bondea) | bond-e-an-a (bondeana) |
| fishia (fichia) | fish-i-a (fichia) | fish-i-an-a (fichiana) |
| memeza (jaza) | memez-e-a (jazia) | memez-e-an-a (jaziana) |
| haghia (fagia) | haghi-i-a (fagilia) | haghi-i-an-a (fagiliana) |
| zenga (jenga) | zeng-e-a (jengea) | zeng-e-an-a (fagiliana) |
| sogeza(sogezea) | sogez-e-a (sogezea) | sogez-e an-a (sogezeana) |

**Chanzo:** Data za Uwandani

Kwa hivyo, data ya vitenzi kumi (10) katika jedwali 4.39 inabainisha maumbo ya vitenzi vyenye mofu nyambulishi ya utendea na kutendana. maumbo hayo yanadhihirisha namna mofu hizo zinavyofuatana kwa mofu ya utendea kuitangulia mofu ya kutendana. Mpangilio wa MASHA-ZU katika unyambulishaji wa mofu hizo katika vitenzi vya Kisambaa ni huu ufuatao.

Mashartizuizi: **T({#Tdea}{-Tdna}) »FIKI UKO»TEGE»SHABI**

**T({#Tdea}{-Tdna})** shartizuizi hili linahitaji mofu ya kutendea itangulie mofu ya kutendana katika vitenzi vinavyonyambulishwa kwa mofu hizo.

**Jedwali 4.40: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: ashiana 'tupiana'**

| | ash-i-an-a<br>Mz-Tdea-Tdna-$M_i$ | **SETI YA MASHA-ZU** | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Maumbotokeo** | T({#Tdea}{-Tdna}) | FIKI UKO | TEGE | SHABI |
| a | ash-an-a<br>Mz-Tdna-$M_i$ | !* | ** | | * |
| b | ash-an-i-a<br>Mz-Tdna- Tdea-$M_i$ | !* | ** | * | * |
| c | ash-e-an-a<br>Mz-Tdea-Tdna-$M_i$ | | ** | * | * |
| d | ☞ash-i-an-a<br>Mz-Tdea-Tdna-$M_i$ | | | | |

**Chanzo**: Data za Uwandani

Katika jedwali Na. 4.40 hapo juu, umbotokeo (a) halijashinda kwa kuvunja shartizuizi lenye nguvu kwa mofu ya kutendana kutokutanguliwa na mofu ya utendea. Hata hivyo, umbo hili halijavunja shartizuzi hafifu linalohitajia mofu katika

umbotokeo zitegemee mofu katika umboghafi. Umbotokeo (b) pia halijashinda kwa kuvunja mashartizuizi yote likiwemo sharti lenye nguvu kabisa. Katika umbo hili, mofu ya utendea haijatangulia mofu ya kutendana. Hivyo halikubaliki katika sarufi ya lugha ya Kisambaa.

Umbotokeo (c) halijavunja shartizuizi lenye nguvu kwani katika umbo hili mofu ya utendea imeitangulia mofu ya kutendana. Hata hivyo, umbo hili halijashinda kwani limevunja shartizuizi linalozuia udondoshaji wa mofu zilizomo katika umboghafi ambapo katika umbo hili mofu ya utendea {-i-} imedondoshwa na kuambikwa mofu ya utendea {-e-}. Umbo hili pia limevunja sharti linalozuia uchopezi wa mofu kwani mofu ya utendea {-e-} imechopekwa. Vilevile katika umbo hili hakuna mshabaha wa sifa za kimofolojia pamoja na umboghafi. Umbotokeo (d) ndio limeshinda kwa kufikia upeo wa ukubalifu katika sarufi ya lugha ya Kisambaa. Katika umbo hili mofu ya utendea imeitangulia mofu ya kutendana, pia mofu katika umboghafi zimejitokeza katika umbo hili hakuna udondoshaji. Pamoja na hayo kuna mshabaha wa sifa za kimofolojia katika umbo hili na umboghafi.

#### 4.3.2.3 MASHA-ZU ya mfuatano wa mofu ya utendeshi na utendea

Data zinathibitisha kuwa mofu nyambulishi ya utendeshi na utendea zinapoambikwa kwa pamoja katika mzizi au shina la kitenzi cha lugha ya Kisambaa, mofu ya utendeshi ndio inatangulia mofu ya utendea. Kwa hiyo, mofu ya utendeshi inaiathiri mofu ya utendea kimofolojia kwani mfuatano huu ni tofauti na mofu ya utendea inapoambatana na mofu nyambulishi nyingine. Mfano, mofu ya utendea inapofuatana na mofu ya utendwa na mofu ya kutendana, mofu ya utendea ndiyo inayozitangulia mofu hizo. Tazama Jedwali 4.41 lifuatalo.

**Jedwali 4.41: Mfuatano wa Mofu ya Utendea na Mofu Nyambulishi Nyingine**

| Kitenzi | Umbo | Nafasi ya Mofu ya Kutendea |
|---|---|---|
| waaghuushia (wanafukuzia) | wa-a-ghuu-sh-i-a<br>Nfs-Nj-Mz-Tdsh -Tdea-$M_i$ | inafuatia Mofu ya utendeshi |
| titaushia (tunaondoshea) | ti-ta-u-sh-i-a<br>Nfs-Nj-Mz-Tdsh-Tdea-$M_i$ | inafuatia Mofu ya utendeshi |
| tizammemezea (tulimjazia) | ti-za-m-mem-ez-e-a<br>Nfs-Nj-Tdw-Mz-Tdsh-Tdea- $M_i$ | inafuatia Mofu ya utendeshi |
| gwishizia (angushia) | gwish-iz-i-a<br>Mz-Tdsh-Tdea- $M_i$ | inafuatia Mofu ya utendeshi |
| ghuushizia (fukuzishia) | ghuush-iz-i-a<br>Mz-Tdsh-Tdea- $M_i$ | inatangulia mofu ya utendeshi |
| mzaushiana (mmetoleana) | m-za-ush-i-an-a<br>Nfs-Nj-Mz-Tdea-Tdna- $M_i$ | inatangulia Mofu ya kutendana |
| aatogoewa (alisifiwa) | a-a-togo-e-w-a<br>Nfs-Nj-Mz-Tdea-Tdw- $M_i$ | inatangulia Mofu ya kutendwa |
| nenihaghiiwe (nitafagiliwa) | ne-ni-haghi-i-w-e<br>Nj-Nfs-Mz-Tdea-Tdw- $M_i$ | inatangulia Mofu ya kutendwa |
| watazughaiana (wanafungiana) | wa-za-zugha-i-an-a<br>Nfs-Nj-Mz-Tdea-Tdna- $M_i$ | inatangulia Mofu ya kutendana |

**Chanzo**: Data za Uwandani

Katika data za Jedwali 4.41 hapo juu, mofu ya mofimu ya utendea inapofuatana na mofu ya mofimu ya utendeshi, mofu ya utendea inatanguliwa na mofu ya utendeshi kama katika vitenzi **waaghushiia**, **titaushia**, **titammemezea**. Hata hivyo, katika vitenzi **aatogoewa**, **nenihaghiiwe**, **wazazughaiana**, **gwishizia** na **ghuushizia** mofu ya mofimu ya utendea inazitangulia mofu ya mofimu ya utedwa na mofu ya mofimu ya kutendana. Hivyo katika lugha ya Kisambaa mofu ya utendeshi inaathiri mofu ya utendea, hivyo katika mfuatano wa mofu hizo kuna sharti kuwa si lazima mofu ya utendea iwe inazitangulia mofu nyambulishi nyingine. Mpangilio wa MASHA-ZU katika mfuatano wa mofu utendeshi na utendea katika vitenzi vya Kisambaa yanafafanuliwa hapa chini:

Mashartizuizi: **T({#Tdsh{-Tdea}) »FIKI UKO»TEGE»SHABI**

**T({#Tdsh}{-Tdea})** shartizuizi hili linahitaji kwamba katika kitenzi cha Kisambaa mofu ya usababishi itangulie mofu ya utendea.

**Jedwali 4.42: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: waaghuushia 'wanafukuzia'**

| | wa-a-ghuu-sh-i-a<br>Nfs-Nj-Mz-Tdsh-Tdea-$M_i$ | **SETI YA MASHA-ZU** | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Maumbotokeo** | T({#Tdsh}{-Tdea}) | FIKI UKO | TEGE | SHABI |
| a | wa-a-ghuu-ish-a<br>Nfs-Nj-Mz-Tdsh-$M_i$ | !* | ** | * | * |
| b | ☞wa-a-ghuu-sh-i-a<br>Nfs-Nj-Mz-Tdsh-Tdea-$M_i$ | | | | |
| c | wa-a-ghuu-ish-i-a<br>Nfs-Nj-Mz-Tdsh-Tdea-$M_i$ | | ** | * | * |
| d | wa-a-ghuu-sh-a<br>Nfs-Nj-Mz-Tdsh-$M_i$ | !* | ** | | * |

**Chanzo**: Data za Uwandani

Katika orodha ya maumbotokeo (a) hadi (d) katika jedwali Na. 4.42 hapo juu, umbotokeo (a) limevunja shartizuizi lenye nguvu kabisa kwa mofu ya utendeshi kutokufuatiwa na mofu ya utendea. Umbo hili pia limevunja mashartizuizi mengine hivyo halijafikia upeo wa ukubalifu. Umbotokeo (b) halijavunja shartizuizi lolote katika seti ya mashartizuizi. Hivyo, umbo hili ndio limeshinda kwa kufikia upeo wa ukubalifu katika sarufi ya Kisambaa. Umbotokeo (c) nalo halijakiuka shartizuizi lenye nguvu kabisa kwa mofu ya utendeshi kutangulia na kufuatiwa na mofu ya utendea.

Hata hivyo, umbo hili halijafikia upeo wa ukubalifu kwa kuvunja mashartizuizi mengine katika seti ya MASHA-ZU hayo. Limevunja shartizuizi lenye nguvu la FIKI UKO kwa kudondosha mofu ya utendeshi {-sh-}. Pia limevunja shartizuizi linalohitajia mofu katika umbotokeo zitegemee mofu katika umbo ghafi kwa kuchopeka mofu ya utendeshi {-ish-}. Umbotokeo (d) limevunja shartizuizi lenye

nguvu kabisa kwa mofu ya utendeshi kutokufuatiwa na mofu ya utendea. Kwa hiyo, umbo hili pia halijafikia upeo wa ukubalifu.

#### 4.3.2.4 MASHA-ZU ya mofu ya urejeshi katika kitenzi cha Kisambaa

Vilevile data zinathibitisha kuwa, mofu nyambulishi ya mofimu ya urejeshi inaponyambulishwa katika mzizi wa kitenzi cha Kisambaa inaathiri mofu ishilizi kimofolojia. Mofu ishilizi inaathiriwa kwa kutoonekana kabisa katika kitenzi kwani nafasi ya mofu hiyo inachukuliwa na mofu ya urejeshi. Maumbo ya vitenzi vyenye tabia hii ya unyambulishaji wa mofu yanadhihirika katika jedwali namba 4.43.

**Jedwali 4.43: Mofu ya Mofimu ya Urejeshi Kuathiri Mofu Ishilizi**

| **Kitenzi** | **Umbo la kitenzi rejeshi** |
|---|---|
| adosiyeye (*aliyefuata*) | a-dos-iye-ye<br>Nfs-Mz-Nj-Rjsh |
| washengiyecho (*walichokata*) | wa-sheng-iye-cho<br>Nfs-Mz-Nj-Rjsh |
| waazizecho (*walichopoteza*) | wa-az-ize-cho<br>Nfs-Mz-Nj-Rjsh |
| tiaviyewo (*tuliotoa*) | ti-av-i-iye-wo<br>Nfs-Mz-Nj-Rjsh |
| mghuliyevyo (*mlionunua)* | m-ghul-iye-vyo<br>Nfs-Mz-Nj-Rjsh |
| tiashizevyo (*tulivyoacha*) | ti-ash-ize-vyo<br>Nfs-Mz-Nj-Rjsh |
| aiziyeye (*aliyekuja*) | a-iz-iye-ye<br>Nfs-Mz-Nj-Rjsh |
| nijatiyeye (*niliyetembea*) | ni-jat-iye-wo<br>Nfs-Mz-Nj-Rjsh |

**Chanzo:** Data za Uwandani

Data katika jedwali 4.43 hapo juu, zinaonesha kuwa mofu ishilizi katika maumbo ya vitenzi vyenye mofu nyambulishi ya urejeshi haipo. Katika nafasi ambayo mofu ishilizi ndipo inapojitokeza imeambikwa mofu ya urejeshi.

Pamoja na hayo, data zinaonesha kuwa mofu ya urejeshi katika maumbo ya kitenzi cha Kisambaa inaambatana na mofu ya mofimu ya njeo ya wakati uliopita {-iye-} na

(-ize-) tu. Aidha, mofu hiyo ya njeo imeathiriwa kimofolojia na mofu ya urejeshi kwani nafasi yake imebadilika, badala ya kuambishwa kabla ya mzizi wa kitenzi inajitokeza baada ya mzizi wa kitenzi. Hali hii ya uambishaji wa mofu ya njeo katika vitenzi hivi ni tofauti na namna inavyoambishwa katika vitenzi ambavyo havina mofu ya urejeshi. Hivyo, mofu ya mofimu ya urejeshi inaathiri mofu ya mofimu ya njeo katika mfuatano wa mofu ili kuunda vitenzi mbalimbali vya lugha ya Kisambaa. Muathiriano huo unadhihirishwa katika jedwali namba 4.44.

**Jedwali 4.44: Mofu ya Njeo na Mofu Nyambulishi ya Urejeshi**

| **Kitenzi** | **Umbo** | **Mofu ya Nj na Rjsh** | **Umbo la kitenzi** |
|---|---|---|---|
| azashunga (alifunga) | a-za-shung-a Nfs-Nj-Mz-$M_i$ | ashungiye (aliyefunga) | a-shung-iye-ye Nfs-Mz-Nj-Rjsh |
| neaavye (atatoa) | ne-a-avy-e Nj-Nfs-Mz-$M_i$ | aaviyeye (aliyetoa) | wa-avy-i-ye-wo Nfs-Mz-Nj-Rjsh |
| mwaaeta (mnaleta) | mwa-a-et-a Nfs-Nj-Mz-$M_i$ | aetiyeye (aliyeleta) | a-et-iye-ye Nfs-Mz-Nj-Rjsh |
| titaja (tunakula) | ti-ta-j-a Nfs-Nj-Mz-$M_i$ | tijiyewo (tuliokula) | ti-j-iye-wo Nfs-Mz-Nj-Rjsh |
| nizaaza (nilipoteza) | ni-za-az-a Nfs-Nj-Mz-$M_i$ | niazizeye (niliyepoteza) | ni-az-ize-ye Nfs-Mz-Nj-Rjsh |
| waaasha (walitupa) | wa-a-ash-a Nfs-Nj-Mz-$M_i$ | waashizewo (waliotupa) | wa-ash-ize-wo Nfs-Mz-Nj-Rjsh |
| azaghula (aliaagiza) | a-za-ghul-a Nfs-Nj-Mz-$M_i$ | aghuliyevyo (alivyonunua) | a-aghul-iye-vyo Nfs-Mz-Nj-Rjsh |

**Chanzo:** Data za Uwandani

Data za vitenzi saba (7) katika jedwali Na. 4.43 zinaonesha namna mofu ya njeo inavyobadilika nafasi yake kutokana na kuathiriwa kimofolojia na mofu ya urejeshi. Matokeo ya utafiti huu kuhusu mofu nyambulishi ya mofimu ya urejeshi kuathiri mofu ya mofimu ya njeo yanatofautiana na tabia za vitenzi katika lugha nyingine

kama Kiswahili. Mathalani, katika lugha ya Kiswahili mofu ya urejeshi inaambatana na mofu ya mofimu ya wakati uliopo, uliopita na ujao kama katika MF.28:

**MF.28**

i. a**na***ye*kuja
ii. wa**na***o*lipa
iii. tu**li***o*washa
iv. a**li***cho*leta
v. u**ta**ka*ye*enda
vi. wa**ta**ka*o*fika

Katika mfano wa 28 hapo juu tunabaini kuwa, mofu ya njeo imeandikwa kwa wino wa kukoza na mofu ya urejeshi kwa mlalo. Maumbo hayo ya vitenzi vya Kisambaa na Kiswahili yanadhihirisha kuwa kila lugha ina utaratibu wake na hivyo kuna mashartizuizi ambayo yanatawala maumbotokeo yanayokubalika katika lugha inayohusika. Vilevile, maumbo ya vitenzi nyenye mofu nyambulishi ya urejeshi yanahitaji pia kuambishwa kwa mofu ya nafsi kama inavyoonekana katika maumbo ya vitenzi kwenye jedwali 4.43 na 4.44.

Hivyo mashartizuizi katika mfutano wa mofu kwenye kitenzi chenye mofu ya urejeshi katika lugha ya Kisambaa yanabainishwa kama ifuatavyo.

Mashartizuizi: **T({#Nfs-Mz}{-Nj$_{pita}$}{-Rjshµ}) »FIKI UKO»TEGE»SHABI**

**T({#Nfs-Mz}{-Nj$_{pita}$}{-Rjshµ})**shartizuizi hili linatuambia kwamba ili upate kitenzi cha Kisambaa chenye mofu ya urejeshi, basi katika umbo la kitenzi itangulie mofu ya nafsi kabla ya mzizi wa kitenzi, iwepo mofu ya njeo ya wakati uliopita na mofu ya urejeshi iwe mwishoni mwa kitenzi.

**Jedwali 4.45: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: ashungiyeye 'aliyefunga'**

| | a-shung-iye-ye<br>Nfs-Mz-Nj-Rjsh | SETI YA MASHA-ZU | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Maumbotokeo** | T({#Nfs-Mz}{-$j_{pita}$}{-Rjshµ}) | FIKI UKO | TEGE | SHABI |
| a | shung-iye-ye<br>Mz-Nj-Rjsh | !* | ** | | * |
| b | ☞a-shung-iye-ye<br>Nfs-Mz-Nj-Rjsh | | | | |
| c | a-shung-iye<br>Nfs-Mz-Nj | !* | ** | | * |
| d | a-shung-ize-ye<br>Nfs-Mz-Nj-Rjsh | | ** | * | * |

**Chanzo**: Data za Uwandani

Katika jedwali 4.45 hapo juu, tunaona orodha ya maumbotokeo hayo (a) hadi (d), umbotokeo (a) halijashinda kwa sababu limekiuka mashartizuizi yenye nguvu. Katika umbo hili mofu ya nafsi imedondoshwa hivyo kuvunja sharti lenye nguvu kabisa. Pia umbo hili limevunja sharti linazuia udondoshaji wa mofu ambapo kila mofu katika umboghafi inahitajiwa kujitokeza katika umbotokeo. Umbotokeo (b) ndio limeshinda kwa kutokukiuka shartizuizi lolote yakiwemo mashartizuizi yenye nguvu. Katika umbo hili mofu ya nafsi imetangulia, ukafuata mzizi, ikaambikwa mofu ya njeo baada ya mzizi na mwishoni ikaambikwa mofu ya urejeshi. Hivyo, umbotokeo hili limefikia upeo wa ukubalifu katika sarufi ya lugha ya Kisambaa.

Umbotokeo (c) limevunja shartizuizi lenye nguvu kabisa kwani baada ya mzizi haijaambikwa mofu ya njeo. Pia limevunja sharti linalohitajia kila mofu katika umboghafi ijitokeze katika umbotokeo. Hivyo umbo hili halijafikia upeo wa ukubalifu katika mfuatano wa mofu kwenye umbo la kitenzi chenye mofu ya urejeshi. Umbotokeo (d) halijakiuka shartizuizi lenye nguvu kabisa. Hata hivyo, umbo hili halijashinda kwani limekiuka shartizuizi lenye nguvu la FIKI UKO kwa kudondosha mofu ya njeo {-iye-}. Vilevile, limekiuka shartizuizi linalohitajia mofu katika umbotokeo zitegemee mofu katika umboghafi kwani katika umbo hili mofu

ya njeo {-ize-} imechopekwa. Kutokana na uchopezi huo maana ya kitenzi pia imebadilika, kitenzi **ashungiyeye** kina maana ya **aliyefunga** na kitenzi **ashungizeye** kina maana ya **aliyechungulia**. Hivyo basi, umbo hili halijakidhi vigezo vya mashartizuizi katika seti ya MASHA-ZU.

#### 4.3.2.5 MASHA-ZU ya mfuatano wa mofu ya utendwa na urejeshi

Data za utafiti huu zinaeleza kuwa mofu nyambulishi ya utendwa na mofu nyambulishi ya urejeshi zinaweza kutokea kwa pamoja katika kitenzi cha Kisambaa. Hata hivyo, katika unyambulishaji wa mofu ya utendwa pamoja na mofu ya urejeshi kuna kuathiriwa kwa mofu nyingine zinazoambatana nazo ili kuunda kitenzi chenye umbo linalokubalika katika Kisambaa. Kwa hivyo, katika mfuatano wa mofu hizo mofu ya utendwa inaathiri kimofofonolojia mofu ya njeo ya wakati uliopita {-iye-} ambayo umbo lake linabadilika na kuwa {-e-}. Kwa mujibu ya maelezo ya Besha (1985) umbo {-iye-} ni mofu ya njeo ya wakati uliopita katika Kisambaa. Maumbo ya vitenzi yenye mofu hizo yanabainishwa katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 4.46: Mofu ya Utendwa na Mofu ya Urejeshi**

| **Kitenzi** | **Umbo** |
|---|---|
| ainulweye 'aliyeinuliwa' | a-inu-lw-e-ye<br>Nfs-Mz-Tdw-Nj-Rjsh |
| waghosholwewo 'waliotengenezwa' | wa-ghosho-lw-e-wo<br>Nfs -Mz-Tdw-Nj-Rjsh |
| tietighwewo 'tulioletwa' | ti-et-ighw-e-wo<br>Nfs-Mz-Tdw-Nj-Rjsh |
| nihokighweye 'niliyepokonywa' | ni-hok-ighw-e-ye<br>Nfs-Mz-Tdw-Nj-Rjsh |
| waghuighwewo 'walioolewa' | wa-ghu-ighw-e-wo<br>Nfs-Mz-Tdw-Nj-Rjsh |
| waanikwewo 'walioanikwa' | wa-anik-w-e-wo<br>Nfs-Mz-Tdw-Nj-Rjsh |
| mutibulwewo 'mliochoshwa' | mu-tibu-lw-e-wo<br>Nfs-Mz-Tdw-Nj-Rjsh |

**Chanzo:** Data za Uwandani

Katika data hizo za vitenzi saba (7) kwenye jedwali 4.46, inaonekana mofu ya utendwa na urejeshi katika maumbo ya vitenzi ambapo mofu ya njeo ina umbo {-e-} la wakati uliopita. Kama tulivyoona hapo awali maumbo ya vitenzi yenye mofu ya urejeshi yanahitaji pia mofu ya njeo ya wakati uliopita {-iye-}. Hivyo katika vitenzi vyenye tabia hii, mofu ya njeo inaathiriwa na mofu ya utendwa ambayo umbo lake linabadilika kuwa {-e-}. Pamoja na hayo, nafasi ya mofu ya urejeshi haibadiliki ambapo mofu hii inatokea mwishoni mwa kitenzi. Hivyo MASHA-ZU yanayotawala mfuatano wa mofu hizi yanafafanuliwa kama ifuatavyo.

Mashartizuizi: **T({#Nfs -Mz}{-Tdw}{-Nj$_e$}{-Rjshμ}) »FIKI UKO»TEGE»SHABI**

**T({#Nfs-Mz}{-Tdw}{-Nj$_e$}{-Rjshμ})** shartizuizi hili linatuambia kwamba katika kitenzi chenye mofu ya utendwa na urejeshi, itangulie mofu ya nafsi kabla ya mzizi, ifuatie mofu ya utendwa na mofu ya njeo {-e-} ambapo mofu ya urejeshi itatokea mwishoni mwa kitenzi.

**Jedwali 4.47: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: Waghosholwewo 'Waliotengenezwa'**

| | wa-ghosho-lw-e-wo<br>Nfs -Mz-Tdw-Nj-Rjsh | **SETI YA MASHA-ZU** | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Maumbotokeo** | T({#Nfs-Mz}{-Tdw}{-Nj$_e$}{-Rjshμ}) | FIKI UKO | TEGE | SHABI |
| a | ghosho-lw-e-wo<br>Mz-Tdw-Nj-Rjsh | !* | ** | | * |
| b | ☞wa-ghosho-lw-e-wo<br>Nfs -Mz-Tdw-Nj-Rjsh | | | | |
| c | wa-ghosho-w-e-wo<br>Nfs -Mz-Tdw-Nj-Rjsh | | ** | * | * |
| d | wa-ghosho-lw-iye-wo<br>Nfs -Mz-Tdw-Nj-Rjsh | !* | ** | * | * |

**Chanzo**: Data za Uwandani

Katika jedwali Na. 4.47 hapo juu, umbotokeo (a) halijafikia upeo wa ukubalifu katika sarufi ya Kisambaa kwa kukiuka shartizuizi lenye nguvu kabisa. Katika umbo

hili mofu ya nafsi haijaambishwa. Umbotokeo hili pia limevunja sharti linalohitajia kila mofu katika umboghafi ijitokeze katika umbotokeo kwa kuwa mofu ya nafsi imedondoshwa. Hata hivyo, umbo hili halijakiuka shartizuizi linalohitajia mofu katika umbotokeo zitegemee mofu katika umboghafi. Umbotokeo (b) halijavunja shartizuizi lolote katika seti ya mashartizuizi hivyo ndio umbo lililoshinda katika orodha ya maumbotokeo yaliyozalishwa. Umbotokeo (c) halijavunja shartizuizi lenye nguvu kabisa kwa mofu ya nafsi kutangulia, ukafuata mzizi, kisha mofu ya utendwa inayofuatiwa na mofu ya njeo na mwishoni mwa kitenzi ni mofu ya urejeshi.

Pamoja na hayo, umbo hili halijashinda kwa sababu limevunja shartizuizi lenye nguvu linalohitajia kila mofu katika umbo ghafi ijitokeze katika umbotokeo ambapo katika umbo hili mofu ya utendwa {-lw-} imedondoshwa. Umbo hili pia limevunja mashartizuizi hafifu ya TEGE na SHABI. Umbotokeo (d) nalo limevunja shartizuizi lenye nguvu kabisa kwa mofu ya njeo ya wakati uliopita kuwa {-iye-} badala ya {-e}. Umbotokeo (d) vilevile limevunja mashartizuizi mengine katika seti ya MASHA-ZU kwa hiyo halijafikia upeo wa ukubalifu.

#### 4.3.2.6 MASHA-ZU ya mfuatano wa mofu ya utendea na urejeshi

Mfuatano wa mofu ya utendea na mofu ya urejeshi katika kitenzi cha Kisambaa unaathiri mofu ya njeo ya wakati uliopita. Data za utafiti huu zinabainisha kuwa mofu ya utendea ndiyo inayoathiri kimofofonolojia umbo la mofu ya njeo ya wakati uliopita ambayo inaambatana na mofu nyambulishi ya urejeshi. Umbo hilo la mofu ya njeo ya wakati uliopita linabadilika kuwa {-e-} badala ya {-iye-}. Mifano ya maumbo ya vitenzi hivyo inabainishwa katika jedwali Na. 4.48.

**Jedwali 4.48: Mofu ya Utendea  na Mofu ya Urejeshi**

| **Kitenzi** | **Umbo** |
|---|---|
| nishengeeye 'niliyekatia' | ni-sheng-e-e-ye<br>Nfs-Mz-Tdea-Nj-Rjsh |
| wazengeewo 'waliojengea' | wa-zenge-e-e-wo<br>Nfs -Mz-Tdea-Nj-Rjsh |
| tihaghiieye 'tuliyefagilia' | ti-haghi-i-e-ye<br>Nfs-Mz-Tdea-Nj-Rjsh |
| waghuukieye 'waliyekimbilia' | wa-ghuuk-i-e-ye<br>Nfs-Mz-Tdea-Nj-Rjsh |
| tiashieye 'tuliyetupia' | ti-ash-i-e-ye<br>Nfs-Mz-Tdea-Nj-Rjsh |
| waekieye 'waliyeacha' | wa-ek-i-e-ye<br>Nfs-Mz-Tdea-Nj-Rjsh |
| azughuieye 'aliyefungulia' | a-zughu-i-e-ye<br>Nfs-Mz-Tdea-Nj-Rjsh |
| atekeeye 'aliyechotea' | a-tek-e-e-ye<br>Nfs-Mz-Tdea-Nj-Rjsh |

**Chanzo:** Data za Uwandani

Data jedwali 4.48 hapo juu, tunabaini vitenzi hivyo vyenye mfuatano wa mofu ya utendea na urejeshi zinabainisha tabia za vitenzi vya Kisambaa kwa namna mofu zinavyoathiriana. Kutokana na mfuatano wa mofu ya utendea na urejeshi katika lugha ya Kisambaa pamoja na kuathiriwa kwa mofu zinazoambatana na mofu hizo kama inavyooneshwa katika jedwali Na. 4.48 kuna mashartizuizi ambayo yanaongoza mfuatano wa mofu hizo. Katika vitenzi vya Kisambaa vyenye tabia hii mashartizuizi yafuatayo ndiyo yanayoongoza mfuatano wa mofu hizo ili kitenzi kikubalike katika sarufi ya lugha ya Kisambaa.

Mashartizuizi: **T({#Nfs -Mz}{-Tdea}{-Nj$_e$}{-Rjshµ}) »FIKI UKO»TEGE»SHABI T({#Nfs-Mz}{-Tdea}{-Nj$_e$}{-Rjshµ})** shartizuizi hili linatuambia kwamba katika kitenzi chenye mofu ya utendea na urejeshi, itangulie mofu ya nafsi kabla ya mzizi, ifuatie mofu ya utendea na mofu ya njeo {-e-} ambapo mofu ya urejeshi itatokea mwishoni mwa kitenzi.

**Jedwali 4.49: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: nishengeeye ‘niliyekatia’**

| | ni-sheng-e-e-ye<br>Nfs-Mz-Tdea-Nj-Rjsh | **SETI YA MASHA-ZU** | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Maumbotokeo** | T({#Nfs -Mz}{-Tdea}{-$Nj_e$}{-Rjshµ}) | FIKI UKO | TEGE | SHABI |
| a | ni-sheng-i-iye-ye<br>Nfs-Mz-Tdea-Nj-Rjsh | !* | ** | * | * |
| b | ni-sheng-e-ye<br>Nfs-Mz-Nj-Rjsh | !* | ** | | * |
| c | ☞ni-sheng-e-e-ye<br>Nfs-Mz-Tdea-Nj-Rjsh | | | | |
| d | ni-sheng-e-e-wo<br>Nfs-Mz-Tdea-Nj-Rjsh | | ** | * | * |

**Chanzo**: Data za Uwandani

Katika jedwali 4.49 hapo juu, umbotokeo (a) limekiuka shartizuizi lenye nguvu kabisa kwa mofu ya njeo ya wakati uliopita kuwa {-iye-} badala ya {-e-}. Kutokana na kukiuka shartizuizi hili pamoja na mashartizuizi mengine, umbo hili halijafikia upeo wa ukubalifu katika sarufi ya lugha ya Kisambaa. Umbotokeo (b) pia halijafikia upeo wa ukubalifu kwa kuvunja sharti lenye nguvu kabisa kwani katika umbo hili mofu ya utendea haijanyambulishwa baada ya mzizi wa kitenzi. Vilevile, limevunja shartizuizi lenye nguvu linalozuia mofu katika umboghafi isidondoshwe katika umbotokeo, katika umbo hili mofu ya utendea imedondoshwa. Pamoja na hayo, umbo hili halijavunja shartizuizi hafifu linalohitajia mofu katika umbotokeo zitegemee mofu katika umboghafi.

Katika orodha ya maumbotokeo hayo, umbotokeo (c) ndio limefikia upeo wa ukubalifu kwa kutokuvunja mashartizuizi yote katika seti ya MASHA-ZU.

Umbotokeo (d) halijashinda kutokana na kukiuka shartizuizi lenye nguvu linalohitajia kila mofu katika umboghafi itokee katika umbotokeo na kuzuia udondoshaji wa mofu. Katika umbo hili mofu ya urejeshi {-ye} imedondoshwa na kuambikwa mofu {-wo} ya urejeshi hivyo kubadili maana ya kitenzi katika umboghafi. Hata hivyo umbo hili halijavunja shartizuizi lenye nguvu kabisa kwa kuwa na mfuatano wa mofu unaokubalika katika muktadha huu.

#### 4.3.2.7 MASHA-ZU ya mofu ya ufanyikaji sana na utendwa

Data za utafiti huu vilevile zinaeleza kuwa, katika mazingira ya mfuatano wa mofu kwenye umbo la kitenzi ili kuunda vitenzi mbalimbali vya lugha ya Kisambaa, mofu nyambulishi ya ufanyikaji sana inapoambatana na mofu ya mofimu ya utendwa, mofu ya ufanyikaji sana ndiyo inayotangulia mofu ya utendwa. Maumbo ya vitenzi yenye mofu hizi yanaoneshwa katika jedwali Na. 4.50.

**Jedwali 4.50: Mofu ya Ufanyikaji sana na Utendwa**

| Kitenzi | Umbo la Kitenzi |
|---|---|
| doseshwa (fuatwa sana) | dos-esh-w-a<br>Mz-Fnysn-Tdw- $M_i$ |
| shengeshwa (katwa sana) | sheng-esh-w-a<br>Mz-Fnysn-Tdw- $M_i$ |
| hituizwa (geuzwa sana) | hitu-iz-w-a<br>Mz-Fnysn-Tdw- $M_i$ |
| hungizwa (pepewa sana) | hung-iz-w-a<br>Mz-Fnysn-Tdw- $M_i$ |
| hakishwa (ogeshwa sana) | hak-ish-w-a<br>Mz-Fnysn-Tdw- $M_i$ |
| shungishwa (fungwa sana) | shung-ish-w-a<br>Mz-Fnysn-Tdw- $M_i$ |

**Chanzo:** Data za Uwandani

Data zinazoonekana katika jedwali namba 4.50 zinadhihirisha kuwa katika lugha ya Kisambaa umbo la kitenzi kinachobeba mofu nyambulishi ya ufanyikaji sana na mofu ya utendwa, mofu ya utendwa inafuatia mofu ya ufanyikaji sana wa jambo fulani. Mpangilio wa mashartizuizi ya lugha ya Kisambaa yanayoongoza unyambulishaji wa mofu katika vitenzi vyenye tabia hii ni haya hapa chini.

Mashartizuizi: **T({#Fnysn}-{Tdw}) »FIKI UKO»TEGE»SHABI**

**T({#Fnysn}-{Tdw})** shartizuizi hili linahitajia kwamba katika mfuatano wa mofu nyambulishi ya mofu ya ufanyikaji sana na mofu ya utendwa, mofu ya ufanyikaji sana itangulie na ifuatie mofu ya utendwa kwenye kitenzi cha Kisambaa.

**Jedwali 4.51: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: shengeshwa 'katwa sana'**

| | sheng-esh-w-a<br>Mz-Fnysn-Tdw- $M_i$ | **SETI YA MASHA-ZU** | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Maumbotokeo** | T({#Fnysn}-{Tdea}) | FIKI UKO | TEGE | SHABI |
| a | sheng-esh-an-a<br>Mz-Fnysn-Tdna- $M_i$ | !* | ** | * | * |
| b | sheng-esh-e-w-a<br>Mz-Fnysn-Tdea-Tdw- $M_i$ | !* | ** | * | * |
| d | ☞sheng-esh-w-a<br>Mz-Fnysn-Tdw- $M_i$ | | | | |

**Chanzo**: Data za Uwandani

Katika Jedwali 4.51 hapo juu, tunaona orodha ya maumbotokeo (a) hadi (c). Umbotokeo (a) halijashinda kwa kuvunja shartizuizi lenye nguvu kabisa ambapo mofu ya utendwa haijaambikwa na badala yake imeambikwa mofu ya kutendana. Umbo hili pia limekiuka mashartizuizi mengine katika seti ya MASHA-ZU.

Umbotokeo (b) vilevile limekiuka shartizuizi lenye nguvu kabisa kwa kuambika mofu ya utendea baada ya mofu ya ufanyikaji sana. Sharti hili linahitajia mofu ya ufanyikaji sana ifuatiwe na mofu ya kutendwa. Kwa hiyo, umbo hili halijafikia upeo wa ukubalifu. Umbotokeo (c) ndio limekidhi vigezo vya mashartizuizi yote katika seti ya MASHA-ZU hivyo kuwa umbo lililofikia upeo wa ukubalifu katika sarufi ya Kisambaa.

#### 4.3.2.8 MASHAZU ya mfuatano wa mofu ya utendeshi na kutendana

Data zinaonesha kuwa kitenzi cha Kisambaa kinaweza kuwa na mfuatano wa mofu ya utendeshi na mofu ya kutendana katika maumbo yake. Katika mfuatano wa mofu nyambulishi hizo mofu ya utendeshi ndiyo inaitangulia mofu ya kutendana. Maumbo ya vitenzi yenye mofu hizo yanabainishwa katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 4.52: Mofu ya Utendeshi na Utendwa**

| Kitenzi | Umbo la Kitenzi |
|---|---|
| uzana ‘rudishana’ | u- z- an- a<br>Mz-Tdsh-Tdna-$M_i$ |
| kinyana ‘angushana’ | kin- y- an- a<br>Mz-Tdsh-Tdna-$M_i$ |
| hozana ‘pozana’ | ho- z- an –a<br>Mz-Tdsh-Tdna-$M_i$ |
| ghooshana ‘simamishana’ | ghoo-sh-an-a<br>Mz-Tdsh-Tdna-$M_i$ |
| ghuzana ‘nunuzana’ | ghu-z-an-a<br>Mz-Tdsh-Tdna-$M_i$ |
| tibuzana ‘choshana’ | tibu-z-an-a<br>Mz-Tdsh-Tdna-$M_i$ |

**Chanzo:** Data za Uwandani

Data hizo katika jedwali Na. 4.52 zinabainisha mfuatano wa mofu nyambulishi ya utendeshi na kutendana zinavyonyambulishwa katika kitenzi cha Kisambaa. Katika maumbo ya vitenzi hivyo mofu ya utendeshi ndio imetangulia na kufuatiwa na mofu ya kutendana. MASHA-ZU ya mfuatano huu yanaoneshwa kama ifuatavyo.

Mashartizuizi: **T({#Tdsh}-{Tdna}) »FIKI UKO»TEGE»SHABI**

**T({#Tdsh}-{Tdna})** shartizuizi hili linahitajia kwamba katika mfuatano wa mofu nyambulishi ya mofu ya utendeshi na mofu ya kutendana, mofu ya utendeshi itangulie na ifuatie mofu ya kutendana kwenye kitenzi cha Kisambaa.

**Jedwali 4.53: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: kinyana 'angushana'**

| | kin- y- an- a<br>Mz-Tdsh-Tdna-$M_i$ | **SETI YA MASHA-ZU** | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Maumbotokeo** | T({#Tdsh}-{Tdna}) | FIKI UKO | TEGE | SHABI |
| a | kin-y-iz-an-a<br>Mz-Tdsh-Tdw-Tdna-$M_i$ | !* | ** | * | * |
| b | kin-an-y-a<br>Mz- Tdna- Tdsh-$M_i$ | !* | ** | * | * |
| c | ☞kin-y-an-a<br>Mz-Tdsh-Tdna-$M_i$ | | | | |

**Chanzo**: Data za Uwandani

Katika jedwali Na. 4.53, umbotokeo (a) limekuiuka shartizuizi lenye nguvu kabisa kwa mofu ya utendeshi kufuatiwa na mofu ya utendwa kisha mofu ya kutendana ambapo sharti hili linahitajia mofu ya utendeshi ifuatiwe na mofu ya kutendana. Umbo hili pia limevunja mashartizuizi mengine katika seti ya MASHA-ZU. Hivyo halijafikia upeo wa ukubalifu. Umbotokeo (b) nalo limevunja shartizuizi lenye nguvu kabisa kwa mofu ya kutendana kuitangulia mofu ya utendeshi. Umbo hili vilevile limevunja mashartizuizi mengine hivyo halijafikia upeo wa ukubalifu. Umbotokeo (c) ndio limefikia upeo wa ukubalifu kwa kukidhi vigezo vya mashartizuizi yote katika seti ya MASHA-ZU ya mfuatano wa mofu ya utendeshi na kutendana katika lugha ya Kisambaa.

#### 4.3.2.9 MASHA-ZU ya mfuatano wa mofu ya utendeshi, utendea na kutendana

Kama alivyobainisha Kaoneka (2009), kitenzi cha Kisambaa kinaruhusu mfuatano mofu nyambulishi tatu. Hata hivyo, mfuatano huo unaongozwa na vigezo vya mashartizuizi ya lugha ya Kisambaa ili maumbo ya vitenzi hivyo yakubalike katika sarufi ya Kisambaa. Katika mfuatano wa mofu hizo mofu ya utendeshi ndio inatangulia, ikifuatia mofu ya utendea na kutendana. Mfuatano ambao hautafuata utaratibu huo wa mofu ya utendeshi kutangulia haukubaliki katika lugha hii.

**Jedwali 4.54: Mofu ya Utendeshi, Utendea  na Kutendana**

| **Kitenzi** | **Umbo la Kitenzi** |
|---|---|
| uziana ‘rudishiana’ | u- z- i-an- a<br>Mz-Tdsh-Tdea-Tdna-$M_i$ |
| kinyiana ‘angushiana’ | kin- y- i- an- a<br>Mz-Tdsh-Tdea-Tdna-$M_i$ |
| hozeana ‘pozeana’ | ho- z- e-an –a<br>Mz-Tdsh-Tdea-Tdna-$M_i$ |
| ghoosheana ‘simamishiana’ | ghoo-sh-e - an-a<br>Mz-Tdsh- Tdea-Tdna-$M_i$ |

**Chanzo:** Data za Uwandani

Hivyo mofu ya utendeshi ndiyo inayoruhusu kufuatiwa na mofu nyambulishi ya utendea na kutendana. Vitenzi vya Kisambaa vyenye maumbo hayo vinaoneshwa katika Jedwali 4.54. Katika data hizo, maumbo ya vitenzi yanabainisha kuwa mofu ya utendeshi inatungulia baada ya mzizi na kufuatiwa na mofu ya utendea kisha kufuatia mofu ya kutendana. Mashartizuizi yanayoongoza mfuatano huu wa mofu yanabainishwa na kufafanuliwa hapa chini.

Mashartizuizi: **T({#Tdsh}-{Tdea}-{Tdna}) »FIKI UKO»TEGE»SHABI**

**T({#Tdsh}-{Tdea}-{Tdna})** shartizuizi hili linahitajia kwamba katika mfuatano wa mofu nyambulishi ya utendeshi, mofu ya kutendea na mofu ya kutendana, mofu ya utendeshi izitangulie mofu nyingine ikifuatiwa na mofu ya utendea kisha mofu ya

kutendana. Mfuatano huu wa mofu ndio unaozalisha maumbo ya vitenzi yaliyofikia upeo wa ukubalifu katika sarufi ya Kisambaa. Seti ya mashartizuizi kulingana na unguvu wa vigezo vya MASHA-ZU hayo unaoneshwa katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 4.55: Seti ya MASHA-ZU Umboghafi: hozeana 'pozeana'**

| | ho- z- e-an –a<br>Mz-Tdsh-Tdea-Tdna-$M_i$ | **SETI YA MASHA-ZU** | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Maumbotokeo** | T({#Tdsh}-{Tdea}-{Tdna}) | FIKI UKO | TEGE | SHABI |
| a | ho-z-an-i-a<br>Mz-Tdsh- Tdna-Tdea- $M_i$ | !* | ** | * | * |
| b | ho-z-an-a<br>Mz-Tdsh-Tdna-$M_i$ | !* | ** | * | * |
| c | ☞ho-z-e-an-a<br>Mz-Tdsh-Tdea-Tdna-$M_i$ | | | | |

**Chanzo**: Data za Uwandani

Katika jedwali 4.55 hapo juu, maumbotokoe yaliyozalishwa (a) hadi (c) yanashindana katika kufikia vigezo vya mashartizuizi katika seti ya MASHA-ZU. Umbotokeo (a) halijashinda kwa sababu limevunja shartizuizi lenye nguvu kabisa ambapo mofu ya utendeshi imefuatiwa na mofu ya kutendana badala ya mofu ya utendea. Vilevile limevunja mashartizuizi mengine yote katika seti ya MASHA-ZU. Umbotokeo (b) pia halijashinda kwani limevunja shartizuizi lenye nguvu kabisa kwa kuwa mofu ya utendeshi katika umbo hili haijafuatiwa na mofu ya utendea. Pamoja na hayo, umbo hili limekiuka mashartizuizi mengine yote. Umbotokeo (c) ndio limeshinda kwa kukidhi vigezo vya mashartizuizi katika seti ya MASHA-ZU. Kwa hiyo umbo hili limefikia upeo wa ukubalifu katika sarufi ya lugha ya Kisambaa.

Pamoja na hayo, katika ufafanuzi wa Kaoneka (2009) kwenye mfuatano wa mofu nyambulishi katika kitenzi cha Kisambaa, hakuna nadharia moja inayoweza kukidhi ufafanuzi wa tabia za vitenzi. Hata hivyo, kwa mujibu wa utafiti huu nadharia ya Umbo Upeo inaweza kukidhi ufafanuzi wa tabia za vitenzi ambao unafanywa kwa kuzingatia mashartizuizi ya lugha inayohusika. Ni dhahiri kuwa nadharia hii inaweza kuwa toshelevu katika kueleza tabia za vitenzi vya Kisambaa pale vinapoambishwa na kunyambulishwa kwa mofu mbalimbali. Mashartizuizi ni ya kimajumui na yanapangwa kimsonge.

Upangiliaji wa MASHA-ZU ndio unaoitofautisha lugha moja na nyingine. Katika mpangilio huo yanabainishwa MASHA-ZU yenye nguvu na yale ambayo ni hafifu kulingana na sarufi ya lugha inayohusika. Aidha, mashartizuizi yaliyojitokeza katika uundaji wa kitenzi cha Kisambaa chenye maumbo mbalimbali kwa njia ya uambishaji na unyambulishaji yanashabihiana na mashartizuizi katika lugha nyingine za Kibantu. Mathalani katika lugha ya Kikinga, mofu nyambulishi ya utendwa inapofuatana na utendea ni sharti mofu ya utendwa itanguliwe na utendea (Gawasike, 2011), hii pia imejitokeza katika kitenzi cha Kisambaa.

Hata hivyo, lugha hizi zinatofautiana katika mfuatano wa mofu nyambulishi nyingine. Mathalani katika Kikinga mofu nyambulishi ya utendea inapofuatana na mofu nyambulishi ya utendeshi, mofu ya utendea lazima itokee kwanza ndipo ifuate mofu ya utendeshi (Gawasike, 2011). Tabia hii ya vitenzi vya Kikinga ni tofauti na vitenzi vya Kisambaa kwani kutokana na matokeo ya utafiti huu, kuna shartizuizi linalohitajia mofu ya utendeshi itangulie mofu ya utendea. Hata hivyo, hilo ni dokezo tu la namna maumbo ya vitenzi katika uambikaji wa mofu yanavyotofautiana

na kufanana katika lugha za Kibantu kwani utafiti huu haujalenga kulinganisha namna mofu zinavyoathiriana wakati wa uambishaji na unyambulishaji katika lugha za Kibantu. Utafiti huu umelenga kufafanua kuathiriana kwa mofu pale zinapokaa pamoja kuunda kitenzi katika lugha ya Kisambaa kwa kuzingatia na kudhihirisha mashartizuizi ya lugha ya Kisambaa yanayotawala utokeaji wa mofu katika umbo la kitenzi.

## 4.4. Muhtasari wa sura

Sura hii imeonesha uchambuzi na uwasilishaji wa data ya utafiti huu. Uchambuzi na uwasilishaji huo umefanywa kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Maswali ya utafiti yamejibiwa katika data iliyochanganuliwa kwa njia ya majedwali. Malengo na maswali ya utafiti huu yaliyojibiwa ni pamoja na ubainishaji wa mofu ambishi na mofu nyambulishi pamoja na mofimu zake katika kitenzi cha Kisambaa, kuchanganua kuathiriana kwa mofu zinapokaa pamoja kuunda kitenzi pamoja na kudhihirisha mashartizuizi yanayotawala uambishaji na unyambulishaji wa mofu katika kitenzi cha Kisambaa.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI WA MJADALA, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inahusu muhtasari wa mjadala, hitimisho na mapendekezo ambapo lengo lake ni kuonesha kwa muhtasari matokeo ya utafiti pamoja na mapendekezo ya tafiti nyingine zinazohitajika katika lugha ya Kisambaa. Aidha, sura hii imegawanyika katika sehemu tatu za muhtasari wa utafiti, hitimisho na mapendekezo juu ya masuala mengine yanayohusiana na utafiti huu yanayohitaji kutafitiwa ambayo ni fursa za kiutafiti kwa watifiti wengine wa lugha na isimu.

## 5.2 Muhtasari wa mjadala wa utafiti

Utafiti huu ulilenga maumbo ya kitenzi cha Kisambaa kwa kuchunguza na kuchambua mofu zinavyoathiriana kimofolojia au kimofofonolojia katika uundaji wa kitenzi. Lengo kuu lilikuwa ni kuchunguza namna mofu zinavyoathiriana kimofolojia au kimofofonolojia zinapoambishwa na kunyambulishwa ili kuunda kitenzi na kudhihirisha mashartizuizi yanayotawala uambikaji wa mofu katika kitenzi cha Kisambaa. Malengo mahususi yalikuwa kama ifuatavyo:

a) Kubainisha mofu ambishi na nyambulishi pamoja na mofimu zake zinazounda kitenzi cha Kisambaa.

b) Kuchanganua namna mofu zinavyoathiriana kimofolojia au kimofofonolojia zinapokaa pamoja wakati wa kuunda kitenzi cha Kisambaa.

c) Kudhihirisha mashartizuizi yanayotawala uambikaji wa mofu katika kitenzi cha Kisambaa.

Maswali ya utafiti yaliyopaswa kujibiwa ni haya yafuatayo:

i. Ni maumbo gani ya mofu ambishi na mofu nyambulishi pamoja na mofimu zake yanayounda kitenzi cha lugha ya Kisambaa?
ii. Mofu zinaathirianaje zinapokaa pamoja wakati wa kuunda kitenzi katika lugha ya Kisambaa?
iii. Ni mashartizuizi gani yanayotawala uambikaji wa mofu katika kitenzi cha Kisambaa?

Maswali hayo yamejibiwa kutokana na data zilizokusanywa uwandani na kuchambuliwa kwa mwongozo wa nadharia ya Umbo Upeo. Kwa kutumia nadharia hiyo uainishaji wa mofu na namna mofu hizo zinavyoathiriana umefanywa kwa kuzingatia mashartizuizi yanayotawala mfuatano na mpangilio wa mofu katika kitenzi cha lugha ya Kisambaa. Mofu ambishi na mofimu zake zilizobainishwa na matokeo ya utafiti huu ni pamoja na mofu za mofimu ya ukanushi {ka-, ku-, ke-, si-, se-, -she-}; mofu za mofimu ya nafsi {ni-, u-,wa-, a-, ti-, mwa-, mu-, m-, wa-}; mofu za mofimu ya njeo {-a-,-ta-,-i-, -za-, -Ø-, -a-, ne-, nee-}; mofu za mofimu ya mtendwa {-ni-, -ku-, -ti-,-mi-,-m-,-mu-,-wa-,-ha-,-chi-, -vi-,-u-,-ya-}; mofu ya mofimu ya masharti {-ki-} na mofu ya mofimu ya ujirejezi {-ki-}.

Vilevile, mofu nyambulishi na mofimu zake zilizobainishwa katika utafiti huu ni pamoja na;

i) Mofu za mofimu ya utendea {-e-} na {-i-}.

ii) Mofu za mofimu ya utendwa {-w-} , {-lw-} na {-ighw-}.

iii) Mofu za mofimu ya utendeka {-ek-} na {-ik-}.

iv) Mofu za mofimu ya utendeshi {-esh-,-ish-/, {-ez-}, {-iz-}, {-s-}, {-y-} na {-z-}.

v) Mofu za mofimu ya ufanyaji sana {-ish-} na {-esh-}.

vi) Mofu ya mofimu ya kutendana {-an-}.

vii) Mofu za mofimu ya ubadilifu {-u-} na {-o-}.

viii) Mofu za mofimu ya urejeshi {-ye-} na {-wo-}.

Pamoja na hayo, matokeo ya utafiti huu yamebainisha namna mofu zinavyoathiriana kimofolojia au kimofofonolojia pale zinapokaa pamoja kuunda vitenzi mbalimbali vya Kisambaa. Kuathiriana huko ni katika maumbo ya mofu kwenye umbo la kitenzi. Katika kuathiriana huko imebainika kuwa, mofu ambishi na nyambulishi zinapoambikwa katika mzizi zina uhusiano na ushikamano ili kupata kitenzi kinachokubalika katika lugha ya Kisambaa. Kutokana na mahusiano hayo ya kushikamana kwa mofu ndipo zinapoathiriana kimofolojia au kimofofonolojia ili kuunda kitenzi chenye umbo linalokubalika katika lugha ya Kisambaa. Kuathiriana kwa mofu zinapokaa pamoja kuunda kitenzi cha Kisambaa kumedhihirika kutokana na mashartizuizi yanayotawala uambikaji wa mofu katika Kisambaa ambayo yamefafanuliwa pia. Hivyo, mofu ambishi na mofu nyambulishi katika kitenzi cha Kisambaa zinaathiriana katika muundo ufuatao.

Kuathiriana kwa mofu ambishi na mofu nyambulishi kimofolojia

i. Kudondoshwa kwa mofu ya nafsi ya kwanza umoja {-ni-}, ya pili umoja {-u-} na ya tatu umoja {-a-} katika vitenzi vyenye mofu ya ukanushi.
ii. Kudondoshwa kwa mofu njeo ya wakati uliopo {-a-/-ta-} katika vitenzi kanushi.
iii. Katika vitenzi kanushi katika wakati uliopita timilifu, mofu ya njeo {-i-} inadondoshwa na kutokea katika umbo {-e-}, {-iye-} au {-ize-} kama mofu

ishilizi.

iv. Katika kitenzi yakinishi, mofu ya mofimu ya nafsi hubadili nafasi ya utokeaji inapoambishwa pamoja na mofu ya mofimu ya njeo ya wakati ujao {-ne-/-nee-}. Mofu ya njeo ndio inatangulia na kufuatiwa na mofu ya nafsi.

v. Katika kitenzi kanushi, mofu ya masharti inaambatana na mofu ya ukanushi {-she}tu na si mofu nyingine za ukanushi kama {-ka-/-ke-/-ku-}.

vi. Katika kitenzi kanushi chenye mofu ya njeo ya wakati uliopita, mofu ya masharti {-ki-} haiambatani na mofu ya ukanushi {-she-}.

vii. Mofu ya utendea kuathiri mofu ya utendwa pale inapoambatana nayo katika kitenzi. Mofu ya utendea inafuatana na mofu {-w-} pekee na si mofu nyingine za utendwa {-ighw-} na {-lw-}.

viii. Mofuya utendeshi kutangulia mofu ya utendea tofauti na mofu nyambulishi nyingine zinaponyambulishwa pamoja na mofu ya utendea ambapo mofu ya utendea inazitangulia mofu hizo.

ix. Mofu ya urejeshi kuathiri mofu ishilizi {-a} kwa kuidondosha na kuchukua nafasi yake.

x. Mofu ya urejeshi kuathiri mofu ya njeo ya wakati uliopita kwa kubadili nafasi ya utokeaji katika kitenzi ambapo inatokea baada ya mzizi wa kitenzi badala ya kabla ya mzizi.

Kuathiriana kwa mofu ambishi na mofu nyambulishi kimofofonolojia

i. Mofu ishilizi {-a} kubadilika kuwa {-e-}, {-iye-} au {–ize-} katika vitenzi yakinishi vyenye mofu ya njeo ya wakati uliopita timilifu {-i-}.

ii. Mofu ya urejeshi kubadili umbo la mofu ya njeo ya wakati uliopita kuwa {-iye-} na inatokea baada ya mzizi wa kitenzi.
iii. Mofu ya urejeshi inapoafuatana na mofu ya utendwa, mofu ya utendwa inaathiri mofu ya njeo {-iye-} kwa kubadili umbo lake kuwa {-e-}.
iv. Katika mfuatano wa mofu ya urejeshi na mofu ya utendea, mofu ya utendea inaathiri mofu ya njeo wakati uliopita {-iye-} kwa kubadili umbo lake kuwa {-e-}.

Kutokana na kuathiriana huko kwa mofu katika vitenzi mbalimbali vya Kisambaa pale mofu ambishi na nyambulishi zinapoambikwa katika vitenzi hivyo, kuna mashartzizuizi katika lugha hii yanayoongoza uambikwaji huo wa mofu. Mashartizuizi hayo ni mashartizuizi ya utangamano na mashartizuizi ya uziada.

Mashartizuizi ya utangamano ni haya yafuatayo:

**a) FIKI UKO** (Fikia Ukomo wa Utangamano wa sifa za kimofolojia): Shartizuizi hili katika uchanganuzi wa mfuatano wa mofu zinazounda kitenzi cha Kisambaa na namna zinavyoathiriana linahitajia kwamba, vitenzi vinavyozalishwa viwe na mofu zenye utangamano na mofu zilizomo katika maumboghafi. Kwahiyo, Shartizuizi hili linazuia udondoshaji wa mofu yoyote iliyomo katika umboghafi.

**b) TEGE** (Tegemea sifa za kimofolojia): Shartizuizi hili katika uambikaji wa mofu na namna zinavyoathiriana linahitajia kwamba, mofu zilizomo katika umbotokeo zitegemee zile zilizomo katika umboghafi. Shartizuizi hili linazuia uchopezi wa mofu katika umbotokeo tofauti na zile zilizomo katika umboghafi.

c) **SHABI** (Shabihiana mofu): Shartizuizi linahitajia kwamba, sifa za kimofolojia za mofu katika umbotokeo zishabihiane na sifa za kimofolojia za mofu katika umboghafi.

Mashartizuizi ya uziada ambapo maumbo ya vitenzi ili kuunda vitenzi vinavyokubalika yalihitaji mabadiliko mbalimbali. Mashartizuizi hayo ni:

a. $\mathbf{T^{yknsh}}$**{# Nj$_{jao}$-}- {Nfs-}** : Shartizuizi hili linatuambia kuwa katika kitenzi yakinishi chenye mofu ya njeo ya wakati ujao, mofu ya njeo inatangulia ikifuatiwa na mofu ya nafsi.

b. $\mathbf{T^{Knsh}}$ **{ØNfs$_{1U}$-}:** Shartizuizi hili linatuambia kuwa katika kitenzi chenye mofu ya ukanushi, mofu ya nafsi ya kwanza umoja inadondoshwa.

c. Shartizuizi $\mathbf{T^{Knsh}}$ **{ØNfs$_{2U}$-}** ndio lenye nguvu kabisa linalohitaji kudondoshwa kwa mofu ya nafsi ya pili umoja.

d. $\mathbf{T^{Knsh}}$ **{ØNfs$_{2U}$-}** ndio shartizuizi lenye nguvu kabisa ambalo linahitaji kudondoshwa kwa mofu ya nafsi.

e. $\mathbf{T^{yknsh}}$ **Nj$_{pita}${-i-} {M$_i$(e, iye-ize}**: Shartizuizi hili linatuambia kwamba katika umbo la kitenzi yakinishi chenye mofu ya njeo ya wakati uliopita {-i-}, mofu ishilizi itakuwa {-e}, {-iye} au {-ize}.

f. $\mathbf{T^{Knsh}}$ **{ØNj$_{po}$-}** sharti hili linahitajia kwamba katika kitenzi chenye mofu ya ukanushi mofu ya njeo ya wakati uliopo idondoshwe.

g. $\mathbf{T^{Knsh}}$ **{ØNj$_{pita}$-} {-M$_i$(Nj$_{pita}$)}** shartizuizi hili linahitajia kwamba katika vitenzi vyenye mofu ya ukanushi, mofu ya njeo ya wakati uliopita idondoshwe, pia katika mofu ishilizi ndipo mofu hiyo ya njeo ya wakati uliopita inajitokeza.

h. **$T^{Knsh}$ {ØNj$_{jao}$-}** shartizuizi hili linahitajia kwamba mofu ya njeo ya wakati ujao idondoshwe katika kitenzi chenye ukanushi.

i. **$T^{Yknsh}$ {-Shrt}-{ØNj-}** shartizuizi hili linahitajia kwamba ili kupata umbo la kitenzi yakinishi chenye mofu ya masharti basi mofu ya njeo isiambatane na mofu ya masharti.

j. **$T^{Knsh}$ {-Shrt}-{Knsh$_{she}$-}** shartizuizi hili katika lugha ya Kisambaa linahitaji kwamba, katika kitenzi kanushi mofu ya masharti ifuatiwe na mofu ya ukanushi {-she-}.

k. **$T^{Knsh}${#Knsh$_{ka,ke,si,ku}$}-{-Jrjz}-{Nj$_{pita}$}** shartizuizi hili linatuambia kuwa katika vitenzi kanushi, mofu ya ujirejezi inatanguliwa na mofu ya ukanushi {ka-, ke-, si-, au ku} ikifuatiwa na mofu ya njeo ya wakati uliopita.

l. **T({#Tdea}-{-Tdw$_{w}$})** shartizuizi hili katika mfuatano wa mofu nyambulishi ya utendea na utendwa linatuambia kuwa, katika vitenzi vya Kisambaa vyenye tabia hii, mofu ya utendea itangulie ikifuatiwa na mofu ya utendwa yenye umbo {-w-}.

m. **T({#Sbsh}{-Tdea})** shartizuizi hili linahitaji kwamba katika kitenzi cha Kisambaa mofu ya usababishi itangulie mofu ya utendea.

n. **T({#Nfs-Mz}{-Nj$_{pita}$}{-Rjshμ})** shartizuizi hili linatuambia kwamba ili upate kitenzi cha Kisambaa chenye mofu ya urejeshi, basi katika umbo la kitenzi itangulie mofu ya nafsi kabla ya mzizi wa kitenzi, iwepo mofu ya njeo ya wakati uliopita na mofu ya urejeshi iwe mwishoni mwa kitenzi.

o. **T({#Nfs-Mz}{-Tdw}{-Nj$_e$}{-Rjshµ})** shartizuizi hili linatuambia kwamba katika kitenzi chenye mofu ya utendwa na urejeshi, itangulie mofu ya nafsi kabla ya mzizi, ifuatie mofu ya utendwa na mofu ya njeo {-e-} ambapo mofu ya urejeshi itatokea mwishoni mwa kitenzi.

p. **T({#Nfs-Mz}{-Tdea}{-Nj$_e$}{-Rjshµ})** shartizuizi hili linatuambia kwamba katika kitenzi chenye mofu ya utendea na urejeshi, itangulie mofu ya nafsi kabla ya mzizi, ifuatie mofu ya utendea na mofu ya njeo {-e-} ambapo mofu ya urejeshi itatokea mwishoni mwa kitenzi.

Kwa hiyo, utafiti huu umeonesha upekee wa lugha ya Kisambaa katika maumbo ya vitenzi na namna mofu zinazounda vitenzi hivyo zinavyojitokeza kimaumbo. Mashartizuizi ya lugha ya Kisambaa yaliyodhihirishwa na utafiti huu wa maumbo ya vitenzi ndiyo yanayoitofautisha lugha ya Kisambaa na lugha nyinginezo. Hii ni kutokana na mpangilio wa mashartizuizi hayo katika kueleza mfuatano wa mofu zinazoambishwa na kunyambulishwa ili kuunda vitenzi vyenye maumbo mbalimbali yanayokubalika katika sarufi ya lugha ya Kisambaa.

## 5.3 Hitimisho

Kutokana na malengo yaliyokusudiwa, utafiti huu umetoa matokeo ambayo yanaibainisha sarufi ya lugha ya Kisambaa katika upande wa mofolojia ya kitenzi. Kitenzi katika lugha ya Kisambaa kimedhihirika kuundwa na mofu mbalimbali kama ilivyokusudiwa katika lengo la kwanza. Mofu zinazounda kitenzi ni mofu ambishi na mofu nyambulishi ambazo ili kuunda vitenzi vyenye maumbo mbalimbali zinaambikwa katika mzizi wa kitenzi cha Kisambaa. Mofu hizo zinadhihirika

kiumbo pale zinapotamkwa na zinapoandikwa hali ya kuwa zina maana ambayo ni dhahania na ipo akilini mwa mzungumzaji ikiitwa mofimu.

Katika lengo la pili utafiti huu ulikusudia kuchanganua namna mofu zinavyoathiriana kimofolojia au kimofofonolojia katika umbo la kitenzi. Matokeo yaliyopatikana yamesadifu kuwa mofu zinazounda kitenzi katika lugha ya Kisambaa zinaweza kuathiriana pale zinapokaa pamoja kuunda vitenzi vyenye maumbo tofauti tofauti. Kuathiriana kwa mofu hizo kunatokana na kuwepo kwa mashartizuizi mbalimbali yanayotawala mpangilio na mfuatano wa mofu zinazounda vitenzi pale zinapoambikwa katika mzizi wa kitenzi. Hivyo, mashartizuizi hayo yanabainisha kuwa lugha ya Kisambaa kwa upekee wa sarufi yake ina sheria, kanuni na taratibu zinazoongoza uundwaji wa maneno ambayo yanakubalika katika lugha hii.

Pamoja na hayo, ubainishaji na upangiliaji wa mashartizuizi yanayoongoza uambishaji na unyambulishaji wa mofu katika kitenzi cha Kisambaa ndio unaotimiza lengo la tatu. Katika utafiti huu lengo la tatu limekusudia kudhihirisha mashartizuizi yanayotawala uambikaji wa mofu katika kitenzi cha Kisambaa. Kwa hiyo malengo ya utafiti huu yamefikiwa kikamilifu na matokeo ya utafiti yameongeza maarifa katika ufahamu wa sarufi ya lugha ya Kisambaa hasa kwa upande wa mofolojia ya vitenzi.

Aidha, nadharia ya Umbo Upeo ambayo ndio imetumika katika uchambuzi wa data za utafiti huu imekuwa na mchango mkubwa kujibu maswali yaliyoongoza utafiti. Madhumuni ya mwanzo ya kuanzishwa kwa nadharia hii yalikuwa kushughulikia masuala ya kifonolojia, lakini baadaye kiunzi hiki kimetumiwa kushughulikia pia

masuala ya kimofolojia (Legendre 2000, Wunderlich 2001). Hivyo, uchambuzi na uchunguzi wa mofolojia ya vitenzi vya Kisambaa kwa namna mofu zinavyoathiriana wakati wa kuunda vitenzi kwa kutumia nadharia hii umefanikiwa. Uchunguzi wa namna mofu zinavyoathiriana katika umbo la kitenzi umefanyika kwa kuongozwa na Mashartizuizi yanayotawala uambikaji wa mofu katika sarufi ya lugha ya Kisambaa. Msingi wa MASHA-ZU ndio kiini cha nadharia hii. Katika utafiti huu maumbo ya vitenzi yametathminiwa kwa kutumia seti ya Mashartizuizi yaliyoweza kubainika katika data iliyopatikana katika utafiti. Mashartizuizi hayo yamebainishwa kwa kuchunguza tabia mbalimbali za vitenzi vya Kisambaa kwa namna mofu zinavyofuatana na kuathiriana katika umbo la kitenzi ili kuunda kitenzi kinachokubalika katika Kisambaa.

Katika seti ya MASHA-ZU yenye mashartizuizi yenye nguvu na yasiyo na nguvu ndipo tathmini ilipofanyika kwa kuangalia ni umbo lipi la kitenzi katika jumla ya maumbo shindani limevunja masharti kidogo, lipi limevunja mashartizuizi mengi na lipi limevunja yale ya chini kabisa yanayoweza kuvumilika. Mashartizuizi hayo ni MASHA-ZU ya uadilifu na MASHA-ZU ya uziada. MASHA-ZU ya uadilifu hujumuisha familia ya MASHA-ZU ya utangamano. Katika MASHA-ZU haya ya utangamano kuna MASHA-ZU yanayozuia udondoshaji wa mofu zilizomo katika umbo ghafi, MASHA-ZU ambayo yanazuia uchopekaji wa mofu katika umbotokeo na MASHA-ZU ambayo yanahitajia kwamba sifa za kimofolojia katika umbotokeo zishabihiane na zile zilizomo katika umboghafi. Pia MASHA-ZU ya uziada ni yale yanayoruhusu mabadiliko katika umboghafi ili kuyafanya maumbotokeo yakubalike katika sarufi ya lugha inayohusika. Mashartizuizi haya yamebainishwa katika utafiti

huu.

Hivyo, ubainishaji wa Mashartizuizi yanayotawala uambishaji na unyambulishaji wa mofu katika vitenzi vya Kisambaa, pamoja na upangiliaji wa MASHA-ZU ya uadilifu na uziada na kutathimini maumbo mbalimbali ya vitenzi kama maumboshindani ili kupata umbo linalokubalika katika sarufi ya Kisambaa, umekuwa mchango mkubwa wa nadharia ya Umbo Upeo katika utafiti huu.

## 5.4 Mapendekezo

Kama ilivyoelezwa tangu mwanzo, utafiti huu ulijikita katika kuchunguza na kuchanganua namna mofu zinavyoathiriana kimofolojia au kimofofonolojia wakati wa kuunda kitenzi katika lugha ya Kisambaa. Mofu ambishi na mofu nyambulishi ambazo zinaweza kuambikwa katika kitenzi cha Kisambaa zimebainishwa. Mofu hizo zimefafanuliwa namna zinavyoathiriana wakati zinapokaa pamoja kuunda vitenzi vyenye maumbo mbalimbali katika Kisambaa. Kuathiriana huko kwa mofu kumebainishwa kwa kudhihirisha mashartizuizi yanayotawala uambikaji wa mofu katika lugha hii.

Hata hivyo, tafiti nyingine katika maumbo ya vitenzi na namna mofu zinavyoweza kuathiriana kisemantiki na kisintaksia zinahitajika katika lugha ya Kisambaa. Tafiti hizo zitasaidia kwa kiasi kikubwa watafiti wengine kuifahamu sarufi ya lugha ya Kisambaa. Vilevile tafiti hizo katika lugha ya Kisambaa zitawapa nafasi watafiti wanaoshughulikia lugha za Kibantu kufanya tafiti linganishi na kuibua masuala mbalimbali yanayohusu sarufi ya lugha hizo za Kibantu.

Pamoja na hayo, katika lugha ya Kisambaa Besha (1985) amebainisha uwepo wa lahaja tatu za lugha ya Kisambaa, hata hivyo japo halikuwa lengo la utafiti huu lakini wakati wa ukusanyaji wa data mtafiti amebaini kuwa kuna haja ya kuzitafiti lahaja hizo kwa kina kujua kwamba ziko tatu au zaidi na ni tofauti zipi baina ya lahaja hizo zinazozitofautisha. Pamoja na hayo suala la toni katika lugha ya Kisambaa ni muhimu litafitiwe kwa kina na kubaini ni kategoria gani ya maneno ina sauti nyingi zenye toni ama toni ina athari gani katika uundwaji wa maneno.

Vilevile, katika upande wa mashartizuizi yanayoongoza mpangilio wa mofu ili kuunda maneno yenye maumbo na maana mbalimbali katika lugha, watafiti wengine wanaweza kufanya utafiti linganishi katika lugha za Kibantu. Utafiti huo utabainisha kufanana na kutofautiana kwa mpangilio na vigezo vya mashartizuizi hayo na hivyo kuongeza ufahamu katika sarufi ya lugha za Kibantu.

Kwa hiyo, kwa watafiti wengine ambao wanashughulikia uhifadhi wa sarufi za lugha kuna uhitaji wa kuziweka lugha za Kibantu katika maandishi hata kuwepo kwa kamusi za lugha hizo ili kuwasaidia watafiti wengine kukusanya data ambayo haijaathiriwa. Hii ni kutokana na kwamba kupita kwa wakati kunaleta mabadiliko katika matumizi ya lugha. Yawezekana lugha inazungumzwa sana na wenyeji lakini katika lugha hiyo kukatokea mabadiliko katika maneno na maumbo ya maneno. Hivyo ni muhimu kuhifadhi lugha za Kibantu katika maandishi ili uasili wa lugha hizo usipotee.

## MAREJEO

Akema, P. na Neelman, A. (1998). Optimal questions. *Natural Language and Linguistic Theory*, 16, 443-490.

Aronoff, M. (1976). *Word formation in generative grammar*. London: MIT Press.

Asiimwe, C. (2011). Unyambulishi wa vitenzi katika lugha ya Runyankore. (Tasnifu ya Uzamili ya M.A Kiswahili), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Dar es Salaam, Tanzania. 99pp.

Athumani, J.B. (2012). Lexicostatistical comparison of Kibondei, Kishambala and Kizigula languages. (Tasnifu ya Uzamili ya M.A Linguistics), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Babbier, E. R. (1998). *The practice of social science research*. Belmont, CA: Wardsworth Publishing Company.

Baker, M. (1985). The mirror principle and morphosyntactic explanation. *Linguistic Inquiry*, 16, 373-415.

Beath, T. (2003). Syntax. In Dereck Nurse & Gerald Philippson (eds). *The Bantu languages*, 127-142. London: Routledge.

Besha, R. M. (1985). A study of tense and aspect in Shambala. (Tasnifu ya Uzamivu), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam, Tanzania.

Besha, R. (1989). Mood in Bantu languages: An exemplification from Shambala. ICLAA Vol.5 *Studies in Tanzanian Languages*. Tokyo: Institute for the Study of Languages and Cultures of Asia and Africa. Dammann, E. 1968. Sprachliche Bemuehungen von Betheler Missionaren um das Schambala' in Ostafrikanische Studien 8.

Besha, R. M. (1993). *A classified vocabulary of the Shambala language with outline grammar*. Institute for the Study of Languages and Cultures of Asia and Africa (ILCAA).

Booji, G. (2007). *The grammar of words: An introduction to linguistic morphology*. New York: Oxford University Press.

Burns, R. (2000). *Introduction to research methods*. London: Longman, Frenchs Forest, NSW.

Castair- McCarthy, A. (2002). *An introduction to English morphology*. Edinburgh: Edinburgh University Press.

Charwi, Z. M. (2011). Unyambulishaji na dhana ya uelekezi katika lugha ya Kikuria. *Kioo cha Lugha*. Juz.11, uk 58-77. TATAKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Chomsky, N. na Halle, M. (1968). *The sound pattern of English*. New York: Harper and Row.

David, O. (1982). Tonal phenomena in Kishambala. *Studies in African Linguistics.* 13(2), 177-208.

Dekkers, J, J., Van der Leeuw, F. na Van de Weijer, J. (2000). *Optimality theory: phonology, syntax and acquisition*. England: Oxford University Press.

Dunham, M. (2002). *On the verbal system in Langi a Bantu language of Tanzania*. Universite de Paris:  LACITO-CNRS.

Enon, J. C. (1998). *Educational research, statistics and measurements*. Kampala: Makerere University.

Feierman, S. (1974). *The Shambaa kingdom: A history*. London: The University of Wisconsin Press.

Fouka, G. na Mantzorou, M. (2011). What are the major ethical issues in conducting research? Is there a conflict between the research ethics and the nature of nursing? *Health Science Journal*, 5, 3-14.

Field, A. (2005). Reliability analysis.. *Discovering Statistics using Spss. 2nd edition*, London: Sage.

Gambarage, J. (2011). Mkanganyiko wa dhana za mzizi, kiini na shina. *Kiswahili*, uk 12-24. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam..

Gawasike, A. (2011). Mfuatano wa mofimu nyambulishi katika vitenzi vya Kikinga. (Tasnifu ya Uzamili ya M.A Kiswahili), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam, Tanzania.

Gawasike, A. (2012). Dhana ya uambikaji katika Kiswahili. *Kioo cha Lugha*. Juz 10, uk 70 – 78. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TATAKI.

Grimshaw, J. (1997). The best clitic: Constraint conflict in morphosyntax. Haegeman, Liliane. *Elements of Grammar*. uk 169-196. Kluwer Academic Publishers.

Grimshaw, J. na Samek-Lodovici, V. (1998). Optimal subjects and subject universals. Barbosa, P. Fox, D. Hagstrom, P. McGinnis, M. and Pesetsky, D. (eds), *Is the Best Good Enough? Optimality and Competition in Syntax*, 193-219. Cambridge, Mass: MIT Press.

Guthrie, M. (1971). *Comparative Bantu: An Introduction to the comparative linguistics and prehistory of the Bantu languages, Vol 2*. Farnborough: Gregg Press.

Habibu, N. (2016). Muundo wa kirai kitenzi katika lugha ya Kisambaa. *Huria*

*Journal of the Open University of Tanzania*. 21, 40-59.

Hartman, R. (1972). *Dictionary of language and linguistics*. London: Applied Science Publisher.

Haspelmath, M na Sims, A. (2010). *Understanding morphology*. London: Hachette UK Company.

Hennink, M., Kaiser, B., na Marconi, V. (2017). Code saturation versus meaning saturation: How many interviews are enough? *Qualitative Health Research*, 27, 591-608.

Hockett, C. F. (1958). *A Course in modern linguistics*. New Delhi: Oxford & IBH Publishing Co.

Hyman, H. M. na Mchombo, S. (1992). Morphotactic constraints in the Chichewa verb stem. In Buszard-Welcher, L., Wee, L. and Weigel, W. (eds), *Proceedings of the Eighteenth Meeting of the Berkeley Linguistics Society, General Session and Parassession*, 350-363. Berkeley: Berkeley Linguistics Society.

Hyman, L. (2003). Suffix ordering in Bantu, A morphocentric approach. Geert Booij and Jaap van Marle (Eds), *Year book of morphology 2002*, 245281, Kluwer: Dordrecht.

Jill, J. F., Johnston, M., Robertson, C., Glidewell, L., Entwistle, V., Eccles, P. M. na Grimshaw, M. (2010). What is an adequate sample size? Operationalising data saturation for theory-based interview studies. *Psychology & Health,* 25(10), 1229-45.

Kaoneka, S. (2009). Verb extensions in Shambala: Their occurrence and co-

occurrence constraints. (Masters of Arts Linguistics), University of Dar es Salaam, Tanzania.

Katamba, F. (1993). *Morphology*. London: Macmillan Press Ltd.

Katushemererwe, F. (2013). Computational morphology and Bantu language learning: An implementation for Runyakitara. (PhD Thesis), University of Groningen, Netherlands.

Khamis, A. M. (2009), *Stadi za lugha ya Kiswahili: Sarufi 1*. Dar es Salaam: TUKI.

Kiango, J. G. (2000). *Bantu lexicography: A critical survey of the principles and process of constructing dictionary entries*. Tokyo: ILCAA.

Kihore, Y. M., Massamba, D. P. B. na Msanjila, Y. P. (2003). *Sarufi maumbo ya Kiswahili sanifu*. Dar es Salaam: TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kihore, Y. M. (2009). *Stadi za lugha ya Kiswahili: Sarufi II*. Dar es Salaam: TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kihore, Y. M. (2011). Majibu kwa makala: Mkanganyiko wa dhana za mzizi, kiini na shina yaliyoandikwa na Joash Gambarage. *Kiswahili*, uk 25-27. Dar es Salaama: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kothari, C. R. (2004). *Research methodology: Methods and techniques*. New Delhi: New Age International Publishers Ltd.

Legendre, G. (2000). Morphological and prosodic alignment of Bulgaria clitics. In: *Optimality Theory: phonology, syntax*. London: Oxford University Press.

Lieber, R. (2009). *Introducing morphology*. New York: Cambridge University Press.

Lightner, T. (1975). The role of derivational morphology in generative grammar. *Language* 5, 617-638.

Lockwood, D. G. (1993). *Morphological analysis and description: A realization*

*approach*. Tokyo: International Language Sciences Publishers.

Lodhi, Y. A. (2002). Verbal extensions in Bantu: The case of Swahili and Nyamwezi. *Afric & Asia*, No 2, 4-26. Department of Oriental and African Languages, Göteborg University.

Lusekelo, A. (2007). Tense and aspect systems in Kinyakyusa. (Tasnifu ya Uzamili ya M.A Linguistics), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam, Tanzania. 197pp.

Mack, N., Woodsong, C., Macqueen, M. K, Guest, G. na Namey, E. (2005). *Qualitative research methods: A data collector's field guide*. USA: Family Health International.

McCarthy, J. J na Cohn, A. (1998). Alignment and parallelism in Indonesian phonology. *Linguistics Department Faculty Publication Series*, 6, 53-137.

McCarthy, J. J. (2002). *A thematic guide to optimality theory*. Cambridge: Cambridge University Press.

McCarthy, J. J. (2007). What is optimality theory. *Linguistics Department Faculty Publication Series*, 98. Massachusettes: Amherst University of Massachusettes.

Maho, J. F. (2003). A Classification of the Bantu languages: an update of Guthrie's referential system. Nurse, D and Philippson, G. (eds), *The Bantu Languages*, p 639-651. London and New York: Routledge.

Massamba, D. P. B. (2004). *Kamusi ya isimu na falsafa ya lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D. P. B. (2009). *Misingi ya fonolojia*. Dar es Salaam: TATAKI.

Massamba, D. P. B. (2011). *Maendeleo katika nadharia ya fonolojia*. Dar es Salaam: TATAKI.

Massamba, D. P. B., Kihore, Y. M. na Hokororo, J. I. (1999). *Sarufi miundo ya Kiswahili sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.

Masebo, H. (2007). The verb extension in Chindali. (Tasnifu ya Uzamili ya M. A Linguistics), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. 189pp.

Mashauri, M. A. (2013). Matumizi ya nadharia ya umboupeo mawanda katika uchanganuzi wa silabi za Kiswahili. *Kiswahili*. Juz. 76, uk. 71-89. Dar es Salaam: TUKI.

Matei, A. K. (2008). *Darubini ya sarufi: Ufafanuzi kamili wa sarufi*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Mgullu, R. S. (1999). *Mtalaa wa isimu*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mkanganwi, K. G. (2002). Shona derivational morphology: An observation in search of a theory. Zambezia. Department of Linguistics, University of Zimbabwe. 174-190pp.

Mohammed, M. A. (2001). *Modern Swahili grammar*. Dar es Salaam: EAEP.

Monette, D. R., Sullivan, T. J. na DeJong, C.R. (2011). *Applied social research: Tools for the human services*. London: Brooks/Cole Cengage Learning.

Mpalanzi, L. (2010). An Analysis of Tense and Aspect Systems in Kihehe: A case of Affirmative and Negative Constructions. (Tasnifu ya Uzamili ya M.A Linguistics), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.

Mreta, A. Y. (1998). *An analysis of tense and aspect in Chasu: Their forms and meaning in the affimative constructions*. Hamburg: LIT.

Mukuthuria, M. (2010). Maadili ya utafiti. *Kiswahili*. Massamba, D. P. B (Mhariri),

Juz. 73, uk. 110- 121. Dar es Salaam: TATAKI.

Mushi, C. P. (2005). Verb derivation in Kibosho. (Tasnifu ya Uzamili ya M.A Linguistics) , Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.

Mutaka, N. M. na Tamanji, P. N. (2000). *Classification of African languages. An introduction to African linguistics*, 1–32. Munich: Lincom Europa.

Muzale, H. R. T. (1998). A Reconstruction of the Proto-Rutara tense/aspect systems. (PhD Thesis), Memorial University of Newfoundland. 347pp.

Mwashota, P. (2016). Ujitokezaji wa viambishi njeo na athari zake kifonolojia katika lugha za Kibantu: Mifano kutoka lugha ya Shimalila. *Kioo cha Lugha*. Juz. 14. Dar es Salaam: TATAKI.

Nida, E. A. (1952). *Morphology: The descriptive analysis of words*. Michigan: University of Michigan Press.

Ngonyani, D. (2003). *Chingoni grammar*. Muenchen: LINCOM, EUROPA.

Nkondokaya, V. G. (2003). *Asili ya Waseuta: Yaani Wazigua, Wasambaa, Wabondei, Wakilindi na Waluvu*. Peramiho: Peramiho Printing Press.

Nurse, D. (2008). *Tense and aspect in Bantu*. New York: Oxford University Press.

Nurse, D. na Phillipson, G. (2003). *The Bantu languages*. London: Routledge

Nyinondi, O. (2013). Tense and aspect in Luguru. (Tasnifu ya Uzamili, M.A Linguistics), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.

Okoa, S. (2012). *Verbal inflection in Hehe language*. Dar es Salaam: University of Dar es Salaam.

O’Leary, Z. (2004). *The essential guide to doing research*. London: SAGE Publications.

Peterson, R. (2008). Baadhi ya vipengele vya uambatizi wa vitenzi katika

Kishambala. *Kioo cha Lugha*. Juzuu 6 uk 52-62. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Prince, A. na Smolensky, P. (1993/2004). *Optimality theory: Constraint interaction in generative grammar*. Rutgers University and University of Colorado at Boulder: Oxford, Blackwell.

Prince, A. (2002). Arguing optimality. Andries, C na Lacy, P (eds). *Papers in Optimality Theory II*. uk. 269-304.

Richards, J.C., Platt, J. na Weber, H. (1985). *Dictionary of applied linguistics*. Harlow: Longman.

Riedel, K. (2009). *The syntax of object marking in Sambaa: A comparative Bantu perspective*. Netherlands: LOT.

Rubanza, Y. I. (1988). Linear Order in Haya Verbal Morphology: Theoretical Implication. (Ph.D. Dissertation), Michigan State University.

Rubanza, Y. I. (1996). *Mofolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Rugemalira, J. M. (1993). Runyambo verb extensions and constraints on predicate structure. (PhD Desertation), Universirty of California: California Digital Library,

Salesio, M. A., Mukuthuria, M. na Matundura S.E. (2016). Uainishaji wa mofimu za kisarufi katika vitenzi vya lugha za mnyambuliko: Mfano kutokana na kitenzi cha Kichuka. *Mara Research Journal of Kiswahili*. Vol,1 pp 37-50.

Spencer, A. (2003). Morphology. Aronoff, M na Rees-Miller, J. (eds), *The Handbook of Linguistics*. UK: Blackwell Publishing Company.

Štekauer, P na Lieber, R. (2005). *Handbook of word formation*. Nertherlands: Springer Publication.

Taherdoost, H. (2016). Sampling methods in research methodology: How to choose a sampling technique for research. *International Journal of Academic Research in Management (IJARM)*, 5, 18-27.

TUKI (1990). *Kamusi sanifu ya isimu na lugha*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI.

Wesana- Chomi, E. (2013). *Kitangulizi cha mofolojia ya Kiswahili*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TATAKI.

Wunderlich, D. (2001). How gaps and substitutions can become optimal: An OT account of argument linking in Yimas. *Transactions of the Philological Society* 99, 315-366.

Yukawa, Y. (1984). *A classfied dictionary of the Shambala language*. Institute for the Study of Languages and Cultures of Asia and Africa (ILCAA). Tokyo: Tokyo University of Foreign Studies.

# VIAMBATANISHO

## KIAMBATISHO A:

## VITENZI VYA KISAMBAA VYENYE MOFU AMBISHI NA MOFU NYAMBULISHI

| KITENZI CHA KISAMBAA | KISWAHILI |
|---|---|
| Ashenigee | asiniwekee |
| Kaonga | hasemi |
| Mshewaaviize | msiwatolee |
| Ushenighambie | usiniambie |
| Kaawa | hatoki |
| Kemuashe | hamtatupa |
| Kewaje | hawatakula |
| Siita | siendi |
| Seniize | sitakuja |
| Kushezigha | huchezi |
| Ketiize | hatutakuja |
| Sija | sili |
| Seniawe | sitatoka |
| nizahaghia | nilifagia |
| senihaghie | sitafagia |
| sihaghie | sijafagia |

| KITENZI CHA KISAMBAA | KISWAHILI |
|---|---|
| taashezigha | tunacheza |
| ketishezigha | hatuchezi |
| tizaghula | tulinunua |
| ketighulie | hatujanunua |
| netisase | tutachanja |
| ketisase | hatutachanja |
| muivutike | mmevimba |
| kemuvutike | hamjavimba |
| mwaashugha | mnafuga |
| kemushugha | hamfugi |
| nemuize | mtakuja |
| kemuize | hamtakuja |
| waaghula | walinunua |
| kewanghula | hawanunui |
| wazashimbuka | walinuna |
| kewashimbuke | hawakununa |
| newafuke | watachimba |
| kewafuke | hawatachimba |
| waang’unda | unalima |
| kung’unda | hulimi |

| KITENZI CHA KISAMBAA | KISWAHILI |
|---|---|
| utanywa | unakunywa |
| kunywa | hunywi |
| uzanywa | ulikunywa |
| kunywee | hujanywa |
| waasuka | ulisuka |
| kusukie | hujasuka |
| aadika | anapika |
| kadika | hapiki |
| atasheusha | anachemsha |
| kasheusha | hachemshi |
| azaasha | alitupa |
| kaashize | hakutupa |
| nishedike | nisipike |
| ushedike | usipike |
| tishishumiyewo | tusiovuna |
| ushishumiyeye | usiyevuna |
| naajata | natembea |
| taajata | tunatembea |
| nitahaka | ninaoga |
| titahaka | tunaoga |

| KITENZI CHA KISAMBAA | KISWAHILI |
|---|---|
| nizamuona | nilimuona |
| tizamuona | tumemuona |
| naaighaa | nilipeleka |
| taaighaa | tulipeleka |
| nionda | natafuta |
| tionda | tunatafuta |
| nighoshoa | nafanya |
| tighoshoa | tunafanya |
| waauya | unarudi |
| mwaauya | mnarudi |
| utaavya | unatoa |
| mtaavya | mnatoa |
| uzaeta | ulileta |
| muzaeta | mlileta |
| neughule | utanunua |
| nemghule | mtanunua |
| aausha | anaondoa |
| waausha | wanaondoa |
| azahaghia | alifagia |
| wazahaghia | walifagia |

| KITENZI CHA KISAMBAA | KISWAHILI |
|---|---|
| aavuziia | alipuliza |
| waavuziia | walipuliza |
| neadike | atapika |
| newadike | watapika |
| atashenga | anakata |
| watauka | wanaondoka |
| utavika | unaomba |
| mtaheta | mnapeta |
| ateoka | alichoma |
| watetongea | walifuata |
| mzabua | mlifika |
| tizazua | tulivua |
| wadikiye | walipika |
| watozize | walishika |
| tiukiye | tuliondoka |
| aiighae | amepeleka |
| muidosize | mmefuata |
| waagona | walilala |
| naahaghasha | nilipapasa |
| netishange | tutachanga |

| KITENZI CHA KISAMBAA | KISWAHILI |
|---|---|
| nenibee | nitabeza |
| newaghue | watachukua |
| neewaete | wataleta |
| neeaize | atakuja |
| uzaniavya | ulinitoa |
| titakuetea | tunakuletea |
| mwaatiink$^{h}$a | mnatupa |
| nenimietee | nitawaletea |
| azamhaka | alimuogesha |
| tizamuasha | tulimuacha |
| muzawaekeeza | mliwasindikiza |
| nemuhahaghie | mtapafagia |
| utachija | unakila |
| waavighula | walivununua |
| titauchunt$^{h}$a | tunauosha |
| mteyashenga | mmeyakata |
| akiiza | akija |
| nikijata | nikitembea |
| wakiima | wakilima |
| tikifuka | tikifuka |

| KITENZI CHA KISAMBAA | KISWAHILI |
|---|---|
| mkibonda | mkibonda |
| aakizinga | anajizinga |
| waakifisha | walijificha |
| netikinyooshe | tutajinyoosha |
| atakitoa | anajikwaa |
| etea | letea |
| shengea | katia |
| sogezea | sogezea |
| ushia | ondolea |
| $zink^hia$ | pitia |
| suguia | sugulia |
| sasia | chanjia |
| tozeeza | shikia |
| fishiiza | fichia |
| hetea | petea |
| zengea | jengea |
| ghookea | simamia |
| hozea | pozea |
| $kont^hea$ | gongea |
| lalia | lalia |

| KITENZI CHA KISAMBAA | KISWAHILI |
|---|---|
| anikia | anikia |
| haghiia | fagilia |
| kindia | zingia |
| ink$^{h}$ia | patia |
| ghuukia | kimbilia |
| hungia | pepelea |
| ukuia | arifu |
| hokwa | pokonywa |
| ekwa | achwa |
| shungwa | fungwa |
| hitulwa | geuzwa |
| inulwa | inuliwa |
| tumbulwa | tumbuliwa |
| ghuighwa | olewa |
| doighwa | guswa |
| ifyighwa | chukiwa |
| dumulwa | katwa |
| fulwa/ fuighwa | fuliwa |
| tibulwa | choshwa |
| ghosholwa | tengenezwa |

| KITENZI CHA KISAMBAA | KISWAHILI |
|---|---|
| togolwa | shukuriwa |
| dolwa/doighwa | shikwa |
| fokolwa | fukuliwa |
| eghulwa | nyolewa |
| honolwa | panguswa |
| tifulwa | tifuliwa |
| zulwa/zuighwa | vuliwa |
| okolwa | opolewa |
| mughushulwa | megwa megwa |
| zuighwa | vuliwa |
| jaighwa | sahauliwa |
| jighwa | liwa |
| avyighwa | tolewa |
| tozighwa/ tozwa | shikwa |
| etighwa/ etwa | letwa |
| ashighwa/ ashwa | tupwa |
| komighwa/ kong’wa | uliwa |
| sonighwa/sonwa | lambwa |
| tekeka | choteka |
| okeka | chomeka |

| KITENZI CHA KISAMBAA | KISWAHILI |
|---|---|
| fyoseka | fyonzeka |
| ikika | wekeka |
| zughaika | fungika |
| haghiika | fagilika |
| tibuka | vurugika |
| ghoshoka | fanyika |
| shengekea | katika |
| memeka | jazika |
| tozeka | shikika |
| ashika | tupika |
| sasika | chanjika |
| ikika | wekeka |
| imika | limika |
| shishika | pakika |
| zutika | vutika |
| umika | ng’atika |
| chunt$^{h}$ika | osheka |
| weeka | angalika |
| tibuka | choka |
| shituka | shituka |

| KITENZI CHA KISAMBAA | KISWAHILI |
|---|---|
| fokoka | chimbika |
| ghoshoka | tengenezeka |
| kupuka | mwagika |
| weeza | fanya aangalie |
| memeza | jaza |
| handiza | fanya apande mbegu |
| vikiza | fanyisha maombi |
| ng’oosha | kimbiza |
| ghoosha | simamisha |
| gonya | laza |
| vutisha | vimbisha |
| izwisha | ivisha |
| uza | rudisha |
| hoza | poza |
| kinya | angusha |
| honya | ponya |
| weeza | angaliza |
| memeza | jazisha |
| koeza | koleza |
| dahiza | fanya aweze |

| KITENZI CHA KISAMBAA | KISWAHILI |
|---|---|
| kandiza | kandisha |
| imiza | limiza |
| vyaza | zalisha |
| inuza | bebesha |
| hituza | geuza |
| ikiza | shusha |
| gwiza | fanya akamatwe |
| dodoza | fanya aokote |
| hunisha | vuta sana |
| umisha | uma sana |
| itangisha | ita sana |
| akisha | waka sana |
| imisha | lima sana |
| vinisha | cheza sana |
| itangiza | ita sana |
| hituiza | geuza sana |
| toesha | piga sana |
| dosesha | fuata sana |
| kemesha | lia sana |
| shengesha | kata sana |

| KITENZI CHA KISAMBAA | KISWAHILI |
|---|---|
| awisha | toka sana |
| akisha | waka sana |
| hakisha | oga sana |
| jiisha | kula sana |
| itikisha | mwagika sana |
| vinisha | cheza sana (muziki/ngoma) |
| puchuisha | nyonyoa sana |
| shungisha | funga sana |
| kwezesha | pandisha sana |
| hetesha | peta sana |
| geesha | tia sana |
| tozesha | shika sana |
| konyesha | kunja sana |
| gonesha | lala sana |
| hakana | ogeshana |
| shengana | katana |
| teiana | juana |
| ighaana | pelekana |
| okoa | epua |
| shungua | fungua |

| KITENZI CHA KISAMBAA | KISWAHILI |
|---|---|
| zunghua | fungua |
| ghubua | funua |
| ateokoewa | ameepuliwa |
| tizaokoeana | tumepuliana |
| waashunguiana | wanafunguliana |
| utazughulwa | unafunguliwa |
| chizaghubulwa | kimefunuliwa |
| nihakiyewo | niliyeoga |
| tishengiyewo | tuliokata |
| uiziyewo | uliyekuja |
| mujatiyewo | mliotembea |
| aghuliyeye | aliyenunua |
| wahaghiyewo | waliofagia |
| chitoziwecho | kilichoshikwa |
| vietiwevyo | vilivyoletwa |
| azaoka | alichoma |
| wazashita | waliziba |
| wazazugha | walisonga |
| aaghula | alinunua |
| tizaja | tulikula |

| KITENZI CHA KISAMBAA | KISWAHILI |
|---|---|
| mwaaiza | mlikuja |
| muzaheta | mlipeta |
| kaokiye | hajachoma |
| kewashitiye | hawajaziba |
| kewazughiye | hawajasonga |
| kaghuliye | hajanunua |
| ketijiye | hatujakula |
| kemuiziye | hamjakuja |
| kemuhetiye | hamjapeta |
| azabadika | alibandika |
| waashimbuka | walinuna |
| mzashezigha | mlicheza |
| aashungua | alifungua |
| tizashimika | tulisimika |
| uzaghubika | ulifunika |
| mwaaanika | mlianika |
| kabadike | hakubandika |
| kewashimbuke | hawakununua |
| kemshezighe | hamjacheza |
| kashungue | hakufungua |

| KITENZI CHA KISAMBAA | KISWAHILI |
| --- | --- |
| ketishimike | hatukusimika |
| kughubike | hukufunika |
| kemuanike | hamkuanika |
| tijiye | tulikula |
| wahakiye | walioga |
| mshezighe | mlicheza |
| tighoshoe | tulitengeneza |
| utaghiye | uliuza |
| agoshize | alilala |
| aushize | aliondoa |
| aitongee | amefuata |
| waihokee | wamepokea |
| tiitange | tumeita |
| muidodoe | mmeokota |
| uimosoe | umenyofoa |
| aiighae | amepeleka |
| muiambize | mmesaidia |
| niiashize | nimetupa |
| tiiuzize | tumerudisha |
| uidosize | umefuata |

| KITENZI CHA KISAMBAA | KISWAHILI |
|---|---|
| muihozize | mmepoza |
| aikonyize | amekunja |
| waitozize | wameshika |
| niikasize | nimepasha |
| muisasize | mmechanja |
| aikiniye | ameanguka |
| waigwiye | wamekamata |
| uikant$^{h}$iye | umefunga nguo |
| muijatiye | mmetembea |
| niiongiye | nimesema |
| tiikomiye | tumeua |
| waikemiye | wamelia |
| nenije | nitakula |
| neuhake | utaoga |
| neazwike | atavaa |
| naatongomaa | ninanyamaza |
| uzamtongea | umemfuata |
| aahuna | alivuta |
| neakaaghae | atakauka |
| neewahye | wataungua |


| KITENZI CHA KISAMBAA | KISWAHILI |
|---|---|
| nechimeme | kitajaa |
| neetibinde | tutamaliza |
| akishesheka | asipocheka |
| wakisheavya | wasipotoa |
| ukisheshama | usipohama |
| tikisheombeza | tusipoomba |
| mkisheavighwa | msipotolewa |
| netiwatongeeze | tutawafuatilia |
| watashaghuana | wanachaguana |
| taatongewa | tulifuatwa |
| mkisheshindikia | msiposukumia |
| waamtoesha | walimpiga sana |
| vizajiika | vimelika |
| muimkemeze | mumemliza |
| titamhakisha | tunamuogesha sana |
| wazaitangiwa | wameitiwa |
| doewa | gusiwa |
| bindiwa | maliziwa |
| ushiwa | ondolewa |
| honoewa | futiwa |

| KITENZI CHA KISAMBAA | KISWAHILI |
|---|---|
| mosoewa | nyofolewa |
| dumuiwa | katiwa |
| gwishiwa | angushiwa |
| hakiwa | ogeshewa |
| ekewa | achiliwa |
| tozewa | shikiwa |
| ashiana | tupiana |
| ghoghoeana | tengenezeana |
| zwikiana | valiana |
| honoeana | futiana |
| waaghuushia | wanafukuzia |
| titaushia | tunaondoshea |
| tizammemezea | tulimjazia |
| aatogoewa | alisifiwa |
| nenihaghiiwe | nitafagiliwa |
| watazughaiana | wanafungiana |
| doseshwa | fuatwa sana |
| shengeshwa | katwa sana |
| hituizwa | geuzwa sana |
| hakishwa | ogeshwa sana |

| KITENZI CHA KISAMBAA | KISWAHILI |
|---|---|
| chishungiwecho | kilichofungwa |
| waavyiyewo | waliotoa |
| aetiweye | aliyeletwa |
| tijiyewo | tuliokula |
| viondiwevyo | vilivyotafutwa |
| waaghuushia | wanakimbizia |
| titaushiizia | tunaondoshea |
| nimmemezee | nishamjazia |
| waimuikizie | wamemshushia |
| newamuuziize | watamrudishia |
| aetiweye | aliyeletwa |
| tijiyewo | tuliokula |
| waingiyewo | walioingia |
| chishungiwecho | kilichofungwa |
| wahaghiyeyo | waliofagia |
| vighuliwevyo | vilivyonunuliwa |

## KIAMBATISHO B:

## RAMANI YA WILAYA YA LUSHOTO NA TARAFA ZAKE




**Chanzo-:** http://lushoto-rise-up.blogspot.com/2017/08/lushoto-mpango-wa-mji-na-ramani-zake.html (2017)